# UHAKIKI LINGANISHI WA KIFANI WA TENZI ZA <u>MIKIDADI NA MAYASA</u> NA <u>SWIFA YA NGUVUMALI</u>

**NA**
**PAUL KARIUKI MUNGAI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**KITIVO CHA SANAA**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

***Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili (M. A.) katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.***

**JULAI, 2005**

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0271460 8

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Paul Kariuki Mungai

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii inatolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Dkt. Kineene wa Mutiso

Mwalimu Mohamed A. Akidah

**TABARUKU**

Kwa wanangu Biancah, Alvin na mapacha Chris na Dan. Pia kwa mke wangu Jane.

## SHUKRANI

Utafiti huu si mchango wa mtu mmoja. Kwa hivyo, sina budi kuwashukuru watu kadhaa ambao wamechangia ufanisi wa kazi hii kwa njia moja au nyingine.
Kwanza namshukuru Maulana kwa kunipa nguvu na uwezo wa kufanya kazi hii. Singeweza bila Yeye. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Kineene wa Mutiso, Mwalimu Akidah pamoja na Dkt. A.I. Al – Asar. Nawashukuru kwa ushauri stadi wenye uzoefu mkubwa ulioniwezesha kufanya kazi hii kuwa namna ilivyo sasa. Mlinifaa si haba kwa kunishika mkono na kunimulikia katika safari hii kwa hekima na ujuzi mwingi.

Shukrani zingine ziwaendee walimu wangu katika Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kutokana na mchango wao maridhawa. Nao ni Dkt. Mwenda Mbatiah, Mwenyekiti wa Idara, Dkt. K. wa Mberia, Mwalimu G. Mungania, Mwalimu H. Mogambi, Prof. Abdulaziz, Dkt. T. M Olali, Mwalimu Mwaliwa, Dkt. Buregeya, Dkt. J. Habwe na Dkt. Mbuthia. Aidha namshukuru Dkt. K. W. Wamitila kwa kunichochea kurudi chuoni ili nianze safari hii.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tuliongoa nanga pamoja. Nao ni Mediatrix Rapando, Assumpta Matei, Njiru Munyi, Veronicah Murimi, Nyambunga Arasa, Julius Mungai, Eddah Wanja, Wepoh Wesa, Kyallo Nguku, F. Kaviti, L. Gakii, Rukiah Swalleh, M. Oichoe, D. Theuri na Were. Nawashukuru kwa ushirikiano wao na mawaidha ya hapa na pale tulipokuwa safarini.

Shukrani zingine ziwaendee marafiki zangu Sammy Njuguna, Paul A.

Nganga, S.I. Nganga, Jackstone Nyonje, Bw. na Bi. Joseph Waweru, Bw. na Bi. Justus Mbugua, Bw. na Bi. Samuel Githongo, pamoja na Bw. na Bi. Nicholas Mugambi kwa ushauri na usaidizi wao wa mara kwa mara.

Nawashukuru baba na mama yangu Bw. John Mungai na R. Wanjiru kwa kunitunza pamoja na kunielimisha kwa mengi. Nawashukuru pia dada yangu Margaret Wanjiku na mumewe Benson Mbugua kwa kunifadhili nilipokuwa masomoni.

Asante mke wangu Jane kwa kuvumilia dhiki na upweke wakati nilipokuwa nikifanya kazi hii. Ulinisubiri kwa hamu ya laili wa nahari hadi nikatia nanga. Licha ya haya, ulijifunga nira na kuhakikisha kuwa nimefanya kazi tangu mwanzo mpaka mwisho. Shukrani wanangu Biancah, Alvin, Chris na Dan. Mlinitia moyo katika safari hii bila ya nyinyi kufahamu. Biancah na Alvin hawakuelewa ni kwa nini nilikuwa ninasoma kama wao. Maswali ya Alvin kama "Dad umefanya homework?" yalikuwa kichocheo kwangu.
Aidha vilio vya Dan na Chris vilikuwa kama timazi ya saa ya kuniamsha na kunikumbusha nikabukue.
Labda sikuweza kuwataja wote mlionitia shime kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote nasema **ASANTE** tena **SANA**.

**KIFUPISHO**

KHJ - Kama hapo juu

M N M - Utenzi wa Mikidadi na Mayasa

S Y N M - Utenzi wa Swifa ya Nguvumali

Taz - Tazama

TUKI- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (Tanzania)

Kiing.- Kiingereza

Uk.- Ukurasa

Rej.- Rejelea

Na.- Nambari

S.A.W. – Swala-llahu Alayhi Wasallam
(amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake)

## MUHTASARI

Tasnifu hii ni juu ya uhakiki-linganishi wa ki-fani wa tenzi za Swifa ya Nguvumali (S Y N M) na Mikidadi na Mayasa (M N M). Utenzi wa M N M ulitungwa na Said Abdallah Masudi el Buhry miaka mingi kabla ya Karne ya Ishirini. Utenzi huu umetafsiriwa kwa Kiingereza na J.W. Allen (1971) lakini haujafanyiwa uhakiki wa aina yoyote. Unasimulia juu ya mashujaa wawili wa Kiislamu, Mikidadi na Mayasa na jinsi walivyoshinda pingamizi walizowekewa na baba yake Mayasa ili wasioane. Utenzi wa SY N M ulitungwa na Bwana Hasan bin Ismail (1968). Umehaririwa na kutarjumiwa kwa Kiingereza na Peter Lienhardt (1968). Utenzi huu umefanyiwa utafiti na Prof. M. H. Abdulaziz (1968), aliyehakiki matumizi ya lugha. Utafiti huo uliendelezwa na E. Kadenge Kazungu (1982) aliyehakiki ukiushi wa kaida za lugha katika utenzi huu. Katika uchunguzi wake, E. K. Kadenge amekipa kipengele cha tamathali za usemi nafasi muhimu. Utafiti wetu umeenda mbali kwa kuvihakiki vipengele vyote vya fani kama vile wahusika, mtindo, muundo, ploti, mandhari na kuvilinganisha katika tenzi husika. Kwa hivyo, tutalinganisha tenzi hizi mbili kifani kwa kuangalia jinsi fani yake inavyolingana au kutofautiana kwa kuzingatia kuwa tenzi hizi zilitungwa kwa nyakati na mazingira mbalimbali.

Mwongozo wetu katika tasnifu hii ni nadharia ya Urasmi ambayo huangalia fasihi kama sanaa ya maneno. Tumelinganisha fani na vipengele vyake katika tenzi hizi mbili kwa kutambulisha kila mojawapo na kuchanganua maana na uamilifu wake katika muktadha wa matumizi.

Kazi yetu imegawanywa katika sura nne. Sura ya kwanza ni utangulizi unaoeleza somo la utafiti, madhumuni ya tasnifu, sababu za kuchagua somo hili, madhumuni ya somo, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, nadharia tete na njia tulizotumia kufanyia utafiti huu. Katika sura hii pia tumerejelea kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusu somo hili.

Katika sura ya pili tumejadili dhana ya fani. Tumeshughulikia vipengele vya fani kwa kurejelea wataalamu na wahakiki mbalimbali pamoja na maoni yetu juu ya kunga hizo. Katika sura ya tatu tumelinganisha kila mojawapo ya vipengele vya fani vinavyojitokeza katika tenzi za M N M na S Y N M.

Sura ya nne ni hitimisho ambapo tumeelezea pale tulipofikia katika utafiti wetu. Katika sura hii pia tumetathimini haipothesia ya utafiti wetu pamoja na kuonyesha kama tumeweza kuifikia au la. Vilevile tumetoa mapendekezo yetu.

**YALIYOMO** **UKURASA**

IKIRARI ........ ii
TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
KIFUPISHO ........ vi
MUHTASARI ........ vii
SURA YA KWANZA ........ 1
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Tatizo la Utafiti ........ 1
1. 2 Sababu Za Kuchagua Somo ........ 2
1.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ........ 3
1.4 Madhumuni ya Utafiti ........ 6
1.5 Upeo na Mipaka ........ 6
1.6 Msingi wa Nadharia ........ 7
1.7 Nadharia Tete ........ 10
1.8 Njia Za Utafiti ........ 10
SURA YA PILI ........ 12
2.0 Utangulizi ........ 12
2.1 DHANA YA FANI ........ 12
2.1.1 FANI NI NINI ........ 12
2.1.2 LUGHA ........ 13
2.2.1 UHURU WA KISHAIRI ........ 19

2.2.1.1 TABDILA ........................................ 20

2.2.1.2 INKISARI ........................................ 20

2.2.2.3 MAZIDA ........................................ 20

2.2.3 TAMATHALI ZA USEMI ........................................ 21

2.2.3.1 TASWIRA ........................................ 22

2.2.3.2 TASHIBIHI ........................................ 23

2.2.3.3 SITIARI ........................................ 24

2.2.3.4 TASHIHISI ........................................ 26

2.2.3.5 METONIMIA ........................................ 26

2.2.3.6 CHUKU ........................................ 27

2.2.3.7 TAKRIRI ........................................ 27

2.2.3.8 TABAINI ........................................ 28

2.2.3.9 BALAGHA ........................................ 28

2.2.3.10 USAMBAMBA ........................................ 29

2.2.3.11 KEJELI ........................................ 29

2.2.3.12 TAHARUKI ........................................ 30

2.2.3.13 MBINU REJESHI ........................................ 30

2.2.3.14 NAHAU ........................................ 31

2.2.3.15 METHALI ........................................ 31

2.2.3.16 ONOMATOPEYA ........................................ 32

2.2.3.17 LITIFATI ........................................ 32

2.2.4 MTINDO ........................................ 32

2.2.5 MUUNDO ........................................ 34
2.2.6 PLOTI ........................................ 34
2.2.7 MANDHARI NA WAKATI ........................................ 36
2.2.8 TONI ........................................ 37
2.2.9 WAHUSIKA ........................................ 38
HITIMISHO ........................................ 39
SURA YA TATU ........................................ 41
3.0 Utangulizi ........................................ 41
3.1 MTINDO ........................................ 42
3.1.1 LUGHA ........................................ 42
3.1.2 LAHAJA ........................................ 42
3.1.3 MSAMIATI WA KIARABU ........................................ 45
3.1.4 MSAMIATI WA KIINGEREZA ........................................ 48
3.2 UHURU WA MSHAIRI ........................................ 50
3.2.1 INKISARI ........................................ 50
3.2.2 MAZIDA ........................................ 51
3.2.3 TABDILA ........................................ 52
3.3 MUUNDO ........................................ 53
3.3.1 VINA ........................................ 54
3.3.2 MIZANI ........................................ 56
3.4 TAMATHALI ZA USEMI ........................................ 58
3.4.1 TASHIBIHI ........................................ 58

3.4.2 SITIARI ........ 63

3.4.3 TASHIHISI ........ 65

3.4.4 METONIMIA ........ 66

3.4.5 CHUKU ........ 66

3.4.6 TAKRIRI ........ 68

3.4.7 BALAGHA ........ 72

3.4.8 TABAINI ........ 76

3.4.9 USAMBAMBA ........ 76

3.4.10 KEJELI ........ 77

3.4.11 TAHARUKI ........ 81

3.4.12 MBINU REJESHI ........ 83

3.4.13 NAHAU ........ 85

3.4.14 METHALI ........ 86

3.4.15 LITIFATI ........ 87

3.4.16 ONOMATOPEYA ........ 90

3.5 PLOTI ........ 91

3.6 MANDHARI NA WAKATI ........ 95

3.7 WAHUSIKA ........ 97

3.8 TONI ........ 104

HITIMISHO ........ 106

SURA YA NNE ........ 107

4.0 HITIMISHO ........ 107

**Utangulizi** ........................................................................................ 107

**4.1 Muhtasari Wa Masuala Muhimu** ................................................ 107

**4.2 Upimaji Wa Nadharia Tete** ....................................................... 111

**4.3 Mapendekezo** ........................................................................... 112

**MAREJELEO** ................................................................................... 114

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Tasnifu hii ni juu ya uhakiki-linganishi wa ki-fani wa tenzi za Mikidadi na Mayasa na Swifa ya Nguvumali. Utenzi wa Mikidadi na Mayasa ulitungwa na Saidi Abdallah Masudi el Buhry. Utenzi huu umetafsiriwa kwa Kiingereza na J. W. T. Allen (1971). Hata hivyo, haujafanyiwa uhakiki wa aina yoyote. Utenzi huu unasimulia juu ya mashujaa wawili wa Kiislamu, Mikidadi na Mayasa na jinsi walivyokabili na kushinda pingamizi walizowekewa na baba yake Mayasa ili wasioane.

Utenzi wa Swifa ya Nguvumali ulitungwa na kusimuliwa na Bwana Hasani bin Ismail. Umehaririwa na kutafsiriwa na Peter Lienhardt (1968). Swifa ya Nguvumali ni utenzi ulioandikwa katika mwaka wa 1968. Unasimulia juu ya kupotea na kifo cha mwanamke katika kijiji kimoja huko pwani ya Afrika Mashariki. Kwa ufupi, utenzi huu ni juu ya uchawi ambao ni kinyume cha dini ya Kiislamu. Tutavihakiki vipengele vyote vya fani vya tenzi hizi kama vile wahusika, mtindo, muundo, ploti , wakati na mandhari na kulinganisha jinsi vilivyotumiwa.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Uhakiki-Linganishi wa ki-fani ni somo ambalo limechunguza fani katika kazi zote mbili na kuzilinganisha katika muktadha wake wa matumizi. Fani ni kipengele ambacho kina uamilifu mkubwa katika sanaa. Sanaa ni ufundi wa hali ya juu wa kuwasilishia mawazo aliyo nayo mtu kwa njia inayoweza kumwathiri anayeona matokeo yake. Kwa hivyo, fani huchukua jukumu la kupitisha ujumbe kwa njia ya umbuji.

Tumehakiki kwa kulinganisha fani ya tenzi za M N M na S Y N M. Utafiti wetu utajaribu kuziba mwanya ulioachwa na watafiti waliotangulia. Watunzi wa tenzi hizi wametumia fani kama malighafi muhimu katika kukidhia mahitaji ya kujenga ujumi. Pengine fani iliyotumiwa kutungia utenzi wa M N M ni tofauti na ile iliyotumika katika S Y N M. Kwa hivyo, kazi hizi hazina budi kuchunguzwa kwa kulinganishwa.

## 1. 2 Sababu Za Kuchagua Somo

Tumechagua mada husika kwa sababu zifuatazo:

i) Kama ilivyo kazi yoyote ya kisanaa, tenzi za M N M na S Y N M zina sifa mahususi ambazo hazina budi kuchunguzwa.

ii) Tunaamini kuwa kuna mengi ambayo hayajachunguzwa kuhusu tenzi hizi

iii) Tuna hamu ya kutaka kuelewa kama kuna tofauti ya kifani kati ya tenzi hizi.

iv) Tumechagua somo hili kwa sababu ya kariha yetu ya kutaka kutoa mchango katika uwanja huu wa uhakiki – linganishi wa ki-fani katika tenzi zinazohusika. Fani ni dhana ni muhimu sana katika fasihi na hutumiwa katika kuelezea mbinu ya kuwasilishia maudhui.

Uchunguzi wetu utakuwa kama changamoto kwa uchunguzi fuatilizi kuhusu tenzi hizi.

Wahakiki wengi wamechangia sana katika uhakiki na uchambuzi wa tenzi mbalimbali. Kwa mfano, mchango wa Dkt. Kineene wa Mutiso wa kuchambua, kutafsiri, kuhakiki na kufasili Kasida ya Burudai (1996), Utenzi wa Fatuma (2002), Utenzi wa Siri li Asirali (2003) na Utenzi wa Hamziyyah (1985 na 2004), pamoja na utafsiri kwa Kiingereza wa tenzi

kadhaa na Lydon Harries (1962). Utafsiri uliofanyiwa utenzi wa M N M na J.W.T Allen (1971) , na uhariri uliofanyiwa utenzi wa S Y N M na Peter Lienhardt (1968) ni mchango madhubuti wa kupanua uelewaji wa tenzi tutakazochunguza. Aidha pamoja uchambuzi wa matumizi ya lugha katika S Y N M uliofanywa na Prof. M.H.Abdulaziz (1968) pamoja na E. Kadenge Kazungu (1982). Kazi hizi hazijatosha kutushawishi kusema kuwa tenzi hizi zimeshughulikiwa vya kutosha. Hii ndiyo sababu iliyotufanya kuchagua somo hili ili nasi tutoe mkono wetu katika uwanja huu wa uhakiki katika tenzi hizo. Utafiti huu hautachangia tu katika uhakiki - linganishi wa tenzi, bali utafungua ukurasa mpya wa uhakiki – linganishi katika sanaa. Vilevile tunatarajia kujaribu kuziba pengo la kuchunguza fani ya tenzi za M N M na S Y N M lililoachwa na watalaamu hawa.

Ni kwa sababu hizi tumeshawishika na kuhamasika katika kuzihakiki kwa kuzilinganisha tenzi hizi. Tumechagua tenzi hizi kwa sababu zilitungwa katika vipindi tofauti vya wakati na kwa hivyo litakuwa jambo la kuvutia kulinganisha fani yake.

## 1.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Kutokana na uchunguzi wetu, tumegundua kuwa mada yetu ya utafiti haijawahi kufanyiwa utafiti wowote. Kwa hivyo, kazi yetu ndiyo ya kwanza kabisa kuwahi kuhakiki – kiulinganishi tenzi zinazohusika. Hata hivyo, kuna kazi za kitaalamu zilizowahi kufanyiwa tenzi mbalimbali kama tutakavyoona hapa chini.

Utenzi ni mada ambayo haijashughulikiwa sana katika utanzu wa ushairi. Wataalamu wengi wa fasihi na isimu wamekwepa somo hili. Hata hivyo, mhakiki kwa jina Kineene wa Mutiso (1985), ameshughulikia maudhui ya

"Hurafa na Uyakinifu" katika Utenzi wa Hamziyyah. Katika kazi hii, ambayo ni tasnifu yake ya Shahada ya Uzamili, amelinganisha sifa apewazo Mtume Muhammadi S.A.W. na zile za mashujaa wengine duniani. Pia amefasiri Kasida yote kwa Kiswahili na kufafanua mtindo wa utenzi huu.Katika waraka huo huo alitafsiri Kasida ya Hamziyyah kwa Kiingereza na kuihakiki pia katika The Hamziyyah Epic: Translation and Commentary.

Mhakiki huyu (KHJ) pia amehakiki Kasida ya Burudai (1996), katika tasnifu yake ya Shahada ya Uzamifu (Ph.D). Ametafsiri Kasida hii kwa Kiingereza na Kiarabu . Pia ameihakiki kwa misingi ya " Archetypal Motifs." Katika kazi hii ameshughulikia suala la fasihi zilizo na misingi ya Kiislamu na ambazo zimeandikwa au kutarjumiwa kwa Kiswahili. Amejaribu kujibu swali ambalo limewasumbua wasomi na wahakiki wengi kwa muda mrefu: Kama fasihi hizo ni za Kiswahili au ni za kigeni. Vilevile katika tasnifu hii ameonyesha jinsi watunzi wa tenzi walivyotunga kwa nia ya kumtukuza Mtume Muhammadi S.A.W. Amejadili pia mtindo wa Kasida ya Burudai. Katika mwaka wa 2002, alitafsiri Utenzi wa Fatuma katika "The Epic of Princess Fatuma." Vilevile ametafsiri Utenzi wa Siri li Asirali katika "Epic of Secret of All Secrets" (2003).
Katika mwaka wa 2005, alishughulikia Kasida ya Hamziyyah ambapo ameifasiri kwa undani zaidi, alihakiki fani yake katika "Tarjumi, Maelezo na Uhakiki." Kazi ambayo imechapishwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Tanzania.

Mtaalamu huyu amejitahidi na kupiga hatua kubwa katika kuchunguza tenzi ambazo E. Kezilahabi (1983:148) analalamikia kuwa " *hazisomwi sana siku hizi."* Kwa hivyo, kama hazisomwi sana ni kumaanisha kuwa

hazishughulikiwi. Kwa kuzisoma tenzi hizi na kuzihakiki kwa jicho la ndani, Kineene wa Mutiso amechangia pakubwa katika kuzitoa kwenye giza la sahau na vilevile kuzua mtazamo mpya kwa wasomi na wahakiki ambao wamezionyesha kisogo kwa muda mrefu . Tenzi zimehusishwa na ugumu na ukale kutokana na lugha yake. Vilevile zinaonekana na wasomi wengi zikiwa na Uarabu na Uislamu mwingi na kwa hivyo kuachiwa wanaojua Kiarabu na wenye dini ya Kiislamu. Chambilecho E. Kezilahabi:

> " *Kwa baadhi ya maandishi, hasa yale yenye athari kubwa ya Kiarabu, huwa vigumu kusema kama mwandishi aliandika kwa uasili wake mwenyewe au alikuwa akijaribu kukumbuka shairi fulani la huko alikotoka."* (1983:147).

Katika kuondoa utata huu tenzi hizi zinafaa kufanyiwa uchunguzi na uhakiki wa kina na wataalamu mabalimbali ili ziweze kueleweka kwa urahisi zaidi.

Lyndon Harries (1962) ameshughulikia tenzi mbalimbali kwa kuzitafsiri na kuzihariri kwa Kiingereza. Utafiti wake haukugusia tenzi tunazochunguza. Ameshughulikia tenzi kama, Mwana Kupona, Ras-al-Ghuli, Inkishafi, Utendi wa Hati, Adili na Liyongo. Vilevile ameshughulikia mashairi mengine. Naye Kithaka wa Mberia (1989), aliuhakiki utenzi wa Fumo Liyongo ambapo ameonyesha Liyongo kama shujaa.

Kazi nyingi zilizoandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza zimeshughulikia fani siyo tu katika ushairi bali katika fasihi kwa jumla. Baadhi ya kazi hizo zimeshughulikia fani katika baadhi ya vipengele vyake tu.

Tumesoma kazi hizo na kuchukua vipengele vinavyofaa katika kuhakiki tenzi za S Y N M na M N M. Kwa Kadiri ya uelewa wetu tenzi hizi hazijashughulikiwa kwa upande wa fani, isipokuwa uchambuzi wa matumizi ya lugha katika S Y N M uliofanywa na Prof. M.H. Abdulaziz (1968).E. Kadenge Kazungu (1982) alishughulikia ukiushi wa lugha iliyotumika katika utenzi huo. J.W.T Allen (1971) ametarjumi Utenzi wa M N M kwa Kiingereza. Peter Lienhardt (1968) amehariri utenzi wa S Y N M na kuutafsiri kwa Kiingereza.

Uchambuzi uliofanyiwa S Y N M na Prof. H.M. Abdulaziz pamoja na ule wa E. Kadenge Kazungu hautoshi kwa sababu walishughulikia kiungo kimoja tu cha fani. Kwa hivyo, tungependa kujaribu kuziba pengo waliloacha kwa kuhakiki vipengele vya fani iliyotumika kwa upana zaidi. Kwa njia hii tutatoa mwangaza zaidi kuhusu fani na vipengele vyake na namna vinavyofanana au kutofautiana katika tenzi hizo.

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni yetu katika utafiti huu ni kuchanganua fani ya tenzi hizi.

Kuonyesha ama udhaifu au ufanifu na uamilifu wa kila kiungo cha fani katika muktadha wake wa matumizi.

Ni matumaini yetu kuwa utafiti wetu utachangia pia kupanua njia za uhakiki wa kifani na kwa hivyo kuvutia uhakiki zaidi wa tenzi ambazo zimepewa mgongo na wahakiki pamoja na wasomi wengi wa sanaa kwa muda mrefu.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Tumeshughulikia na kulinganisha fani na vipengele vyake, ambavyo ni matumizi ya lugha, mtindo , wahusika , ploti , muundo , wakati, mandhari

na toni katika tenzi za M N M na S Y N M. Hatukushughulikia Hadithi ya Miqdadi na Mayasa iliyotafsiriwa kwa Kiingereza na Alice Werner (1932) kwa vile muda tulionao wa kufanya kazi hii ni mfupi. Aidha tulichagua utenzi wa M N M ulioandikwa na Saidi Abdallah Masudi el Buhry kwa sababu ni utenzi mrefu-wenye beti 778 na kwa hivyo tunaamini kuwa una mengi ya kushughulikiwa. Hadithi ya Miqdadi na Mayasa iliyotafsiriwa na Alice Werner (1932) ni fupi (beti 161) na ambayo inasimulia kisa tofauti kabisa na kile kilichopo katika utenzi wa M N M.

Tumeshughulikia fani katika tenzi hizi. Tumechunguza kila mojawapo ya viungo vyake ama udhaifu au ufanifu pamoja na uamili wake katika muktadha. Uamili huu ndio uliotuwezesha kutathmini fani iliyotumiwa.
Ni sharti tutaje hapa kuwa haingewezekana kuzungumzia wahusika bila kutaja masuala wanayowakilisha. Tumegusia masuala hayo kijuujuu pale ambapo ilitubidi kutoa mwanga zaidi juu ya wahusika. Aidha somo hili halikushughulikia maudhui lakini pale ambapo tulilazimika kuyataja tumefanya hivyo katika kufafanua kiungo cha fani kinachohusika. Kama tulivyosema hapo awali tenzi hizi zimeshughulikiwa kwa kiasi kidogo sana na kwa hivyo kutupa ufinyu wa kurejelea kazi zilizofanywa hapo mbeleni. Vilevile somo hili halikujishughulisha na falsafa ya watunzi au historia yao. Hii ni kwa sababu ya muda tuliokuwa nao wa kufanya kazi hii.

### 1.6 Msingi wa Nadharia

Nadharia tuliyotumia katika utafiti ni ile ya Ufani au Urasimu.
Ufani ni nadharia ambayo ina uhusiano wa karibu na isimu. Kimani Njogu na Rocha Chimerah (1999:9) wanadai kuwa urasimu ni wakati maalum ambapo msingi wa kazi ya sanaa huwekwa na kukubalika na wanajamii

kwamba ndiyo mizani bora kwa kazi nyingine katika muktadha wa jamii hiyo. Kutokana na madai hayo tunaweza kusema kuwa nadharia hii huchunguza kama kazi fulani ya kisanaa imefuata mtindo uliozoeleka na jamii husika.

Uhakiki wa kifani hukaribiana sana na uhakiki wa kiisimu. Uhakiki huu hujikita hasa katika vipengele vya kiisimu vya kazi ya kifasihi. Vipengele hivyo ni kama vile silabi, vina / sauti, mofimu, mizani, na kadhalika. Hivyo ndivyo baadhi ya vipengele vya fani ambavyo nadharia hii hushughulikia.

Uhakiki huu pia hujishughulisha na mbinu mbalimbali za usimulizi au matukio. Jinsi ambavyo visa mbalimbali vinavyoanishwa ili kujenga hadithi moja. Aidha kuhusiana na wahusika , jinsi wanavyohusiana hasa katika kiwango cha familia. Lengo kuu la kushughulikia vipengele hivi ni kujaribu kubainisha stadi mbalimbali zinazotumiwa katika kubuni hadithi.

Kwa mujibu wa K.W. Wamitila (2003:190), nia ya wanaurasimu ni kuitazama fasihi kama sanaa ya maneno kuliko kama akisicho la jamii. Hamu yao katika ushairi ilikitwa kwenye ushairi wenyewe bali sio mshairi au msanii anayehusika. Walishughulikia maana ya kazi maalumu za kifasihi wala sio chimbuko wala athari zake kwa msomaji.

Walitaka kuchunguza sifa zinazoipa kazi ya kifasihi upekee wa kutambuliwa kama kazi ya kifasihi. Kwa kuzibainisha sifa za fasihi, hali hii ingeweka mpaka wazi kati ya fasihi na taaluma nyinginezo kama saikolojia wasifu, historia, na kadhalika.

Katika nadharia hii, dhana ya mizani huchukuliwa kama sifa mojawapo kuu ya kimuundo katika viwango mbalimbali vya lugha ya kishairi na ambayo

inachangia pakubwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya sauti na maana katika shairi.

Wanadai kuwa fasihi inaajinabisha vitu ambavyo vimekuwa vya kawaida au kidesturi katika maisha yetu na kuvifanya vionekane kama vigeni. Katika ushairi lugha ya kawaida inaajinabishwa na baadhi ya maneno hupewa sifa zinazoyakuza na kuyachimuza yakawa waziwazi.

Nadharia hii inachukulia kuwa lugha ya kishairi hutofautiana na lugha ya kawaida kutokana na matumizi yake ya mbinu mbalimbali kama wizani na mizani. Mbinu hizi kwa kiasi kikubwa zinaunda maneno haya upya. Nadharia hii haitilii uzito wowote kwenye maana ya kazi ya kifasihi.

Mwelekeo wa wana-urasimi wa kujihusisha na sifa za ufasihi unaishia kuusababisha uchunguzi wa tanzu za kifasihi. Haiwezekani kulizungumzia suala la ufasihi pasi na kuziangalia tanzu za kazi zinazohusika. Tanzu hizi zinatofautishwa kimisingi na mbinu zilizotumiwa pamoja na uajinabishaji. Kwa mfano, ushairi unaishia kukiuka misingi ya kisemantiki na kuchochea maana nyinginezo za neno fulani.

Mbinu zinazochunguzwa katika nadharia hii ni kama jazanda, chuku, usambamba, ulinganishi na urudiaji. Mbinu hizi huchunguzwa ili kubainisha uwezo wake katika uajinabishaji. Dhana ya hadithi na msuko pia huchunguzwa.

Kwa muhtasari ni kuwa nadharia hii inajaribu kuitathmini fasihi kwa kuchunguza fani yake kisayansi kwa namna inavyojengwa na namna

inavyotekeleza kazi yake ili kuleta maana. Mwelekeo huu wa kuitalii fasihi kisayansi kwa kushughulikia vipengele mahususi vya kifani ulipelekea wasanii kuafikiana kuwa sifa za kijamii ni za kijumla.

Kilichotufanya kuchagua nadharia hii kama mwongozo wa somo hili ni sababu imejikita sana katika ushairi. Nadharia hii inaelekea kuegemea sana upande wa fani katika ushairi. Haya ndiyo mambo yaliyotuvutia katika kutumia nadharia hii katika utafiti wetu.

## 1.7 Nadharia Tete

i) Tunatazamia kwamba uteuzi pamoja na matumizi ya vipengele vya uandishi walivyotumia watunzi wa tenzi hizi vimechangia katika ama ufanifu au udhaifu wa kazi hizi.

ii) Fani ya tenzi hizi inafanana licha ya kutungiwa katika mazingira na nyakati tofauti.

iii) Uteuzi wa msamiati na tamathali za usemi katika tenzi hizi umefanywa kwa malengo maalum.

## 1.8 Njia Za Utafiti

Kimsingi, uchunguzi wetu ni wa maktabani. Kwanza tumezisoma tenzi hizi ili tuwe na nguzo kamili ya kuzifanyia uhakiki.

Utafiti huu vilevile ulilenga kupitia kazi za waandishi, wahakiki na wataalam mbalimbali maktabani na kwingineko. Tumedurusu kazi ambazo zinafaa kwa kututolea mwongozo bora wa kuchambulia na kuhakikia –kiulinganishi fani katika tenzi za M N M na S Y N M. Tumesoma vitabu, majarida na makala ya waandishi wengine ambayo yana uhusiano na mada tuliyochunguza. Vilevile tumetilia maanani mwongozo tuliyopewa na

wasimamizi wetu pamoja na wataalamu wengine. Baada ya hayo tumekusanya na kuweka data yetu pamoja.

# SURA YA PILI

## 2.0 Utangulizi

Madhumuni ya sura hii ni kuchunguza na kufafanua dhana ya fani. Kuna umuhimu wa kuelezea maana ya fani kabla ya kushughulikia matumizi yake katika tenzi zinazohusika. Tutatekeleza haya kwa kuchunguza vipengele vyake, maana ya kila mojawapo na uamilifu wake kwa mujibu wa wataalamu na wahakiki mbalimbali. Maoni na maelezo tutakayokusanya kutoka kwa wataalamu hawa, pamoja na yale tutakayotoa yatatuongoza kwa kutupa mwanga zaidi juu ya sifa za fani na hivyo kutuelekeza katika kueleza fani.

Dhana ya fani ni somo ambalo ni pana mno. Tutashughulikia vipengele vya fani vinavyojitokeza katika tenzi za M N M na S Y N M. Tutafafanua kila mojawapo ya vipengele hivyo huku tukizingatia uamilifu wa kila mojawapo katika sanaa. Katika sura hii, hatutahusisha fani na utenzi au tenzi zenyewe, bali tutaielezea tu kivyake. Hatutafuata utaratibu wowote katika kufanya hivyo.

## 2.1 DHANA YA FANI

### 2.1.1 FANI NI NINI

M. Msokile (1993:57), Kineene wa Mutiso (2005:33), F. E. M. K.Senkoro (1982:8) na K. W. Wamitila (2003:92), wanadai kuwa fani ni jumla ya mbinu, ufundi na nyenzo za kisanaa ambazo hutumiwa katika kuwasilishia ujumbe au maudhui katika fasihi. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, viungo vya fani ni lugha, umbo, muundo, wahusika, mandhari, ploti, mtindo, wakati na toni.

Maoni yetu ni kwamba, madai hayo yanaafiki katika kuelezea dhana ya

fani kwa sababu yanajumulisha ufafanuzi wake pamoja na vipengele vyake. Hivyo basi, fani katika sanaa huwa ni pamoja na viungo ambavyo, kwa kushirikiana na tamathali za usemi, husaidia katika kufanikisha kazi husika kwa kuiwasilisha kwa njia ya umbuji. Fani hubeba kunga muhimu za utunzi ambazo katika sanaa, mbinu hizo hujenga maudhui na ujumbe wa shairi na vilevile kulipa umbo lake la ndani.

Ubora wa kazi yoyote ya kisanaa hutegemea jinsi fani yake ilivyotumiwa katika kuwasilisha kazi hiyo. Kwa hivyo, fani ni kipengele muhimu sana katika ujenzi wa kazi yoyote ya kisanaa.

Baada ya kuelezea maana ya fani, tumefafanua kila mojawapo ya vipengele vyake hapa chini.

### 2.1.2 LUGHA

Katika kijisehemu hiki, tumeshughulikia dhana ya lugha ya kifasihi. Hatukushughulikia lugha kwa jumla. Tumeangalia jinsi lugha inavyotumiwa katika fasihi na lengo lake katika matumizi hayo. Kwa kufanya hivyo, tumejikita sana katika utanzu wa ushairi. Kwa mintarafu hiyo, tumelazimika kuchunguza lugha ya ushairi kwa kuitofautisha na lugha ya nathari.

B.Syambo na A. Mazrui, (1992:Vii), wanadai kuwa, lugha ya fasihi huwa na lengo la kuchochea fikra na hisia za binadamu. Maoni yao ni kuwa

"*Mwandishi mzuri ni yule*
*anayeweza kutumia msamiati,*
*tamathali za usemi, na miundo*
*mingine. Lugha hufanya msomaji*
*awe na hisia fulani – hasira,*
*furaha, huzuni, huruma,*

*kuhusu tabia na vitendo vya*
*wahusika wake na matokeo ya maisha yao."*

Kutokana na madai haya, wataalamu hawa wanaendelea kushikilia kuwa lugha hutumiwa katika fasihi kwa malengo maalum. Malengo hayo ni pamoja na kujengea hadhira picha za aina mbalimbali kwa nia ya kuchochea hisia au fikra zake.

Naye K.W. Wamitila (2003:96), anadai kuwa

*"Katika uandishi wa kazi za kifasihi,*
*lugha ni nyenzo kuu na muhimu sana.*
*Dhamira na maudhui hayawezi*
*kuwasilishwa bila ya lugha.*
*Kimsingi, matumizi ya lugha huhusisha*
*tamathali za usemi, uteuzi na*
*mpangilio wa maneno, matumizi*
*ya nahau, methali, msamiati na kadhalika."*

Kwa hivyo, dhana ya lugha ina kazi muhimu ya kuwasilisha dhamira na maudhui kwa kutumia tamathali za usemi kama uteuzi wa lugha unaofaa katika sanaa. Msanii anastahili kuteua msamiati unaofaa katika muktadha wa kazi yenyewe na pia katika kuleta athari anayokusudia. Wakati mwingine athari zisizokusudiwa na mwandishi huzuka. Hali hii inaweza kutokea pale ambapo msamiati ulioteuliwa huwa na maana zaidi ya moja. Maana hizo tata huenda pia zikaafiki muktadha unaohusika na kwa hivyo maana hizo huenda zikasababisha mtafaruku kwa hadhira. Muktadha ni muhimu katika kutanzulia utata wa maana katika neno. Umuhimu wa

neno hutegemea mazingira.

Athari iliyokusudiwa kwa msamiati fulani hupatikana katika muktadha wa neno hilo.

Kwa mujibu wa Geoffrey N. Leech (1969:5), lugha ya ushairi inaweza kuwa na sifa kadha wa kadha. Mtaalamu huyu ameorodhesha sifa tatu za lugha hiyo: Kwanza, lugha ya ushairi inaweza kukiuka au kupuuza kaida zinazopatikana na katika lugha ya nathari kwa njia nyingi tofauti, zingine za kawaida na zingine za umbuji. Anapendekeza kuwa ukiushi na upuuzaji huo wa kaida za lugha huhitaji kuchunguzwa ili ujulikane aina zake pamoja na madhumuni ya kukiuka kanuni zake.

Pili, mtunzi hasa wa shairi huwa na uhuru wa aina fulani wa kutumia lugha miongoni mwa watunzi wa lugha, ambao unaweza kuwa ni juu ya vyombo vya mawasiliano bila kujali masuala yake ya kimuktadha, ya kijamii na ya kihistoria. Hii inamaanisha kuwa, mshairi anaweza kuchota lugha ya kizamani, akope kutoka kwingine au achote lugha ambayo si ya kisanaa. Madai hayo yanapigiwa mwangwi na Kineene wa Mutiso (2005:34) anaposema kuwa "*. . . mtunzi huketi na kubukua kwenye*

*makamusi na mabuku ya lugha na*
*kukusanya maneno yaliyochakaa na*
*kusahauliwa na wazee walio 'mabingwa wa lugha.'*
*Baada ya kupata maneno ya kutumia,*
*hatua ya pili ni kutumia, 'uhuru wa*
*shairi' kupita kiasi.*
*Neno moja linavyalizwa na*
*kuvyalizwa kiasi cha kuchosha na*

*kupoteza ladha."*

Kutokana na madai ya mtaalamu huyu, uhuru wa mshairi unapotumiwa kupita kiasi, huenda ukakosesha shairi utamu wake.Tunaunga mkono madai hayo kwa kuwa neno likivyalizwa kupita kiasi huenda likazua maana zingine ambazo hazieleweki na hadhira, ila mtunzi mwenyewe.

Tatu, G.N. Leech (KHJ) anaendelea kudai kuwa, msanii ana uhuru wa kutumia tamathali za usemi kama vile kinaya na jazanda. Kwa maoni yetu, madai haya hayatofautishi lugha ya ushairi na lugha ya kawaida kwa sababu wazungumzaji hutumia tamathali za usemi katika maongezi yao ya kila siku. Hata hivyo, mapambo yanahitajika ili kulifanya shairi livutie hadhira. Maoni haya yetu yanaelekea kukubaliana na yale ya Kithaka wa Mberia (1987: 15), anayedai kuwa mojawapo ya sifa muhimu za fasihi ukiwemo ushairi ni ile hali ya kuwasilisha fikra, hisi, mawazo, tajriba na kadhalika. Kwa lugha ya fasihi inayovutia na kupendeza msomaji au msikilizaji. Kupendeza huko kwa lugha ya fasihi kunatokana na sababu ya lugha kutumiwa kisanaa. Mojawapo ya sifa za lugha iliyotumiwa kisanaa ni urembo wake ikilinganishwa na lugha ya mazungumzo au maandishi yasiyo ya kifasihi.

Maoni hayo yote yanatiliwa nguvu na K.W. Wamitila (2002:99), anayedai kuwa mshairi ana uhuru wa kupindua miundo ya sentensi au ki-sintaksia kwa kusudi la kupata upatanifu wa kiarudhi au kwa sababu za kibalagha. Tunapogeuza muundo wa sentensi wa kawaida husisitiza kinachotangulia au kuja mwanzoni. Huwa ni njia ya ukuzaji. Kitu kinachotangulia kinahimizwa na kutiliwa maanani. Kwa mujibu wa maoni hayo, msanii

hufanya ukiushi kwa lengo mbalimbali. Tumechunguza nia ya kufanya hivyo katika sehemu ya tatu.

## 2.2.0 MSAMIATI KATIKA USHAIRI

Mtunzi wa kazi ya kishairi ana uwezo na uhuru wa kuchota msamiati wake kutoka asili nyingi. Hali hii hutupa aina za kunga za uhamishi ndimi, mchanganyo wa ndimi na tadmini. Baadhi ya mbinu hizo huwasilishwa kimofolojia, kifonetiki, kisemantiki na baadhi hutumiwa kiasi cha kutoweza kutambulika kuwa zina asili ya kigeni.

Mtazamo wa msamiati wa ushairi kiwakati ni muhimu katika kutuwezesha kutambua kama maana zao asilia zimehifadhiwa, kupotea au hata kuongezeka. Jambo hili lafaa katika kuchunguza maendeleo yaliyofikiwa kisanii. Kuna msamiati mwingi wa kiasili uliohifadhiwa, mwingine umepanuka kimaana, huku mwingine ukipotea kwa sababu za kihistoria, kiisimu, na kadhalika. Msamiati kama mtima, ng'andu, vitimbi, hadi sasa wahifadhi maana zao. Msamiati kama sono, nyono, zitono, karaba, tindikano, mtelo na mwingine mwingi hautumiki sana ila katika lugha ya ushairi (Donald O. Osiemo, 1997:17).

Washairi, kwa jumla, wana tabia ya kukusanya na kutumia msamiati wa kale katika ushairi wao, kama anavyodai Kineene wa Mutiso (2004:42). Jambo hili linayafanya mashairi yawe magumu kueleweka na wasomaji au hadhira yake. Mtunzi wa shairi anaweza kutumia msamiati mbaya au mzuri. Kama asemavyo K.W. Wamitila (2002: 108), uchunguzi wowote wa ushairi hauna budi kuliangalia suala la msamiati. Uchunguzi huu haupaswi

kujifunga kwa neno au maneno fulani maalum kipekee, bali unapaswa kuangalia uteuzi wa maneno au msamiati katika ujumla wake. Kwa mfano, Kineene wa Mutiso (1986b:36), katika shairi lake la "Lugha Zetu" ameteua msamiati kutoka kwa jamii mbalimbali. Uteuzi huu unamfanya msomaji kufurahia ubunifu wa shairi na kujifunza msamiati wa lugha mbalimbali za Kiafrika. Kama wasomaji, tunatarajia kuona udhabiti fulani katika uteuzi wa msamiati, kama unavyojitokeza katika shairi hilo.

Hii ni sifa mojawapo inayochangia kuuvyanza mtindo wa msanii fulani. Kwa mfano, tunapochunguza ushairi wa Kithaka wa Mberia (1997:7, 13), tunaona mashairi yaliyo na umbo la nyumba, ndege mboga, na wanyama. Umbo ambalo huleta dhamira na maudhui ya ushairi huo. Hali hii inaonyesha nguvu na uamilifu wa kimaana katika mtindo uliotumika kuwasilishia kazi fulani ya kifasihi.

Kutokana na uhuru wa kishairi, katika kiwango cha fonolojia na mofolojia, baadhi ya maneno hupata vipashio vya ziada (mazida), hupunguzwa (inkisari), au hubadilishwa (tabdila). Kwa kufanya hivyo, maana hubadilika katika baadhi ya matumizi. Jambo hili hufanyika kila wakati bila kujali matokeo. Vipashio vingine huwa havikutarajiwa na havifai katika matumizi. Vipashio vya aina hii huleta uhitilafiano wa mpangilio wa mizani katika neno. Hivyo hupotosha maana na kulegeza nguvu za neno au hata kulikosesha maana kabisa. Baadhi ya maneno si rahisi kupata maana yake kutokana na kuongezewa au kubadilishwa kwa vipashio.

Uchunguzi wa viambajengo ni muhimu sana kwani huongoza mhakiki na msanii katika kutambua sio tu vina na idadi ya mizani, bali pia aina za

bahari za tungo hizo. Hali hii hukusudia katika uainishaji wa tungo hizo.

### 2.2.1 UHURU WA KISHAIRI

Kwa mujibu wa S. C. Gonga na wengine, katika Mulika Na. 16:67, uhuru wa ushairi kama *"kutumia miundo msamiati au kuweza mpangilio wa lugha isiokuwa sanifu bila ya kutoka nje ya msingi wa lugha inayohusika, kwa mfano, kutumia "mbene" badala ya "nimeona."*

Naye Dyden [katika M.H. Abrams, (1957:133)] anadai kuwa uhuru wa ushairi ni "*uhuru ambao washairi hujipatia, katika vizazi vyote, kwa kuzungumzia mambo ya ushairi yaliyokiuka kaida za nathari ."*
(Tafsiri na msisitizo ni zetu)

Maoni yetu ni kuwa uhuru wa ushairi ni aina ya uhuru ambao mshairi hujipatia anapotunga kazi fulani. Uhuru huu unampa fursa ya kukiuka kaida za lugha ya kawaida katika viwango vya kimuundo, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na hata kileksika.

Matumizi haya ya lugha hukusudiwa kuipa kazi ya kishairi nguvu za ujumi. Madhumuni yetu katika kijisehemu hiki ni kuchunguza jinsi uhuru huo umetumiwa katika tenzi za M N M na S Y N M, pamoja na uamilifu wa matumizi hayo.

#### 2.2.1.1 TABDILA

Kineene wa Mutiso (2005:55), Kithaka wa Mberia (1987:22), na S. M. Kuvuna na wengine (1992:9) wanasema kuwa tabdila ni kunga ya utunzi ambapo mtunzi hubadilisha sauti fulani katika neno ili kuleta uwiano fulani. Anaweza kubadilisha vitamkwa katika neno mwishoni mwa kipande cha mshororo, yumkini kwa nia ya kupata urari wa vina vinavyotakikana. Uhuru huu wa kubadilisha mpangilio wa sauti katika neno unakubalika katika ushairi.

#### 2.2.1.2 INKISARI

Kithaka wa Mberia (1987:18), Kineene wa Mutiso (2005:54), na S.M. Kavuna na wengine (1992:8), wanasema kuwa hii ni mbinu ya kufupisha maneno fulani kwa madhumuni ya kupata ulingano wa idadi wa mizani inayohitajika. Aina nyingine ya inkisari ni kuunganisha maneno mawili baada ya kuondolea mbali baadhi ya silabi za mojawapo ya maneno hayo. Maoni yetu ni kwamba mtunzi hutumia mbinu hii kwa lengo la kupata urari wa vina katika mshororo.Hivyo basi hudumisha mdundo wa shairi.

#### 2.2.2.3 MAZIDA

Kwa mujibu wa Kineene wa Mutiso (2005:54), S.M. Kuvuna na wengine (1992:9), na Kithaka wa Mberia (1987:20), kunga hii ni kinyume cha inkisari ambapo mtunzi hurefusha neno kwa kuongezea sauti ili kupata idadi ya mizani inayohitajika. Mbinu hii hutumiwa pale ambapo mtunzi amepungukiwa na mizani katika mshororo.

Mtunzi wa shairi hupunguza, huongezea au hubadilisha sauti ya maneno kwa nia tulizozitaja hapo juu. Uhuru wa mshairi humsaidia katika kukuza

na kupamba kazi yake kwa njia ya ubunifu ili kumvutia msomaji au msikilizaji wake.

### 2.2.3 TAMATHALI ZA USEMI

Kwa mujibu wa M. Mbatiah (2001:77) tamathali za semi ni *"Ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (Semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo, mifano ya aina ya tamathali ni kama vile sitiara , metonimia, tashibiha, chuku, majazi na kikinzani."*

Nao S.M. Kuvuna na wengine (1992:21), wana unga mkono kauli hiyo kwa kusema kuwa *"Tamathali za usemi ni mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika maandishi au mashairi kwa nia ya kuongeza maana kwenye lugha na fikra za mashairi au maandishi."*

Maoni haya ya S.M. Kuvuna na wengine yana upungufu kwa sababu hayaelezei kwa uwazi kabisa namna lugha ya tamathali hutumika katika utunzi.

K. W. Wamitila (2003:17) anasema tamathali za usemi hutumiwa kuelezea fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiulejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine . Mtaalamu huyu vilevile ametoa baadhi ya mifano ya tamathali za usemi ambazo hakuna haja ya kuzinakili hapa. Vilevile mtaalamu huyu (2002:103) anadai kuwa ushairi ni sanaa moja ambayo hutumia lugha kwa ufanifu mkubwa ikilinganishwa na tanzu zingine. Lazima mtunzi atumie mbinu za kiutunzi zinazomwenzesha kuyasema mengi kwa maneno machache.

G.N. Leech (1969:50) na Kithaka wa Mberia (1987) wameainisha tamathali kadhaa na kuelezea jinsi zinavyoamili katika miktadha mbalimbali. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, tofauti za kunga zinazoelekea kufanana zinadhihirika.

Baada ya kuelezea maana ya tamathali za semi, tutafafanua kila mojawapo ya vipengele vyake.

### 2.2.3.1 TASWIRA

M. Msokile (1993:60), Kineene wa Mutiso (2005:64), Kithaka wa Mberia (1987:6), S.M. Kuvuna na wengine (1992:25), K.W. Wamitila (2003:225) na F.E.M.K. Senkoro (1982:36), wote wanadai kuwa taswira ni picha ya mahali, wazo, dhana, kitu au uzoefu wa jamii fulani. Picha hii ambayo huibua hisi huchorwa mawazoni mwa msomaji au msikilizaji kwa kutumia lugha. Matumizi ya taswira mara nyingi huambatana na yale ya ishara. Ishara ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na washairi na waandishi mbalimbali katika kazi zao kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine.

Kupitia kwa picha hii, msomaji huhisi, hugusa, hunusa, huoja, au huona yanayoendelezwa. Msanii hutumia nguvu za maneno kusawiri picha akilini mwa hadhira. Huchora picha wazi inayoweza kuonekana na hadhira na ambayo huteka hadhira kiasi cha kufanya kusahau kama inasikiliza au kusoma.

Taswira huibua hisi zinazomfanya mhusika wa kazi fulani ya fasihi kuwa na msukumo wa kutenda kitu fulani. Anaweza kuamua kuteta, kupiga kamsa

kupigana au kujiepusha. Vitendo atakavyotenda mhusika ni matokeo ya msisimko alioupata iwe ni huzuni, chuki, hasira, kinyefunyefu, na kadhalika.

Taswira huibuka kutegemea uteuzi wa maneno ya mtunzi. Utenzi huo ni muhimu kwa sababu picha zinaweza kutabirika kwa njia tofauti kutegemea jamii husika. Ni kazi ya fanani kwa mtunzi kupanga taswira zake ili kujiepusha na utata unaoweza kuzuka kutegemea maneno aliyotumia. Kama anataka hadhira ifikie hitimisho fulani alilotarajia. Ni vizuri ieleweke kuwa katika taaluma ya fasihi, taswira si lazima zihusishwe na kitu fulani maalum tu. Taswira zinaweza kufafanulika kwa njia nyingi tofauti kwa kutegemea utamaduni, siasa, elimu na historia ya jamii. Jambo hili linakubalika kabisa.

Taswira zinaweza kuundwa kutokana na mbinu si haba za kisanaa, kama vile, semi, maelezo, taashira, tashibihi, balagha, takriri, istiari, na zingine nyingi kama tutakavyoona baadaye.

### 2.2.3.2 TASHIBIHI

Hii ni tamathali ya usemi ambayo hufananisha vitu viwili kwa njia ya moja kwa moja. Kineene wa Mutiso (2005:58), S. M, Kuvuna na wengine (1992:24), Kithaka wa Mberia (1987:2), K.W. Wamitila (2003:122), Mwenda Mbatiah (2001:79), M. Msokile (1993:60), F.E.M.K. Senkoro (1982:14) S.C.Gonga na wengine katika Mulika Na. 16:71, na G.N. Leech (1969:156), wote wametoa maelezo yanayokubaliana juu ya tashibihi. Wanasema kuwa tashibihi ni tamathali ya usemi ambapo hali au vitu viwili hulinganishwa kwa njia ya waziwazi kwa kutumia maneno: **Kama, mfano**

**wa, kulingana na, kuwa sawa na, -nga, kama vile, mithili ya, ja, fanana na, mathalani** na kadhalika. B. Syambo na A. Mazrui wanaafikiana na wataalamu hao lakini wadai kuwa matumizi ya kiambishi awali {**ki-**} yanaweza kuelezewa kama mojawapo ya tashibihi, Kwa mfano, "Alifanyishwa kazi kipunda." Maoni hayo yote tunayaunga mkono.

Matumizi ya tashibihi huweza kubainishia msomaji zaidi juu ya hali, sura au rangi ya kitu, mtu au kitendo fulani kwa kujenga picha kamili mawazoni. Ulinganisho unaofanywa na kunga hii huleta mahusiano ya namna fulani ya ndani juu ya kinachozungumziwa.

### 2.2.3.3 SITIARI

Matumizi ya kunga hii huonyesha ubunifu wa mwandishi katika kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa <u>Kamusi ya Lugha na Isimu</u> iliyochapishwa na TUKI (1990:40), sitiari ni mtindo wa usemaji ambao hulinganisha vitu au watu bila kutumia viunganishi.

Sitiari ni dhana muhimu na ya kimsingi katika sanaa ya ushairi. Umuhimu wake unaifanya kuchunguzwa kwa upekee pasi na kuihusisha na dhana zingine zenye kuhusisha maana. Kunga hii huwa na sheria maalum ya uhamishaji wa maana na sifa ambayo huhusiana nayo. G. N. Leech (1969:159) ameiita kanuni hii "Sheria Kisitiari." Anasema kuwa katika sheria hii, A = kama B. Hapa ni kusema kuwa A hufikiwa kutokana na maana sisisi ya B kwa sababu ya kuwa na fahiwa kama B.

Madai hayo yanakubaliana na yale ya B. Syambo na A. Mazrui (1992:xv), Mwenda Mbatiah (2001:75), K.W. Wamitila (2003:202), F.E.M.K. Senkoro

(1982:14) na Kineene wa Mutiso (2005:59). Wataalamu hawa wanadai kuwa mbinu ya sitiari inafanya kazi sawa na tashibihi, ya kulinganisha vitu, hali au watu.Tofauti na tashbihi, sitiari haitumii viunganishi.

Sifa kuu ya tamathali hii ni kuleta tangamano katika vitu vinavyolinganishwa ambavyo vinakuwa kitu kimoja kwa ajili ya ile sifa inavyovileta pamoja. Sana sana sifa ya kitu cha kwanza huhama hadi cha pili kama tulivyoona hapo juu.

Matumizi ya sitiari hulengwa kwenye hadhira husika. Jinsi mshairi anavyotumia mbinu hii itawawezesha wasomaji wake kuamua ikiwa mshairi huyu amemudu matumizi yake au la. Kwa hivyo sitiari na matumizi yake huwa kama jaribio mwafaka la uwezo wa umbuji katika ushairi na sanaa kwa jumla. Ni kutokana na uwezo huu ndipo mtunzi ataweza kuunga dhana au vitu viwili vilivyo tofauti kabisa na kuwa na muungano mpya wa kitu kimoja.

Matumizi ya dhana hii huwa na lengo maalum. Dhamira hiyo ndiyo humfanya msanii kuchagua ni sitiari ipi aitumie wapi na kwa nia ipi.

Kwa mujibu wa K.W. Wamitila (KHJ), kuna sitiari aina nyingi, kwa mfano,

(i) Sitiari fiche – ambayo haijitokezi waziwazi

(ii) Sitiari fifi au chakavu: Sitiari ambayo imetumiwa katika lugha ya kawaida kiasi kwamba haionekani kama sitiari tena. Kwa mfano, "Kilimo ni uti wa mgongo"

(iii) Sitiari kuu: Hutumiwa kuelezea sitiari inayochukua nafasi kubwa katika kazi ya kifasihi. Sitiari hii huwa na nafasi muhimu katika kuyawasilisha maudhui ya kazi hiyo.

(iv) Sitiari shehenezi: Hii ni sitiari ambapo kilinganishi huwa kimefumbata au kina sifa ya ishara na kimefumbata kilinganishwa.

Katika kuchunguza sitiari katika kazi yoyote ya sanaa, umuhimu wake utadhihirika kutokana na uamili wake katika muktadha fulani. Hali hii inachochewa na ukweli kwamba, licha ya tofauti za kimakundi, sitiari yoyote ile huwa inalenga ujumi fulani. Ili kutalii ujumi na umuhimu wa sitiari katika kazi yoyote ile ya sanaa, kipengele cha muktadha ndicho huwa cha muhimu zaidi na wala sio kundi la sitiari. [Wellek na Warren, 1949:178 katika P.O. Ochoi (1998:23)].

### 2.2.3.4 TASHIHISI

Hii ni mbinu ambapo kitu, mnyama au mdudu hupewa sifa za binadamu. Kineene wa Mutiso (2005:61), Kithaka wa Mberia (1987:3), B. Syambo na A. mazrui (1992:xv), M. Mbatiah (2001:80), na K.W. Wamitila (2003:223), wanadai kuwa tashihisi ni tamathali ya semi ambapo vitu visivyokuwa na uhai pamoja na wadudu, ndege, wanyama na miti hupewa uwezo wa kuhisi, kuongea,kusikia, na kufikiria kama binadamu kinyume na hali yake halisi ulimwenguni. Tamathali hii ina uwezo wa kugusa hisia za msomaji au msikilizaji.

### 2.2.3.5 METONIMIA

Mwenda Mbatiah (2001:46), M. Msokile (1993:87) na G. N. Leech (1969:152) wanadai kuwa hii ni tamathali ambapo jina la kitu **A** linatumiwa kutajia kitu **B**. Ni tamathali inayotumia neno kuwakilisha neno, kitu au dhana nyingine yenye kuhusiana nalo. Vitu hivyo viwili vinakuwa na

uhusiano unaoeleweka.

Kwa mfano, Jembe - Mkulima

Mioyo - Watu.

Tamathali hii hutumiwa na mtunzi kufumbata maana ya kitu au dhana fulani.

### 2.2.3.6 CHUKU

Kwa mujibu wa Kineene wa Mutiso (2005:60), Kithaka wa Mberia (1987:7), S.M. Kuvuna na wengine (1992:24), K.W. Wamitila (2003:31), M. Mbatiah (2001:6), F.E.M.K. Senkoro (1982:18) na S.C.Gonga na wengine katika Mulika Na. 16: 61, chuku au udamisi ni mbinu ambapo jambo fulani hukuzwa au hutiwa chumvi kupita kiasi. Kunga hii hutumiwa kwa nia ya kuchekesha au kusisitiza ujumbe au hali. Vilevile kunga hii hutumika katika kutia moyo na hudhihirisha ujumi wa mtunzi katika kazi ya kisanaa. Sifa zinazotolewa huwa zimevuka kingo za uhalisia.

Kwa hivyo, sifa kuu ya mbinu hii ni kupotosha uhalisia kwa kusema mambo mengi ambayo hayapatikani au hayafanyiki katika ulimwengu halisi. Msanii hubuni ulimwengu wake dhahania kwa kutumia uwezo wake wa ubunifu kuwasilisha hali au jambo ambalo haliwezi kuthibitika au kukanushika. Chambilecho G.N. Leech (1969:166), mshairi ana jukumu la kutuongoza kwenye aina nyingine ya 'kweli' ambayo hukiuka kaida kwa kutumia chuku.

### 2.2.3.7 TAKRIRI

M. Mbatiah (2001:77), S.M. Kuvuna na wengine (1992:23), Kineene wa Mutiso (2005:56), Kithaka wa Mberia (1987:23), K.W. Wamitila

(2004:215), na F.E.M.K. Senkoro (1982:16) wanatoa maelezo yanayooana juu ya takriri kwa kusema kuwa ni mbinu ya utunzi inayohusu urudiaji wa sauti, neno au mstari fulani. Urudiaji huo hufanywa kwa nia ya kusisitiza au kushadidia. Katika ushairi, takriri inayojitokeza sana ni ile ya vina, ambapo sauti fulani inarudiwarudiwa katika mishororo. Vilevile panaweza kuwa na urudiaji wa maneno au msitari fulani. Takriri pia inaweza kutokea katika urudiaji wa maana fulani. K.W. Wamitila (KHJ) amezieleza aina za takriri kwa kina zaidi. Hii ni njia ya kishairi ya kuonyesha hisia nzito za kishairi.Mbinu hii hutumika katika kuipamba lugha ya kishairi. Marudiorudio ya maneno au sauti hupamba sanaa ya shairi.

### 2.2.3.8 TABAINI

M. Mbatiah (2001:76), K.W. Wamitila (2003:209), na Kineene wa Mutiso (2005:69), wanadai kuwa hii ni mbinu ya kusisitiza jambo kwa kutumia mtwezo, ambapo badala ya kutumia kauli chanya, kikanushi '**si**' kinatumiwa kutwezea kitu au hali fulani. Maneno yanayotumika huwa hayaonyeshi msisitizo huo waziwazi.

### 2.2.3.9 BALAGHA

Kithaka wa Mberia (1987:11), F.E.M.K. Senkoro (1982:17), K.W. Wamitila (2003:27), na Kineene wa Mutiso (2005:67) wanasema kuwa hii ni tamathali ambapo swali linaulizwa na mshairi huku tayari akiwa anajua jibu lake. Jawabu la jibu hilo huwa tayari linafahamika waziwazi. Maswali ya aina hiyo hayanuiwi kutafuta habari kama yalivyo maswali mengine katika lugha, bali hudhamiriwa kusisitiza ujumbe anaowasilisha mshairi.

Maoni yetu ni kuwa maswali ya balagha ni maswali ambayo majibu yake

yako wazi na hayahitajiki wakati huo. Huulizwa kwa nia ya kuathiri, kusisitiza, kushawishi, na kutia changamoto. Huwa na uzito wa kimatumizi kwani inatumiwa kama njia ya kuelezea au kutoa hisia za ndani kuhusu hali fulani. Maswali haya pia huleta mchomo wa aina fulani.

Ni muhali kutaja hapa kuwa si lazima alama ya kuulizia iwepo ndipo usemi uliohusika udhihirike kama swali la balagha. Wasanii wengi huwa hawatumii alama hii katika balagha. Muundo wa sentensi inayohusika ndio hubainishia msomaji kama inabeba swali la balagha au la.

### 2.2.3.10 USAMBAMBA /TANAKUZI

Kineene wa Mutiso (2005:70), S. C. Gonga na wengine katika Mulika nambari 16:176, M. Mbatiah (2001:101) wanadai kuwa ni tamathali ya usemi inayotumia ulinganishi wa sehemu mbili ambazo zina ukinzani wa kimaana. Mshairi hutumia maneno au hata semi mbili ambazo zinakinzana kimaana ili kusisitiza ujumbe. Kineene wa Mutiso (KHJ) ametoa mifano ya aina ya usambamba: wa kimaana, kidhamira, kiusawe, kisintaksia, na kadhalika.

Mchango wetu ni kuwa kunga hii inapotumika, humfanya msomaji au msikilizaji kujenga picha kamili ya kinachozungumziwa.

### 2.2.3.11 KEJELI

K.W. Wamitila (2003:79) anadai kuwa kejeli au kinaya hupatikana katika hali ambapo kuna kinyume fulani katika usemi, hali au tukio. Mtaalamu huyu amegawanya tamathali hii kwa makundi mawili:

(i) Kejeli hali – ambapo utokeaji wa jambo au mambo unakwenda kinyume na matarajio ya msomaji au mhusika anayepatikana katika kazi fulani.

(ii) Kejeli ya kibalagha: Hii ni aina ya kejeli ambapo toni ya sauti na maneno yanayosemwa ni kinyume na maana iliyokusudiwa.

Kineene wa Mutiso (2005:68) na M. Mbatiah (2001:27) wana madai sawa yanayotilia nguvu madai haya ya K.W. Wamitila. Wao wanasema kuwa maneno yanayotumiwa katika tamathali hii huwa ya kumtweza, kuchoma, kukata na kutia uchungu. Kunga hii pia inaweza kutumika kwa kumpa mtu sifa asizostahili.

Maoni yetu ni kuwa kejeli ni tamathali ambayo matendo au usemi wa mhusika huwa ni kinyume cha matarajio ya hadhira, na kulenga kufanya nini?

## 2.2.3.12 TAHARUKI

K.W. Wamitila (2004:212), M. Mbatiah (2001:77) na S.C.Gonga na wengine katika Mulika Na 16:71 wanatoa maoni yanayolingana kwa kudai kuwa istilahi hii hutumiwa kuelezea hamu kubwa anayokuwa nayo msomaji ya kutaka kujua jinsi mambo yatakavyojiri katika hadithi fulani. Hali hii hutokea kwa sababu mtunzi ameficha kimakusudi habari muhimu kumhusu nguli au mhusika fulani. Taharuki hutokea sana pale ambapo msomaji huwa na hamu kubwa au anajua yanayoweza kutokea lakini hajui jinsi yatakavyotokea.

## 2.2.3.13 MBINU REJESHI

K.W.Wamitila (2003:117), na S.C. Gonga na wengine katika Mulika Na.16:60 wanasema kuwa hii ni mbinu ambayo kwayo msanii anaelezea matukio yaliyotokea wakati wa nyuma.

Umuhimu wa kunga hii ni kumwezesha msomaji au msikilizaji kuelewa

zaidi yale yanayofanyika wakati ule yanafanyika kwa nini au chanzo chake ni nini. Kwa hivyo, mbinu hii hutufafanulia zaidi asili ya kitendo au hali fulani katika kazi ya sanaa.

### 2.2.3.14 NAHAU

Kwa mujibu wa K.W.Wamitila (2003:163) na Kineene wa Mutiso (2005:67), hii ni misemo ya picha ambayo huwa na maana iliyofichika. Nahau huwa na undani wa kimaana kuliko baadhi ya misemo inayopatikana katika lugha fulani. Kimuundo, nahau huwa kitenzi na jina. Maoni yetu ni kwamba nahau ni usemi ambao umefumbata maana yake ya ndani.

### 2.2.3.15 METHALI

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya Oxford (2004:240), methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia na kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.

Kulingana na K.W. Wamitila (2003b:108), Kimsingi, methali na nahau huleta sifa ya kufanya lugha ikaribiane na jinsi inavyotumiwa katika hali ya kawaida. Huu basi ni msingi muhimu wa kuonyesha uhalisi wa matumizi ya lugha. Methali hufanya ujumbe unaowasilishwa uwe na uzito wa kisanaa.Kama M.Msokile (1993:118) anavyodai, methali ni kifungu cha maneno yaliyosaniiwa kwa njia ya kufumba au kupiga mifano na ambacho kinachukua maana ndefu kuliko vile knavyoonekana.

Kwa maoni yetu, tunaunga maoni hayo mkono kwa kusema kuwa methali ni msemo wenye hekima na ambao hufumbata maana fulani.

### 2.2.3.16 ONOMATOPEYA

M.H. Abrams (1971:118), G.N. Leech (1969), K.W. Wamitila (2003:218) na M. Msokile (1993:95), wote wanadai kuwa onomatopeya au tanakali sauti hurejelea sauti katika kazi ya sanaa ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kinavyoenda, kiangukavyo, kilivyo au mapigo ya neno yanayoashiria kitu fulani.

Kuna tanakali sauti aina mbili: Kwanza, inayotuletea hisia za mlio wa kitu fulani.

Pili, inayotukumbusha maneno yanayohusiana na neno fulani maalumu.

Katika ushairi, mbinu hii hutumika sana. Wasanii huwa waangalifu sana wanapoteua maneno katika kazi zao. Wasanii hawa huteua na wakati mwingine huunda msamiati ambao una aina fulani ya sauti inayoashiria mnong'ono, fujo, unyonge, mwendo, kufyoza, mcheko, mlio, na hisia. Matumizi ya kunga hii hutoa picha na athari ya aina fulani.

### 2.2.3.17 LITIFATI

Kithaka wa Mberia (1987:13) na K.W. Wamitila (2003:100), wanadai kuwa hii mbinu ya kifasihi ambapo mtunzi hutoa nafasi kwa mhusika au kitu kinachohusika kuzungumza chenyewe. Hii ni aina ya unukuzi wa msemaji ambapo maneno halisi yaliyosemwa yanafikia hadhira katika hali ya nafsi ya kwanza.

## 2.2.4 MTINDO

Dhana ya mtindo imewahi kutolewa maelezo na wahakiki na wanasanaa mbalimbali. Lakini kufikia sasa bado upo mtafaruku wa sifa zake zinazopaswa kuwepo katika kila kijielezi. Katika kutilia mkazo madai hayo,

Jay Kitsao (1975:1) pia amesisitiza ugumu wa kufasili dhana ya mtindo. Jambo hili linafanya dhana hii iwe tata na changamani kutokana na fafanuzi mbalimbali zilizotolewa. Kwa sababu hii, tumetoa tu maelezo kutoka kwa baadhi ya wataalamu wanaolekea kukubaliana kuhusu mtindo ni nini. Baadhi yao wanadai kuwa lugha, wahusika, muundo, mandhari, toni, wakati na ploti vinapaswa kuzingatiwa katika ufafanuzi wa mtindo. Wanachokubaliana ni kuwa, mtindo ni kipengele mojawapo cha fani, huku wengine wakidai kuwa mtindo ni sawa na fani.

M. Mbatiah (2001:58), Wales (1989:435), na K.W. Wamitila (2003a:145; 2003c:191), wanadai kuwa mtindo ni jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi kwa kutumia lugha. Watalaamu hawa wanaendelea kukubaliana kuwa uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, beti, na mbinu zingine za lugha. G.N. Leech na Short (1981:9) wanasema kuwa kila mwandishi lazima afanye uteuzi wa kujieleza. Na ni kutokana na uteuzi huu wa njia ya kupanga kazi yake ndipo mtindo utapopatikana. Wanaendelea kudai kuwa mtindo ni njia ya kujieleza. Kila mwandishi lazima achague jinsi ya kujieleza. Kuna njia nyingi za kupitisha ujumbe mmoja. Kwa hivyo, itategemea vile mwandishi atakavyojieleza.

Maoni yetu ni kuwa mtindo katika fasihi ni namna mwandishi anavyowasilisha mawazo yake. Kila mwandishi hutumia mtindo fulani katika kazi yake. Uteuzi wa lugha humpambanua mwandishi na waandishi wengine. Namna mwandishi anavyojieleza ndivyo tunavyosema kuwa ni mtindo wake wa uandishi.

Mtindo ni muhimu sana katika kuwaongoza wahakiki kutathmini na kuainisha watunzi na kazi zao kwa misingi ya sifa hizo tulizotaja. Kwa mfano, katika ushairi, kupitia kigezo cha vina na mizani, tunaweza kupata aina ya ukawafi, mathnawi, gungu, tenzi na kadhalika. Kigezo cha mizani ni muhimu pia katika kutupa aina ya bahari tunazopata kwa kuangalia mikondo yao (D.O. Osiemo, 1997:42). Katika uchunguzi wetu tutazingatia kipengele cha mtindo kama namna watunzi wa tenzi za M N M na S Y N M wanavyojimundu katika kuteua na kutumia lugha na viungo vyake.

## 2.2.5 MUUNDO

Kwa mujibu wa Kineene wa Mutiso (2005:72), M. Mbatiah (2001:59), M.H.Abrams (1957:64) na K.W.Wamitila (2003:153) wanadai kuwa muundo ni jumla ya uhusiano uliopo kati ya visehemu mbalimbali vinavyounda kazi ya kifasihi na jinsi vijisehemu hivi vinavyohusiana na kuunda kazi nzima. Hutumiwa kuelezea mpangilio wa kazi ya kifasihi. Mpangilio huu hujionyesha kwenye maumbo ya kazi ya kifasihi. Uhusiano huo ndio unaoipa kazi umbo, ruwaza na sura.

## 2.2.6 PLOTI

Kwa mujibu wa K.W. Wamitila (2002:6 na 2003b:142) na Kineene wa Mutiso (2005:74), ploti au msuko ni mfuatano au mpangiliano wa matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi kwa kutegemea uhusiano wake wa kiusababishi. Ploti ni kiepengele muhimu cha kimuundo katika hadithi yoyote ile.

Mhakiki huyu (KHJ) anafananisha ploti na injini ya gari kwa kudai kuwa

> *"Haimkiniki gari kufanya*
> *Kazi vizuri kama injini yake*
> *ina matatizo.... Msuko*
> *huleta taharuki, msisimko*
> *wa mshangao. Hizi ni sifa*
> *ambazo zina mchango*
> *mkubwa katika kumburudisha*
> *msomaji wa kazi fulani."*

Tunaunga mkono madai hayo kwa sababu hakuna kazi ambayo inaweza kuitwa ya kisanaa kama haina ploti. Ubora na utamu wa kazi yoyote ya kisanaa hutegemea jinsi mtunzi alivyoweza kufuma vitushi kwa njia ya kiusababishi. Naye M.H. Abrams (1957:127) amedai kuwa ploti hutumiwa katika kazi ya kifasihi kwa lengo la kuleta athari za kihisia au za kisanaa.

Katika ushairi, ploti tiririshi hutumika. Ploti ya aina hii ni ile inayosimulia au kuelezea matukio kutoka mwanzo hadi mwisho. Ploti inaweza kuwa changamani, kwa mfano, ploti ya Utenzi wa Hamziyya, ambapo mtunzi anaenda mbele kisha kurudi nyuma na kwenda mbele tena katika usimulizi wake.

Ploti vilevile inaweza kuwa sahili, hivi kwamba inaweza kuelezeka kwa muhtasari wa maneno machache. Hata hivyo, K.W. Wamitila (2002:7) anadai kuwa

> *"Kusema kazi ina msuko sahili*
> *au rahisi sio kusema kuwa ni*
> *dhaifu. Ili kufikia uamuzi wa*

*aina hii, kuna vigezo vingi vingine vya kuangaliwa".*

Kulingana na madai hayo, ni lazima vigezo vyote viangaliwe na mhakiki katika kuiweka kazi fulani ya kifasihi mizanini na hukumu kwamba kazi hiyo ni changamani au sahili.

## 2.2.7 MANDHARI NA WAKATI

Ni vigumu kutenganisha vipengele hivi. Hii ni kwa sababu dhana hizi zinahusiana kwa kuchangiana. Mandhari ya kazi fulani hutegemea wakati ambapo kazi hiyo inatungiwa. Vivyo hivyo, wakati wake hutegemea mandhari ya kazi hiyo.

Maoni hayo yetu yanaelekea kuungwa mkono na K.W. Wamitila (2003:108) amabaye amedai kuwa, dhana ya mandhari hurejelea wakati na mahali pa kazi ya kifasihi, yaani mazingira ya utendaji au usimulizi wake. Dhana hii pia huelezea mazingira ya kijamii wanakojikuta wahusika wa kifasihi.

Wakati ni muda unaohusishwa kisanii na matukio yanayoelezwa. Kazi yoyote ya kisanaa hukosa umuhimu na uzito pale ambapo inaangaliwa nje ya wakati. Wakati unaweza kuwa maalum au wowote ule. Baadhi ya matukio hutengewa tu wakati mmoja na huwa vigumu tena kuelezeka nje ya wakati ule. Wakati ni muhimu katika kuwawezesha wasomaji kujua kama matukio yanayosimuliwa au kuelezewa yamekwishatokea, yanatokea au yatatokea. Jambo hili huwezesha wasomaji wawe na uwezo wa kufuatilia matukio kutokeapo mabadiliko katika mitindo mbalimbali ya

fani. Kwa kufanya hivyo wataweza kujua matukio hayo yalitokea lini, kwa nini na umuhimu wake.

Umuhimu wa mazingira ni kumwezesha msomaji kuelewa picha anayoilenga msanii. Mazingira yanaweza kuwa ya kivita, kisiasa, kidini, kimapinduzi, kiuchumi, kihistoria, kijamii, kimapenzi, na kadhalika. Mandhari huhusisha mahali mbalimbali hususan, ahera, duniani, peponi, misikini, porini, pangoni, msituni, milimani, na mahali pengine pengi.

Mazingira mengine ni ya kidhahania kama vile peponi, mbinguni na ahera. Mandhari hutokea dhahiri au hufichika kwa kutegemea kiwango cha ubunifu wa wasanii. Kwa mfano, ikiwa ni kuabudu, mahali kama msikitini, kanisani, mlimani, mtini, jabalini, pangoni hufaa. Vilevile hali ya mkusanyiko wa watu wengi katika eneo moja kwa nia ya kusali au kutoa kafara itatuchorea mandhari ya kuomba Mungu au miungu.

Tungo zinapoteza thamani kwa sababu ya kutokea katika nyakati na mandhari yale ambapo hazitakiwi. Tungo nzuri ni zile ambazo siyo za wakati mmoja maalum, ambazo zinafaa katika nyakati zote na mandhari yake yanaafikiana na utunzi pamoja na wakati wake.

### 2.2.8 TONI

Kwa mujibu wa K.W. Wamitila (2003:235), hii ni dhana inayotumiwa kuelezea mkabala alionao msimulizi wa hadithi kwenye wahusika waliomo katika hadithi yake na yaliyomo pia, matukio na hali iliyopo. Mara nyingi toni huhusishwa na masafa ujumi katika fasihi.

Toni hujitokeza katika shairi lolote. Aina nyingi za toni hujitokeza ama za huzuni, huruma, masikitiko, kuamrisha, furaha, kuchanganyikiwa, ukatili, kilio au hali zingine nyingi.

Msanii hutumia toni kwa lengo la kuathiri hadhira yake kwa kuziba masafa ya ujumi. Toni hutusaidia kupima au kujua hisia zinazosababishwa na kazi ya kifasihi inayohisika. Nguvu ya toni itatambulikana kulingana na muktadha na mazingira inapojitokeza. D.O. Osiemo (1997:48) anadai kuwa toni lazima ikubaliane na wakati, mandhari na mwendelezo wa ploti. Lengo letu ni kutathmini matokeo ya toni katika tenzi za M N M na S Y N M.

### 2.2.9 WAHUSIKA

D.O. Osiemo (1997:38), Kineene wa Mutiso (2005:79), K.W. Wamitila (2003:123), na M. Mbatiah (2001:109), wanadai kuwa wahusika ni watu, vitu, wanyama, ndege, wadudu, miti, mashetani, majini wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe. Kutokana na matendo na mazungumzo yao, wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika.

Kila mhusika huwa na umuhimu mkubwa sana katika kazi ya sanaa. Huingizwa katika kazi kwa makusudi ili kutimiza malengo maalum ya msanii kwani bila hivyo, huenda baadhi yao wakaonekana kama waliozuka kiajali tu. Jambo kama hili lapaswa kuepukwa katika sanaa hata kama nia yake itakuwa tu kusukuma kazi mbele.

Baadhi ya wahusika hushirikishwa kwa kupatiwa nafasi ya kutenda, kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira. Kusawiriwa kwao hudhihirika kwa kutegemea msanii anavyopendelea. Msanii humuumba

mhusika kwa nia ya kumfanya kielelezo cha wema kwa hadhira au kama njia mojawapo ya kuthibitisha hoja kuhusu uovu wa jamii. Mara nyingine, msanii anaweza kuonyesha kuwa licha ya uozo wa mhusika fulani, bado ana mifano mizuri ya kuigwa.

Wahusika wengine ni wale vivuli, ambao huchukua nafasi za wahusika halisi. Jambo hili hufanyika pale watunzi kwa malengo mbalimbali huamua kuwafumba wasomaji kwa kuchukua wahusika kama ndege, wanyama, wadudu na vitu visivyo na uhai badala ya watu. Wahusika hawa huwa na tabia na mienendo kama ya wanadamu. Huwakilisha watu halisi katika ulimwengu halisi.

Ubora wa kazi ya kisanaa hutegemea jinsi wahusika walivyoumbwa. Katika kipengele hiki, tutachunguza jinsi wahusika walivyochorwa, namna walivyodhirika na namna walivyotekeleza majukumu yao.

## HITIMISHO

Katika sehemu hii tumeshughulikia dhana ya fani na vipengele vyake. Vipengele hivyo ndivyo tutakavyoshughulikia katika sura ya tatu na ya nne kama vinavyojitokeza katika tenzi za M N M na S Y N M. Vipengele hivyo ni kama matumizi ya lugha kwa jumla pamoja na uhuru wa kishairi. Tumechunguza maana ya baadhi ya vipengele vya tamathali za semi kama vile tashibihi, istiari, balagha, na vinginevyo. Katika kila kipengele, tumeelezea maana na umuhimu kinavyotekeleza katika sanaa huku tukijikita sana katika utanzu wa ushairi.

Katika sura ya tatu, tutachunguza kwa kulinganisha na kufananisha kila

mojawapo ya viungo hivyo vya fani katika tenzi za M N M na S Y N M huku tukionyesha ama ufanifu au udhaifu pamoja na uamilifu wake katika muktadha wa matumizi.

# SURA YA TATU

## UCHANGANUZI NA ULINGANISHAJI WA FANI YA TENZI ZA MIKIDADI NA MAYASA NA SWIFA YA NGUVUMALI

### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutachanganua na kulinganisha fani ya tenzi za M N M na S Y N M. Kabla ya kufanya hivyo, tutaelezea tenzi zinazohusika kwa ufupi.

Utenzi wa M N M, ambao una beti 778, ni juu ya kisa kinachohusu mashujaa wawili, Mayasa na Mikidadi. Kinasimulia namna vijana hawa walivyoshinda pingamizi walizowekewa ili wasioane. Mikidadi anadaiwa posa ya mali nyingi sana na baba yake Mayasa. Hii ikiwa njama ya kumkosesha nafasi ya kumuoa Mayasa. Mikidadi anajitahidi kupata mali hiyo licha ya vikwazo vingi. Wakati anapoleta mali ili amuoe Mayasa, anapata tayari ameozwa tajiri mmoja, Malik bin Riyahi. Mikidadi anakasirishwa na jambo hili na kutangaza vita dhidi ya Malik na kumtwaa Mayasa. Anwani ya utenzi huu inarejelea wahusika hao wawili ambao ndio wakuu katika kisa hiki. Utenzi huu ni wa kishujaa. Unazungumzia juu ya maisha ya wahusika ambao wamewahi kuishi humu duniani katika nyakati za Mtume Muhammadi S.A.W. Ni mashujaa wa Kiislamu.

Kwa upande mwingine, utenzi wa S Y N M unasimulia juu ya kupotea kwa mwanamke mmoja, Salima Binti Hanifu na kifo chake. Kisa hiki ni cha kweli kilichofanyika katika kijiji kimoja kilichojulikana kama Mteniyapa,

sehemu iliyoitwa Panenenene, eneo la pwani ya Afrika Mashariki.

Uchunguzi unafanywa na mganga aliyesifika na kutambulika sana kama Nguvumali. Kwa kutumia ujuzi wake, Nguvumali anathibitisha kuwa Salima Binti Hanifu aliuawa kwa kurogwa. Anawatambua wachawi waliofanya kitendo hicho na kuwakabidhi serikali.

Sasa tutachunguza fani ya tenzi hizi na kuilinganisha.

## 3.1 MTINDO

### 3.1.1 LUGHA

Mtunzi wa ushairi ana uhuru wa kuchota msamiati kutoka asili nyingi na kuutumia katika utunzi wake. Katika tenzi za M N M na S Y N M, watunzi wametumia lugha ya kilahaja, Kiswahili sanifu, Kiarabu na hata Kiingereza. Uhuru wa mshairi umewapa nafasi ya kufupisha, kurefusha na kubadilisha sauti ya maneno kwa malengo mahususi.

Kijipengele hiki kitachunguza jinsi lugha ilivyotumiwa katika tenzi hizi pamoja na ufanifu wake katika kufanikisha ujumbe na dhamira ya watunzi wake. Katika kufanya hivyo, tutaangalia uteuzi wa msamiati, uhuru wa mshairi, na tamathali za usemi.

### 3.1.2 LAHAJA

Mtunzi wa utenzi wa S Y N M ametumia maneno ya lahaja inayozungumzwa sehemu ya Kilwa (Abdulaziz 1968:83). Hata hivyo, tunaona kuwa sifa za lahaja hiyo hazijitokezi vizuri. Zaidi ya hayo, msamiati uliotumiwa una sifa zingine ambazo tunaweza kudai kuwa

zinatokana na athari ya uhuru wa mshairi kwa sababu baadhi ya msamiati huo hauwezi kuwekwa katika kiwango cha Kiswahili sanifu.

Katika matumizi ya lahaja, tunashuhudia kuwa mtunzi anatumia sauti [**h**] kuitambulisha lahaja hiyo. Wakati mtunzi anapotumia [**h**], anatumia mabano, kwa mifano, (h) **umo** (ubeti 53**), (h) uko** (64), **(h)ao** (76), **(H) apa** (101), **(H) apawi** (113), **(H) ujiona** (121), **(h) atumwoni** (148), **(H) akuna** (180), **(h) aswili** (194), **(h) azina** (200). Mifano mingine inapatikana katika beti za **206, 207, 211, 213, 227, 234, 235, 241, 245, 252, 254, 256, 260, 265, 285, 291, 297, 321, 336, 353, 361, 383 na 387.**

Wakati mwingine, ni kama kwamba mtunzi analazimisha matumizi ya [**h**]. Kwa mfano, **mitahani** (365) na **mahovu** (43) badala ya **mitaani** na **maovu.**

Mara nyingine, pale panapohitajika [h] katika Kiswahili sanifu, sauti hiyo inaachwa. Kwa mfano, **Asubui** (56), **kuangaika** (84), **kioro** (131), **tukasangaa** (138**), tumesituka**

(148), na **uyo** (222) badala ya **asubuhi, kuhangaika, kihoro, tukashangaa, tumeshtuka** na **huyo**.

Matumizi ya lahaja yanajitokeza pia katika matumizi ya sauti ya konsonanti [ **r** ] na [ **l** ]. Kwa mfano, pale ambapo panastahili kutumiwa [ **r** ], sauti [ **l** ] inatumika badala yake. Vilevile pale panapohitajika kutumiwa [ **l** ] katika Kiswahili sanifu, [ **r** ] inatumiwa badala yake. Kwa mfano, maneno kama **kalamu, tulia, shauli, badili, kukatalia, kusimulia, ripoti,**

**kufeli,** na **Nguvumali** Kilahaja,maneno haya yanajitokeza kama **karamu (9), shauri (33), turia (28), kikataria (50), kusimuria (81), lipoti (127), kuferi (178) na Nguvumari (222).**

Kuna kutofuatilia au kushikilia matumizi hayo. Kwa mfano, neno **serikali** (303, 350) linajitokeza kama **silikali** (360) na Nguvumali linajitokeza kama **Nguvumari** (308), **shauri** (33) na **shauli** (26). Msanii anaonyesha kutokuwa na msimamo katika matumizi ya sauti [ r ] na [ l ], kwa sababu hata pale ambapo sauti ya mwisho katika mishororo ya ubeti ni [ li ] anabadilisha sauti na kutumia [ r ] badala ya [ l ] Kwa mifano, (308)

Wakashukuru tayali
Nataka kushamburia.
'Akasema Nguvuma<u>ri</u>
'Sasa nakaa uzuri

Yumkini mtunzi huyu anachukulia kuwa matumizi ya sauti **[r]** na **[l]** kuwa mamoja kama inavyodhihirika katika mifano tuliyotoa hapo juu.

Aidha msanii amepuuza kiyeyushi [**y**] katikati ya konsonanti **v, o** na baada ya **n**. Matumizi haya yanaonyesha athari za kilahaja. Kwa mfano, maneno yanayoendelezwa kama **mwenyewe, ndivyo, ulivyoniambia, ninavyokupima, alivyodhani** na **tunavyofikiri**, yanajitokeza kama: **Mwenewe** (21)**, ndivo** (76), **ulivonambia** (65), **ninavokupima** (154), **alivodhani** (231) na **tunavofikiri** (238).

Mbali na matumizi ya lahaja ya Kilwa, uteuzi huu wa msamiati una athari za lahaja zingine kama Kiamu ambapo sauti [**y**] inatumiwa pahali pa sauti [**j**]. Maneno kama, **wanajua** na **pamoja,** yanajitokeza kama **wanayua**

(39, 68) na **pamoya** (154, 214, 246).

Kuna matumizi ya herufi [**t**] badala ya sauti [**č**]. Kwa mfano, neno kama **machungu** linajitokeza kama **matungu** (50, 81, 103).

Katika M N M vilevile, kuna matumizi ya lahaja ya Kiamu, kwa mfano, **mbwene** (12, 68), **awene** (186). Sauti [**y**] inatumiwa badala ya [**j**], kwa mfano, **mmoya** (7), **pamoya** (69) na **wayua** (476). Sifa za lahaja ya Kimvita pia zinajitokeza,kwa mfano, konsonanti [**t**] inajitokeza mahali pa sauti [**č**] kama tunavyoona katika maneno kama, **mato** (18;98), **walotukua** (50;128), **waliotukua** (73), **tini** (173), **hatuyati** (248), **ukaata** (342), **usinifite** (474), **siniwate** (477) na kadhalika.

Mtunzi pia amepuuza sauti [**h**]. Kwa mfano, **havitakwisa** (133), **akisa** (164), **ikiisa** (166) na **kisa** (740). Matumizi haya pia yana sifa ya lahaja ya Kiamu.

### 3.1.3 MSAMIATI WA KIARABU

Msamiati wa dini ya Kiislamu umejitokeza katika utenzi wa S Y N M, ambao unabainisha kuwa mtunzi alikuwa na athari za Kiislamu. Matumizi ya msamiati wa aina hii yanaleta dhana ya motifu ya kidini katika utenzi huu. Kwa mfano, majina ya Mwenyezi Mungu yanayojitokeza ni kama **Mola** (1), **Rabbana** (2, 180, 205), **Rabbi** (3, 176), **Ilahi** (77), Rabbuka (93), **Jalia** (180). Majina haya yote yanaashiria sifa za Mwenyezi Mungu. Matumizi ya msamiati huu yanaonyesha dua ya Waislamu kwa wenye kuutumia. Kwa mfano, ubeti wa 205:

Waliondoka vijana
Wakamwomba Rabbana

'Ya Rabbi ya Molana
Utunusuri baria'

Jambo hili linaonyesha vile wahusika walivyokuwa wameathirika kwa hofu kutokana na kupoetea kwa Salima Binti Hanifu.

Msamiati wa Kiarabu unaopatikana katika utenzi huu asili yake ni **Kurani Tukufu**, na kwa hivyo, unaleta athari za kidini kama anavyodai Kazungu Kadenge (1982: 138). Ni msamiati mchache tu wa Kiarabu ambao hauleti dhana ya kidini. Kwa mfano, **kuruhi** (102), **kuradidi** (109), **kudhwili** (117), **baidi** (164), **haswili** (194), **iqabu** (241), na kadhalika. Matumizi ya msamiati wa kigeni katika ushairi ni athari iliyokuwepo tangu jadi (Abdulaziz 1979:88).
Mtunzi ana uhuru wa kuchota msamiati wake kutoka asili yoyote ile. Hufanya hivyo kwa njia ya kisanaa ili kuwasilisha wazo alilonalo kwa njia ya wazi zaidi.

Utenzi huu wa S Y N M, unaanza kwa neno la Kiarabu **Bismillahi**, linalomaanisha kwa jina la Mwenyezi Mungu. Hii ni dua inayosemwa na Muislamu ye yote popote alipo kabla ya kuanza jambo lolote. Kwa mfano, kabla ya kula asubuhi, kabla ya kuchinja mnyama, kupanda chombo cha kusafiria, kuanza kujenga nyumba, na kadhalika.

Mtunzi ameanza kwa dua ambayo ni sifa mojawapo ya kutanguliza utenzi. Chambilecho M. Msokile (1993:55) Tenzi nyingi katika usimulizi wake huanza na dua, na kumalizia na dua. Kwa mujibu wa E.K. Kadenge (1982:142) kila sura ya Korani huanzia kwa "**Bismillahi Rahaman**

**Rahim**" kama mwanzo wa kuandika au kakariri maneno matakatifu. Sifa hii vilevile inapatikana katika utenzi wa M N M ambao unaanza kwa **Bismillahi.** Hii ni sifa inayopatikana katika tenzi nyingi kama vile utendi wa **al-Akida, Inkishaffi,** utenzi wa **Maisha ya Nabii,** na utenzi wa **Adamu.**

Katika S Y N M, msamiati wa Kiarabu ulioandikwa kwa fonolojia ya Kiswahili ni kama, yaqini (18, 29, 183, 187) **arbini** (167), **Waliyaqini** (198), **Iqabu** (241), **Khabari** (4, 44) **akaqimu** (42). Katika Kiswahili, hakuna matumizi ya konsonanti **–q-.** Matumizi ya msamiati huo yanathibitisha athari ya lugha ya Kiarabu kwa mtunzi.

Msamiati mwingine wa Kiarabu katika utenzi wa S Y N M, ni kama vile, **Nawaita 'l-Khadathi** (6). Kwa mujibu wa Peter Lienhardt (1968:88), huu ni msemo wa Kiarabu ambao hutumiwa wakati wa kuanza kutawadha au kusali. Hata hivyo, nilipoongea na Dkt.A.I. Al-Asar (28/06/2005) alipinga madai haya na kudai kuwa neno **nawaitu** lina maana ya kufanya jambo fulani kwa nia halisi kwa upande wa moyo, akili na matendo. Tunaunga maoni haya mkono kwa sababu kuwa mtunzi alitumia msamiati huu katika utangulizi wa utenzi wake ili kuonyesha vile alivyojitolea kwa vyovyote ili kuwasilisha mawazo yake muhimu. Kazungu Kadenge (1982:150) anadai kuwa mtunzi ametumia msemo huu kimakusudi ili kuonyesha umuhimu wa kisa chake katika jamii husika.

**Agheru shetan** (130) ni msemo ambao Kazungu Kadenge anadai **Agheru** ni neno la Kiarabu linalotokana na kitenzi **ghair** (kukataa, kukana), lakini maana yake kamili ni kubadili nia. Katika ubeti huu, Binti

Ramadhani anamshtumu shetani kwa kufanya uamuzi ambao sasa anasikitikia.

**Fi – 'l-leyli** (225) lina maana ya usiku. Neno usiku linatangulia kuonyesha msisitizo wa jambo ambalo mhusika Shambi alikuwa anafikiria – kuweka maiti ya mhusika Salima katika banda ili iaminike kuwa alipatwa na ajali alipokuwa akivunja kuni (227).

Msamiati mwingine wenye asili ya Kiarabu unaopatika katika utenzi wa M N M ni kama: **Fakhari** (19), **swaghiri** (62), **takhubiri** (180, 129), **khamsu** (187), **akdadhukuri** (38), **khanjari** (71), **usikhofu** (93), **khamsini** (216, 150), **khayusi** (196), **khabarizo** (227), **akhiri** (266), **murtadi** (282), **marhaba** (289), **khadaa** (293), **tumkhitarize** (565), **na 'lfajiri** (597).

Mtunzi ameuswahilisha msamiati huo kwa kuupa fonolojia ya Kiswahili. Amefanya hivyo ili kudumisha mdundo wa utenzi ili uimbike kwa mahadhi. Vilevile tunapata kwamba baadhi ya msamiati uliokopwa kutoka Kiarabu na ambao umetumika katika utenzi huu, unatumika katika Kiswahili cha siku hizi baada ya kusanifishwa.

### 3.1.4 MSAMIATI WA KIINGEREZA

Mtunzi wa S Y N M, ametumia msamiati wa Kiingereza. Msamiati huu umepewa umbo la Kiswahili. Hata hivyo, sio wote uliopewa umbo la Kiswahili, kwa mfano, **headman** (144). Tutachunguza na kutoa mifano ya matumizi ya maneno hayo yaliyokopwa kutoka Kiingereza.

Matumizi ya neno **dabali** (double) kama linavyojitokeza katika ubeti wa 288 lina uamilifu na athari katika matumizi yake. Neno hili linavyotumiwa katika muktadha ni tofauti kidogo na matumizi yake ya kawaida. Mtunzi ametumia neno hili wakati Binti Ramadhani anapopigwa na kuhojiwa na polisi kuhusu kifo cha Salima Binti Hanifu. Anakanganyika na kuropokwa majina ya watu wengi – hata wengine hawakuhusika katika uhalifu huo. Kwa kusema, kawataja kwa dabali, mtunzi anamaanisha wanachama wa kikoa cha wachawi na watu wengine waliotajwa, walitajwa kwa haraka na kwa mfululizo kutokana na kuchanganyikiwa na kuogopa mchapo wa polisi. Msamiati huu una uzito kwa sababu unaleta mvuto na mnato kwa kutuchorea picha mawazoni juu ya tukio hilo.

Mifano mingine ya msamiati wa Kiingereza ni kama **keshi** (20) – cash, **chemba** (41) – Kiing. chamber, **lipoti** (260) – report, **baiskeli** (207) – bicycle, **polisi** (251) – police, **kukorosi** (260) – cross-out, **motukari** (312, 382) – motor car, **jajiment** (277) – judgement, **saini** ( 204) –sign.

Msamiati huu umetoholewa kimakusudi ili kuleta athari iliyokusudiwa. Kama Abdulaziz (1968:83) alivyodai, mtunzi wa utenzi wa S Y N M, amejikakamua kuwasilisha matukio ya kisanaa ambayo ni ya kisasa kwa njia mwafaka na ambayo inadhamiriwa kuteka usikivu wa hadhira ya kisasa. Vilevile mtaalamu huyu anasema kuwa jaribio la mtunzi huyu la kutojifunga na kaida za utunzi zilizozoeleka ni hatua njema ya kuuweka ushairi huru kutokana na muundo wa kiasili ulioshikilia kaida hizo.

Wasanii wa tenzi hizo wameteua msamiati wao kwa makini na hadhari kubwa. Utenzi huo unaoana na mandhari na wakati. Kwa mfano, uteuzi

wa msamiati wa kidini unaleta toni ya kidini katika mandhari ya Kiislamu. Watunzi wamepamba tenzi hizi kwa kutumia msamiati wa aina nyingi. Wameteua msamiati wao kutoka asili nyingi ili kuwasilisha ujumbe kwa uazi zaidi. Wamefanya hivyo kwa kutumia uhuru wa mshairi, jambo ambalo linakubalika.

## 3.2 UHURU WA MSHAIRI

Huu ni uhuru ambao mshairi huwa nao katika utunzi. Uhuru huu huwa katika viwango vya kileksika, fonolojia, mofolojia, semantiki, sintaksia na hata kiothografia. Kama tulivyotaja hapo awali, mtunzi anaweza kuutumia kwa kuteua msamiati, mpangilio wa msamiati huo katika mshororo, kufupisha maneno, kurefusha, kubadilisha mpangilio wa sauti katika neno na matumizi ya lugha kwa jumla. Uhuru huu ni ukiushi wa kaida za lugha zilizozoeleka katika lugha ya kawaida. Ukiushi huo hufanywa kwa lengo maalum.

Watunzi wa M N M na S Y N M, wametumia uhuru wa mshairi katika kufanikisha tungo zao katika viwango mbalimbali kama tulivyotaja hapo juu. Aidha wamefupisha msamiati kama tutakavyoshuhudia hapa chini.

### 3.2.1 INKISARI

Hii ni dhana ya kufupisha maneno kwa nia ya kupata ufananisho au urari wa mizani katika mshororo. Hata hivyo, sio kila wakati mbinu hii hutumiwa kwa lengo la kupata urari wa mizani. Katika utenzi wa S Y N M, maneno yanayojitokeza ni kama: **wa** (37) – wana**, walifatia** (191) – walifuatia**, miko** (209) – miiko**, kachukua** (212) – akachukua au alichukua**, kenda** (250) – akaenda, **ufajiri** (272) – alfajiri, **hapapa** (272) –hapakuwa, **alivo**

(333) – alivyokuwa, **wachama** (336) – wanachama.

Mifano katika utenzi wa M N M ni kama ifuatayo. **Ona** (1) – kuona, **pekeyo** (5) – peke yako, **chajiyo** (5) – cha jioni, **pekeye** (7) – peke yake, **ali** (19) – alikuwa, **upendeye** (29) – umpendaye **nasende** (35) - na asiende, **fumole** (57) fumo lake, **akiweta** (58) – akiwaita, **kungia** (79) – kuingia, **unazime** (81) – uniazime, **nazima** (83) – niazime, **kawangia** ( 85) – kawaingia, **suraze** (98) – sura zao, **suraye** (99) – sura yake, **juhudiye** (101) – juhudi yake, **akawalani** (124) – akawalaani, **kuwauza** (140) – akawauliza, **usikasiri** (146) – usikasirike, **tondoke** (184) – tuondoke, **minawe** (346) – mimi na wewe.

Kutokana na mifano hiyo, tunagundua kuwa watunzi wa tenzi hizi wamefupisha maneno kwa kupunguza sauti zake au kuunganisha maneno zaidi ya moja na kuyafupisha. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kupata urari wa mizani katika mishororo ya beti. Wakati mwingine wanafupisha kwa ufundi zaidi ili kupata mizani na vina vinavyohitajika. Mifano kama hii inapatikana katika utenzi wa M N M kama, peke yako na cha jioni yanafupishwa na kuwa **pekeyo** na **chajiyo** (50) ili kina –**yo** kipatikane. Niazime na usikasirike yanafupishwa na kuwa nazima (83) na usikasiri (148), ambapo silabi za mwisho wa maneno (-**ri** na **-ma**) zinapatikana.

### 3.2.2 MAZIDA

Madhumuni ya matumizi ya kunga hii ni kutosheleza idadi ya mizani inayohitajika katika mshororo ili utenzi uweze kuimbika au kukaririka kwa mahadhi au mdundo unaovutia. Kunga hii pia kama ilivyo inkisari, haitumiwi kwa lengo la kupata idadi ya mizani kila wakati.

Katika tenzi zote mbili, watunzi wametumia kunga hii ya kurefusha maneno. Katika utenzi wa S Y N M, kuna mifano kama vile, **mwenginewe** (38) – mwingine, **kuchelewea** (278) – kuchelewa, **mwinginewe** (300) – mwingine, **tulivokusema** (327) – tulivyosema.

Katika utenzi wa M N M kuna mifano kama, **mdawara** (81) – duara, **kumwonakwe** (27) – kumwona, **mashujaani** (34) – mashujaa, **aula** (87) – au, **huyule** (100) – huyu, **farasila** (151) – farasi, **kuyafikilia** (175) – kayafikia, **kuonake** (182) – kuona, **anisimangiza** (520) – anisimanga.

Utenzi wa M N M umetumia kunga hii pia kwa madhumuni ya kupata silabi inayohitajika mwishoni mwa mshororo. Matumizi haya yamefanikisha kazi hii kwa ufundi zaidi. Maneno mengine katika lahaja za Kiswahili hujitokeza kwa umbo ambalo likiangaliwa kwa jicho la Kiswahili sanifu huonekana kama kwamba mbinu ya mazida au inkisari imetumiwa lakini sio hivyo. Kwa hivyo, mifano mingine tuliyotoa hapo juu huenda ikawa ni baadhi ya matumizi ya lahaja.

### 3.2.3 TABDILA

Hii ni mbinu ya kubadilisha mpangilio wa sauti au vitamkwa katika neno. Mbinu hii imetumiwa katika utenzi wa M N M kwa lengo maalum. Aghalabu matumizi haya huwa ya kilahaja pia. Kwa mfano, **kumkurubia** (91) – kumkaribia, **hutoweza** (82) – hataweza, **nitakao** (126) – nitakaye, **Kesu** (238) na **Kesa** (201) badala ya Kesi, **shujai** (366) - shujaa, **Mayasi** (564) –Mayasa na **alipomkurubia** (732) badala ya alipomkaribia. Sauti

za maneno hayo zinabadilishwa katika utenzi huu kwa nia ya kupata vina vinavyohitajika lakini sio kila wakati. Fauka ya kutumia mbinu ya tabdili, baadhi ya matumizi yanaonyesha athari za kilahaja. Athari hii inajidhihirisha pale ambapo neno linalobadilishwa sauti huwa halina athari yoyote katika vina. Kwa mfano, **kumkurubia** (91), **hutoweza** (82) na **alipomkurubia** (732).

Katika S Y N M, tunapata maneno kama: **Moyonzi** (120) badala ya moyoni, **kiviri** (210) – kivuli, **imemziwia** (301) – imemzuia. Tunaweza kusema kuwa katika mfano wa ubeti wa 210, mtunzi ametumia mbinu ya tabdila ili kutosheleza silabi ya mwisho wa mshororo unaohusika lakini haieleweki ni kwa nini sauti za neno 'kivuli' zikabadilishwa katika ubeti wa 210, ambapo neno kiviri linapatikana. Jambo hili linakanganya hata sauti ya mwisho ya mshororo huo ambapo kina kinastahili kuwa -**li** na ambacho kingepatikana bila kubadilisha vitamkwa vya neno kivuli. Vilevile katika neno **imemziwia** (301) hakuna athari yoyote inayosababishwa kwa kubadilishwa kwa sauti za neno imemzuia.

Maoni yetu ni kwamba matokeo haya yamesababishwa na kuathiriwa na lahaja kwa mtunzi kiasi cha kutotambua au kujali matokeo ya athari hiyo katika utenzi.

### 3.3 MUUNDO

Wasanii wa tenzi za M N M na S Y N M, wameteua maneno na kuyapanga kishairi katika kuunda kazi zao. Muundo huo umezipa kazi hizi sura za mashairi na sifa ya tenzi inayotokana na urefu wa mashairi haya.

Utenzi wa M N M una beti 778. Kila ubeti una mishororo minne yenye kipande kimoja. Hii ni sifa mojawapo inayotambulisha tenzi. Utenzi wa S Y N M, una beti 393. Kila ubeti una mishororo minne. Mizani katika mishororo hiyo huhitilafiana kiidadi kama tutakavyoona baadaye.

### 3.3.1 VINA

Kina ni sauti au silabi zinazolingana na zinazopatikana katika mwisho wa mstari wa ubeti. Wataalamu wengine hudai kuwa kina ni silabi ya mwisho katika ubeti. Hatutajihusisha na mjadala huu katika somo hili bali tutashughulikia kina kama kitamkwa cha mwisho katika mishororo ya beti za tenzi husika. Tutachunguza jinsi kina hiki kinavyojitokeza katika tenzi hizi.

Katika utenzi wa M N M, vina vinalingana katika mishororo mitatu ya kwanza katika kila ubeti. Mtunzi amedumisha kaida ya kufananisha vina katika mwisho wa mishororo lakini katika beti za 174 na 252 hakuzingatia ulinganisho huo kama tutakavyoona hapa chini.

(174) Khamisi na tuagane
takwenda maji hayanwe
nikifa nenda kanene
Mayasa nisalimia

Maoni yetu ni kwamba mtunzi ni kama alichukulia kina kama irabu ya mwisho wa mstari lakini siyo kitamkwa kama ilivyo kaida ya vina. Mifano ifuatayo inatilia nguvu madai hayo yetu:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| M K M: ( 256) | **-a** | ( 265) | **-za** | ( 276) | **– o** |
| | **-a** | | **- zwa** | | **-o** |
| | **-ya** | | **- za** | | **-yo** |
| | **-a** | | **- a** | | **-a** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (294) | **–i** | (444) | **- yo** |
| | **-i** | | **-yo** |
| | **-ya** | | **- o** |
| | **- a** | | **- a** |

Aidha kina cha kibwagizo katika beti ni **-a** lakini wakati mwingine kinabadilikabadilika na kuwa **– ya, -wa, -za** au **-ja** kama ilivyo katika mifano ifuatayo: - **ya** (7), -**wa** (18), - **wa** (48), - **wa** ( 57), - **ya** (7), -**wa** (18), - **wa** (48), - **wa** ( 57), - **ya** (167), - **ya** (211), - **wa** (267), - **ya** (303), - **ya** (356), - **wa** (423), - **wa** (435), - **ya** (446), - **wa** (448), - **wa** (463), - **za** (492), -**wa** (527) – **ya** (564), - **ya** ( 590), - **ya** (650), - **wa** ( 661), - **wa** (670), -**ya** (674), - **wa** (719), - **ya** (744), - **ya** (715) , - **ya** (772).

Katika S Y N M, mtunzi pia amekiuka kaida ya ufanonisho wa vina. Kwa mfano,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **(5) -ri** | **(38) – o** | **(40)-e** | **(51)-tu** | **(99)-ri** |
| **-ri** | **-o** | **-ye** | **-to** | **-ri** |
| **-li** | **-yo** | **-e** | **-tu** | **-li** |
| **-a** | **-a** | **-a** | **-a** | **-a** |

Mifano mingine, kama hii, inapatikana katika beti za 60, 188, 230, na 352. Kina cha mshororo wa mwisho katika kila ubeti ni [-**a**] lakini tunaona ya kwamba wakati mwingine kinabadilika badilika na kuwa – **ya** au **wa**. Kwa mfano, - **wa** (22), - **wa** (23), - **wa** (27), - **wa** (49), - **wa** (172), - **wa** (200), - **wa** (216), - **wa** (241), - **wa** (266), - **ya** (274), - **wa** (320), - **wa** (352), - **wa** (378), - **wa** (393).

Washairi wengi wa Kiswahili hawatofautishi matumizi ya **–wa** na **–a** katika tungo zao. Wao hutumia yoyote ile. Hii ni kwa sababu **w-** ni kiyeyushi na kwa hivyo, hakuna tofauti kati yake na – **a** katika matumizi.

Kutotiririka kwa vina katika tenzi hizi kunatatiza mahadhi na mdundo wake. Mabadiliko haya yanapatikana pale ambapo wasanii hawa hawataki kiathiri maana. Kama wangeshikilia kudumisha mtiririko wa vina, maana iliyokusudiwa ingebadilika na hivyo kutatiza mawasiliano. Watunzi hawa wametumia uhuru wa mshairi kutimiza malengo hayo. Hii ni hatua mojawapo ya kunyanyua ushairi kutoka kaida zinazoshikilia sana mambo ya muundo katika mdundo. Jambo hili linawafanya wahakiki wengine kuona kama kwamba huu ni udhaifu wa msanii. (Abdulaziz 1968:82).

### 3.3.2 MIZANI

Mizani ni silabi zinazopatikana katika neno. Kaida ya idadi ya mizani katika tenzi huwa ni nane katika kila mshororo. Mtunzi wa S Y N M, amekiuka kaida hii mara kwa mara. Wahakiki wengine wanaita matokeo ya ukiushi huu wa urari wa vina na mizani uguni. Kwa mfano, S.M. Kuvuna na wengine (1992:16) wanasema kuwa shairi guni ni shairi ambalo mtunzi amejaribu kutekeleza urari wa vina na mizani lakini akashindwa.

Matokeo yake katika utenzi wa S Y N M ni kuwepo kwa mishororo ambayo ina mizani 6, 7, 9, 10 na hata 11, kama tunavyoshuhudia katika beti zifuatazo:

130. 'Bassi leo abadani
Tena narudi nyumbani
Agheru Shetani
Najuta na kuzaliwa.

23. 'Awe mtoto wako
Ao ni ndugu yako
Isiwe jelani yako
Siye anayetakiwa.

83. Kabla ya kumweka chini
Dadaye alibaini
'Hiyo deni nampani
Sina nnalodaiwa.'

155. Bwana Mwenye kaondoka
Na jumbe akapanganyika
Kwa Bwana Liwali hakufika
Kaona kuchelewea.

319. Kaanza kwa wanawake
Kulisha uganga wake
Aliye mchawi aoneke
Kilevi kitamjia.

114 Yale kwisha kubaini
Alijibu Binti Ramadhani
'Mkewe huyu yaqini
Kila mtu anajua..

Mifano mingine inapatikana katika beti 9, 27, 40, 82, 110, 136, 152, 153, 158, 166, 199, 201, 204, 211, 248, 250, 253, 263, 272 na 336.

Tunaweza kudai kuwa mtunzi amefanya hivyo bila kujali athari itakayotokea haswa katika mdundo wa utenzi unapoimbwa au kukaririwa. Kuna uwezekano kuwa mtunzi wa utenzi huu hakutaka kubadilisha maana kwa kuzingatia kaida ya mizani nane katika kila mshororo. Amefanya hivyo ili kudumisha maana ya ujumbe anaowasilisha.

Utenzi wa M N M umezingatia sana idadi ya mizani nane katika kila mshororo. Pale ambapo mtunzi alikuwa na upungufu wa idadi ya mizani, alitumia mbinu ya mazida na wakati inapokuwa zaidi, anatumia inkisari. Matokeo yake yanadhihirisha ubunifu wa hali ya juu kwa kudumisha maana, mdundo na mahadhi ya utenzi. Jambo hili linaleta tofauti ya kudumisha maana kati ya utenzi huu na ule wa M N M.

Watunzi wa tenzi hizi wametumia uhuru wa mshairi. Uhuru huu umetumiwa kwa ubunifu zaidi kiasi cha kutotatiza mdundo wake.

## 3.4 TAMATHALI ZA USEMI

Katika kijisehemu hiki, tumechunguza jinsi wasanii wa tenzi husika walivyotumia lugha katika viwango vya maana pamoja na mpangilio wa maneno ili kuzua maana mpya au kusisitiza. Tumechunguza jinsi ukiushi wa lugha unavyosababisha matokeo ya tamathali za usemi kama vile taswira, tashibihi, istiari, tashihisi, metonimia, chuku, takriri, tabaini, balagha, usambamba, kejeli, taharuki, urejeshi, nahau, methali, litifati na onomatopia. Tumeanganzia matumizi ya kila mojawapo ya dhana hizo ama udhaifu au ufanifu pamoja na uamilifu wake katika kuchangia uundaji wa kazi husika.

### 3.4.1 TASHIBIHI

Kunga hii imetumiwa na watunzi wa tenzi za M N M na S Y N M, katika kuwasilisha mawazo yao kwa njia ya kufananisha vitu. Katika S Y N M, kuna mifano kama ubeti wa 20:

' Yatakimbia majeshi
(H) upati tena bireshi

Ila kwa kitu ni keshi
Mfano wa kununua.'

Hapa mhusika Binti Jizi anamsisitizia Binti Hanifu kuwa zamu yake imefika ya kutoa mmoja wa familia yake kwa kundi la wachawi. Kile kitendo cha kumtoa mmoja wa aila zake kinafananishwa na kununua kitu kwa pesa taslimu. Ufananisho huu unajaribu kutilia nguvu umuhimu uliokuwepo wa Binti Hanifu 'kulipa' kuendelea kuwa mmoja wa wanachama wa kikoa cha wachawi. 'Malipo' hayo pia yangemkinga kutokana na kukimbiwa na wenzake hao.

Ufananisho huo vilevile unatuchorea picha ya mnunuzi wa bidhaa fulani. Ili kupata bidhaa hiyo, lazima mteja huyo atoe kiasi cha fedha kinachotakikana. Naye Binti Hanifu lazima angetoa kile kilichohitajika kwa kundi lake bila ya kupunguza.

Mfano mwingine ni katika ubeti wa 96.

Binti Hanifu mdogo
Alibaki zigozigo
Kafungwa kama muhogo
Sakti ameturia.

Katika kutumia "Kafungwa kama mhogo, sakti ameturia," mtunzi anatuchorea picha mawazoni ya namna Salima Binti Hanifu alivyokuwa amefungwa na kundi la wachawi, tayari kuuawa. Hali hiyo inafananishwa na mzigo wa mhogo uliofungwa na ambao huwa hauna namna ya kujitetea. Salima alikuwa ametulia kwa sababu labda alielewa vizuri kuwa hangefanya lolote ili kujinusuru. Picha hii inatuonyesha pia kiwango cha

ukatili uliotekelezwa na wachawi hao kwa mwanamke huyo.

Matumizi ya "Maji yakimwagika, hayazoleki kama taka" (125), yanaonyesha kuwa hata kama hii ni methali, kuna ufananisho wa vitu viwili. Msemo huu unatumiwa na Bwana Shambi kuonyesha kuwa haingewezekana kurudisha Salima nyumbani kama alivyopendekeza mhusika Binti Ramadhani. Haingewezekana kwa sababu hakuna dawa ambayo ingemtibu kurudia hali yake ya kawaida. Pia angewataja wachawi hao wote. Hapa Salima analinganishwa na maji ambayo tayari yamemwagika. Hangenusurika.

Tashibihi zingine zinazojitokeza katika utenzi huu zinapatikana katika ubeti wa 223.

Na kuja kampa yeye
Mfano kama nduguye

Hapa Bwana Shambi anaota akimpa Nguvumali koja kama kwamba ni ndugu yake. Shambi ni mchawi aliyeshiriki kumuua Salima. Nguvumali ni mganga ambaye angekuja kugundua aliyehusika na mauaji hayo. Kwa hivyo, msanii hapa anafananisha ushirika wa maadui hawa na ndugu wawili ili kutuchorea picha ya mchawi huyu akimtolea Nguvumali vyombo vyake vya uchawi kwa hiari. Mifano mingine inapatikana katika beti zifuatazo:

S Y N M : 276.

Polisi (h) ao wawili
Kama ni kumi na mbili
Walipanda basikeli
Wanakula kama njiwa.

334. Akautoa ulimi

Unawaka kama lami

'Mtu nimeua mimi'

Jamii wakasikia.

Katika utenzi wa M N M, kunga hii imetumiwa kwa upana mno. Kwa mfano, ubeti wa 10.

Sifa zake Mukhtari

siwezi kuzikadiri

kama mai ya bahari

na mani ya shajaria.

18. Ali mzuri wa sura

na uso wake mdawara

na mato yake king'ara

kama wanda wa kutiwa.

Katika ubeti wa 10, sifa za Mtume Muhammadi S.A.W. zinafanaishwa na maji ya bahari au matawi ya mti. Tashibihi hii inatuchorea picha mawazoni juu ya sifa maridhawa za Mtume Muhammadi S. A. W. ambazo haziwezi kukadirika.

Urembo wa Mayasa uliyafanya macho yake yang'are kama yaliyotiwa wanja. Kwa mfano, Mato yake king'ara kama wanda wa kutiwa.

Hapa tunapata picha ya urembo wa ajabu wa msichana huyu uliowafanya masultani, wakwasi na mashujaa kutoka nchi za mbali kutamani kumuoa.

Maji matamu kama asali (173). Maji haya ni ya ajabu kwa sababu yalikuwa yanamilikiwa na jinni hatari aliyetoa ndimi za moto (181).

Mikidadi mkali kama sadi (301). Ukali na ushujaa wa Mikidadi unafananishwa na ule wa simba.

Wakamzinga kwa wote kama kidole na pete (320) - Kuzingirwa kwa Mikidadi na mamia ya maadui katika vita kunafaninishwa na vile kidole kinavyozingirwa na pete. Hapa tunachorewa picha ya vile Mikidadi alivyozingirwa na watu wengi katika vita. Picha hii inazua taharuki ya kutaka kujua kama mhusika huyu angenusurika au la. Vilevile inatuonyesha uajabu wa Mikidadi katika vita.

Mbinu hii pia inapatikana kaitka ubeti wa 529:

Ameikabili jeshi
wala hana tashwishi
ni kama mwenye atashi
mai akiyatapia

Hapa, ujasiri na heka heka za mhusika Mikidadi katika vita zinalinganishwa na mwenye kiu anayeng'ang'ania maji. Mifano mingine ya kunga hii inapatikana katika beti zifuatazo: 29, 20, 540, 583, 756, na 757.

Matumizi ya kunga hii katika tenzi hizi yanamwezesha msomaji kupata na kujenga picha kamili ya hali au kitu kinachozungumziwa. Hivyo basi kuonyesha ubunifu wa hali ya juu wa kufananisha hali au vitu kwa njia ya moja kwa moja. Watunzi hawa wamefaulu sana katika matumizi ya mbinu hii kwa kuhamisha maana na sifa. Matumizi haya ya kufananisha licha ya

kujenga taswira, yanawasilisha hisia za ndani za wasanii kwa njia ya umbuji.

### 3.4.2 SITIARI

Watunzi wa tenzi hizi wametumia mbinu hii ya kufananisha vitu, watu au hali kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

Katika utenzi wa M N M mbinu hii imetumiwa kwa kulinganisha mashujaa na wanyama wakali kama chui na simba. Kwa mfano, tazama beti zifuatazo:

221 Ewe Luhani adui
na kamba hunitambui
ndimi simba ndimi tui
nawe utajionea

253. Kaumu ikaeleza
twakupa huyu wa kwanza
jina lake ni Hamza
simba wa Mola twaa.

255 Isimuye ni Abbasi
naye ni simba mtesi
naye usimrahisi
ushujaa wamwelea

256. Na wa tatu twakwambia
ndiye simba akilia
na jadi yao ni moya
nawe hao wakwelea

Katika ubeti wa 221, Sheikh Luhani anajitanguliza kwa kujiita simba na chui. Sifa hizi zinatokana na ushujaa wake wa kivita wa hali ya juu. Licha ya kujipa sifa hizo za wanyama wakali, anashindwa na kuuawa na Mikidadi.

Katika beti za 255 na 256, wahusika Hamza, Abbas na binamu yake wanajitanguliza kuwa wao ni simba. Wahusika hawa walikuwa mashujaa

na washirika wa Mtume Muhammadi S. A. W. Hawashindiki katika vita kama tunavyowaona katika utenzi huu. Hata Mikidadi alishindwa na Ali (619). Tunaona kuwa baada ya Ali kumshinda Mikidadi, Mayasa anamwita Ali simba (620). Vilevile katika ubeti wa 599, Ali anajiita simba wa Mungu. Alipigania Mwenyezi Mungu na Mtume wake Muhammadi S. A. W. katika vita vitakatifu.

Katika ubeti wa 295, Mikidadi pia anajifananisha na simba. Sifa hii inarudiwa kwake na jemedari wa Sultani Kisiri, baada ya kushindwa na kutwaliwa na Mikidadi kama tunavyoona katika ubeti ufuatao:

M N M; 338 . Kamwambia Mikidadi
Ewe shujaa asadi
Ya nini ikujifisidi
Bara ukaizuwia

Sultani Kisiri alipoona vile majeshi yake yaliyotambulika na kwa ushujaa wao yalivyoshambuliwa na kushindwa na Mikidadi, anagadhibika sana na kuyafananisha na kuku kutokana na uoga waliokuwa nao. Kwa mfano, ubeti wa 401:

Kuona kwake maliku
wote wenele vikapu
kaweta enyi zikuku
kwa ghadhabu kumngia

Katika utenzi wa S Y N M pia kuna matumizi ya mbinu ya sitiari kama tunavyoona katika beti zifuatazo:

36. Akalia Binti Jizi
Shambi akasema wazi
'Mimi kunifanya ngozi
Sitaweza kuridhia.

37. Mimi kunifanya ngoma
Sitakubali wa chama
Bora mtoe gharama
Na menginewe sikia

Katika ubeti wa 36, mhusika Shambi analalamika kwa kusema kwamba hatakubali kufanywa ngozi yaani anakataa kutumiwa vibaya kwa kuelekezewa kila lawama na wenzake. Sitiari ya aina hii inarudiwa katika ubeti wa 36, ambapo neno ngoma linatumiwa kwa maana ya ile ile ya mwanzo.

Kutokana na mifano hiyo, tunaweza kusema kuwa kunga hii ya sitiari haikujitokeza sana katika utenzi wa S Y N M kama ilivyojitokeza katika M N M. Ufananisho huu unalenga hadhira na kuifanya kujenga picha mawazoni inayoiwezesha kuelewa vyema zaidi kupitia taswira hiyo. Vilevile inadhamiria kujenga masafa ujumi ya karibu kati ya utenzi na hadhira.

### 3.4.3 TASHIHISI

Hii ni mbinu ya kukipa kitu sifa za binadamu za kuwaza, kuongea, kutoa uamuzi, kutembea, na kadhalika. Mbinu hii imejitokeza mara moja tu katika utenzi wa M N M. Kwa mfano, Kwenu kumekukataa (335). Mahali panapewa sifa ya biandamu ya kutoa uamuzi wa kumkataa anayerejelewa. Tamathali hii inatumiwa kwa jemedari wa Kisiri aliyeshindwa na Mikidadi na kufungwa kwa kamba. Inaleta mtwezo wa aina fulani kwa jemedari huyo. Katika utenzi wa S Y M N, hatukupata matumizi ya mbinu hii.

### 3.4.4 METONIMIA

Hapa ni pale ambapo jina la kitu fulani linasimamia kitu kingine. Katika utenzi wa M N M Mikidadi anapokea pete kutoka kwa baba yake Mayasa kama ishara ya kumkubalia kuoa binti yake. Hapa pete inasimamia ndoa.

Sultani Kisiri anavua taji lake na kumpa Mikidadi (463). Taji hapa linasimamia ufalme. Kwa hivyo, kitendo cha sultani cha kumkabidhi Mikidadi taji lake kina maana kuwa Mikidadi alipata nguvu na mamlaka yote ya kutawala nchi ile. Jambo hili linamkasirisha sana Waziri Mkuu wa Sultani Kisiri (467). Hapa tunaona dhana zinazokaribiana au zilizo sawa na zile zinazozungumziwa na mtunzi. Dhana hizi zimetumiwa kuupa ujumbe unaowasilishwa uzito zaidi.

Mbinu hii imefaulu kwa kuwasilisha mawazo ya msanii kwa kutumia vitu vinavyoeleweka katika maisha ya kila siku kusimamia dhana au vitu vingine. Kunga hii haikujitokeza katika utenzi wa S Y N M.

### 3.4.5 CHUKU

Hii ni mbinu ya kuelezea au kukuza jambo kupita kiasi. Katika utenzi wa M N M, mbinu hii imetumiwa kwa upana mno ili kutilia mkazo. Mambo mengi yanayozungumziwa yametiwa chumvi kupita kiasi. Katika ubeti wa 216, tunaambiwa jinsi Mikidadi alivyowakabili maadui zake peke yake na muda si muda anaua watu hamsini. Mtunzi anasema:

> Kajipeka kati mwao
> kwa siaha na zomeo
> alotinda mwida huo
> ni Khamsini rijaa (216).

Katika ubeti wa 279, tunaambiwa jinsi Mikidadi alivyokabili zaidi ya watu mia ambao hawakuweza kumshika. Aliua hamsini kati yao na kuchukua mali zao:

Na wane kamkamata
na wa tano na wa sita
hisabuye nilopata
khamsini kawondoa (279).

Katika ubeti wa 299, ushujaa wa mhusika Mikidadi unatiwa chumvi kupita kiasi:

Wakangia kupigana
kwa panga wakitemana
muda punde kiwaona
waeleo watu mia (299)

Tunaambiwa kwamba aliweza kukabili maadui mia tano (286) na kuwaua mia moja mara moja. Chuku ya aina hii inapatikana pia katika ubeti wa 317 ambapo Mikidadi anawaua mamia ya watu waliokuwa wamemzingira wakiwa wamejihami kwa mikuki na mapanga.

Aidha mali aliyodaiwa Mikidadi ya kulipia mahari imetiwa chumvi – (beti 147-152). Anaitishwa ngamia mia nne, ngamia hamsini wakiwa wamebeba mizigo na vito vya thamani kubwa, nguo za Kisomali mia saba, nguo za kichwani mia mbili, farasi mia weusi na vijakazi hamsini na kiasi kikubwa sana cha dhahabu.

Katika ubeti wa 749, licha ya kuwa Mikidadi alikuwa amefungwa kwa siku kadhaa bila maji wala chakula, anapofunguliwa, anapigana vilivyo na kuua watu wengi pamoja na Malik aliyekuwa amemchukua mkewe Mayasa. Hili si jambo la kawaida katika ulimwengu halisi. Mifano mingine ya chuku inapatikana katika beti zifuatazo: 328, 329, 360, 395, 597, 557, 748 na 753.

Katika utenzi wa S Y N M, tunaambiwa jinsi askari wawili, Mnyamwezi na Jaluo walivyowapiga wanakijiji ili wataje wale waliomuua Salima (280). Hatuoni uwezekano wa watu wawili pekee wakiwapiga watu kijiji kizima na kuwafanya wengine kuzirai.

Kwa kutumia mbinu hii, watunzi wa tenzi hizi wametumia ubunifu wa hali ya juu ili kuvuta hadhira na kuipa hamu ya kutaka kuendelea kusoma au kusikiliza. Kunga hii inazipa kazi hizo ladha na utamu wa kisanaa.

### 3.4.6 TAKRIRI

Urudiaji unajitokeza katika viwango vya silabi, vokali, neno, sentensi au ujumbe katika utungo kwa nia ya kusisitiza au kudumisha na kuboresha mdundo wa shairi.

Katika utenzi wa S Y N M, kuna takriri ya vokali **-a** katika kina cha kila ubeti. Hii ni sifa mojawapo ya tenzi. Kikaida, kina cha kibwagizo hukaririwa katika tenzi.

Taz. S Y N M, (74)

Anapotea porini
Upande ule wa pwani
Masikini masikini
Salima anapotea.

Katika ubeti wa 74, neno maskini maskini, linatilia mkazo jinsi Salima alivyokuwa anajipeleka kwa wachawi bila kufahamu kutokana na marogo. Mtunzi anaonyesha hisia zake za ndani.

Kulekule maporini (78) - inasisitiza mahali ambapo salima anapoingia. Mahali hapo ndipo palipokuwa na wachawi ambao walimuua.

Mfano mwingine ni kama (79).

Kamwona dada yake
Mzawa na baba yake
Jumla na mama yake
Pamoja wamezaliwa

Katika ubeti wa 79, neno yake linakaririwa ili kusisitiza unasaba baina ya Salima na dada yake Binti Hanifu aliyemtoa ili auawe.

Mtunzi amekariri Ewe mama! Ewe mama! (142). Maneno hayo yanasemwa na Bwana Mwenye kwa Binti Ramadhani aliyekuwa anamzuia kwenda kupiga ripoti juu ya kupotea kwa Salima. Takriri hii inaleta wazo kuwa Bwana Mwenye hakufurahia pendekezo la Binti Ramadhani. Ni kama kwamba aliona mwanamke huyu alikuwa anavuruga harakati za kumtafuta

Salima kwa lengo fulani.

Katika ubeti wa 232, Waje tena wale wale. Ndugu yangu yule yule. Hapa mtunzi anasisitiza unafiki wa mhusika Binti Hanifu anapoelezea juu ya kupatikana kwa ndugu yake Salima. Anajifanya kagundua maiti ya dada yake ilhali ni mmoja wa wale waliomweka pale.

Aina nyingine ya takriri inapatikana pale ambapo mstari unaomalizia ubeti unatumiwa kuanzia ubeti unaofuata. Kwa mfano, kibwagizo cha ubeti wa 273, Dalili ilitokea, kinarudiwa katika ubeti unaofuata (274) lakini mpangilio wake unabadilishwa hivi kwamba neno lililomalizia ndilo linaloanzia na kuwa, ilitokea dalili. Takriri hii inachukuliwa na washairi wengine kama bahari ya pindu (Kuvuna na wengine 1992: 17). Mifano mingine kama hii inapatikana katika ubeti wa 352, Vibao Vimeenea. Fungu hilo la maneno linaanzia ubeti unaofuata kama vilienea vibao (353).

Vilevile kuna takriri ya ujumbe. Ujumbe unaopatikana katika ubeti wa 338, juu ya idadi ya watu walioshiriki uchawi na ambao walimuua Salima unarudiwa katika ubeti wa 350. Kwa mfano, S Y N M:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 338 | Jumla ya wale watu | 350 | 'Anayekabidhi sirikali |
| | Wachawi sana watatu | | Wachawi watatu kamili |
| | Wa nne tena si mtu | | Wa nne amesafiri |
| | Amekwisha kujifia | | Akhera ameingia. |

Katika utenzi wa M N M, kuna takriri ya vokali katika kina cha utenzi. Vilevile kuna takriri ya maneno yanayomalizia ubeti wa 3, aibu mkamtia ambayo yanaanzia ubeti wa 4 kama, mkamtia aibu. Mifano mingine ni

kama ifuatayo:

Ndani kuwangojea (427). Mstari huu unarudiwa vivyo hivyo katika ubeti wa 428 bila kupanguliwa; ndani kuwangojea,

Na mali walotukuwa (73)
Mali waliotukuwa (74)

Hamza akamwambia (733)
Akamwambia hamza (734),

Mali zitungu zitungu (51) - maneno haya yanasisitiza wingi wa mali ambazo zililetwa na waposaji wa
Mayasa. Ondokeni ondokeni (209), kusisitiza amri. Hapa Mikidadi anaamrisha majeshi ya Sheik Luhani kutoka nje ya hema ili wapigane naye.

Katika ubeti wa 722, mbinu hii imetumiwa kwa ubunifu sana kama tunavyoona,

Enendani enendani
Upesini upesini
Mpateni mpateni
Asubuhi tauawa (722)

Hapa malaika anatumia takriri kutilia mkazo dharura iliyokuwepo ya Hamza na Ali kuharakisha ili wakamwokoe Mikidadi. Mifano mingine ya mbinu hii inapatikana katika beti 309, 630 na 711.

### 3.4.7 BALAGHA

Hii ni mbinu ya kuuliza maswali yasiyohitaji majibu. Kunga hii imetumiwa kwa wingi katika utenzi wa M N M. Kwa mfano:

Hughani akiomba
ni yupi mtaka ndoa
anitakae kuoa
napenda kumwangalia (26)

Hapa Mayasa anauliza swali kwa wanaume waliotamani kumwoa. Swali hilo ni changamoto kwa wanaume hao kwani hakuna angemuoa kwa kulipa mahari tu, bali ingewabidi kupigana naye ili yule ambaye angemshinda amuoe. Mayasa analirudia swali hilo katika ubeti wa 34 kwa madhumuni yale yale. Vilevile maswali hayo yanawakejeli wanaume waliotamani kumwoa na ambao waliamini kuwa mali yao nyingi ingewawezesha kumpata Mayasa bila tatizo.

Katika ubeti wa 88, swali la balagha linatumiwa ili kutilia mkazo ushujaa wa mhusika Mikidadi:

Ni mtu gani huyule
apiganaye hivile
hatuoni tangu kale
mtu kamaye mithaa. (88)

Watu walioshuhudia akipigana walistajabia umaarufu wake wa kivita. Taz. ubeti wa 89,

Au yule ni ruhani
au ni mwana wa jinni

aula ni sheitwani
aula ni malakaa

Pia katika ubeti wa 112,

Mashujaa ni wangapi
niliowanyesha mkupu
nawe utapita wapi
utakapokimbilia

Maswali hayo yameulizwa na Mayasa akiwa ameghadhibika sana kwa kuvuliwa kitambaa alichokuwa amevalia kichwani na usoni ili asionekane na waposaji wake. Maswali haya yamelengwa kumkejeli Mikidadi kwani Mayasa alidhani kuwa angemuua kama alivyowaua mashujaa wengine.

Katika ubeti wa 211, majeshi ya Sheikh Luhani yanapanda farasi tayari kwa vita na kuuliza adui Mikidadi ako wapi. Wanauliza;

Yuwapa mpiga kunga
Mbele ya mwenye ulaya

Swali hili linaonyesha mshangao waliokuwa nao kwa kushindwa Mikidadi alikuwa mtu wa aina gani. Mtu ambaye alidhubutu kumdunisha na kumtolea vitisho shujaa wao waliomtambua na kumtumikia. Majeshi haya yaliona kama kwamba Mikidadi alitamani kifo tu kwani kulingana na fikra zao walidhani wangemuua mara moja.

Sultani Kisiri anashangazwa na ushujaa wa kiajabu wa Mikidadi. Anashindwa mtu huyo ni wa aina gani ambaye majeshi yake yote

yalimkimbia na kumwachia silaha zao.

Mtunzi ametumia balagha kusisitiza mawazo ya sultani huyo (ubeti wa 351-353).

Uko wapi Mikidadi

Sikuze zimetimia ( 50).

Swali hili linaulizwa na Jabir anapoamua kuchukua mahari kutoka kwa wakwasi waliokuja kumposa Mayasa, kwa kisingizio kuwa Mikidadi alikuwa amekawia sana kurudi.

Walionapi asadi
Akaepuka na baa (604).

Swali hili ni kama changamoto kwa Mikidadi aliyetaka kupigana na Ali. Katika ubeti wa 609, Mayasa anatoa changamoto kwa Mikidadi kwa kushindwa kumnyang'anya mkewe Ali taji ili ampe Mayasa. Anamuuliza: (609)

Sifa ulizojisifu
na watu kuwatilifu
mbona leo una khofu
Mikidadi karejea

Maswali mengi ya balagha yanayoulizwa vitani yanasisitiza, kukejeli au kutoa changamoto kwa wanaoulizwa.

Kunga hii haijitokezi sana katika utenzi wa S Y N M. Hata hivyo, kuna mifano katika beti zifuatazo:

103 'Tafadhali dada yangu:
Mbona wanipa matungu?
Haswa nipe kosa langu
Nini nimekukosea.

127. 'Akisha rudi nyumbani
Utafanya dawa gani?
Wote wanamjuani
Waweza kusimuria.'

Maswali yanayoulizwa katika ubeti wa 103 yanazua hisia za huruma na masikitiko. Salima anauliza dada yake Binti Hanifu aliyemtoa ili auawe kwa kuteswa, "Mbona wanipa matungu? Nini nimekukosea." Mtunzi anamwonyesha Salima kutokuwa na hatia yoyote. Vilevile anatuonyesha kwamba hakukuwa na damu mbaya kati ya Salima na dada yake.

Swali lililo katika ubeti wa 127 linasisitiza kutowezekana kwa kuachiliwa kwa Salima Binti Hanifu na wachawi wale. Swali hilo pia linamkejeli Binti Ramadhani kwa kughairi katika mkataba wake na wachawi wenzake na kupendekeza kuwa Salima aachiliwe.

Matumizi ya kunga hii yanazipa tenzi hizi utamu na uzito wa lugha kama zinavyofanya tamathali zingine za usemi. Wasanii hawa wametumia kunga hii kwa ufanifu mkubwa katika kutimiza malengo yoa.

Tofauti iliyopo katika matumizi ya kuunga hii katika tenzi zote mbili ni umbo lake. Maswali yaliyopo katika utenzi wa M N M hayana alama ya kuulizia. Kinachomwezesha msomaji kuyatambua maswali haya ni umbo la sentensi. Maswali yaliyopo katika S Y N M yanatambulikana kwa urahisi kwa sababu yametumia alama ya kuulizia.

### 3.4.8 TABAINI

Kunga hii hutumika kusisitiza jambo kwa kutumia mtwezoBadala ya kutumia kauli chanya, kikanushi **'si'** hutumiwa. Mbinu hii haikutumika sana katika tenzi husika. Katika utenzi wa S Y N M, kuna mifano kama si urongo, kumaanisha ni kweli. Si wema, kumaanisha ni vibaya. Katika mifano hiyo tunaona kuwa badala ya mtunzi kutumia kauli chanya, anatumia neno **'si'** kutwezea hali anayozungumzia. Mtunzi anafanya hivyo kwa lengo la kusisitiza kwa njia isiyo ya moja kwa moja.
Matumizi ya kunga hii hayakujitokeza katika utenzi wa S Y N M.

### 3.4.9 USAMBAMBA

Hii ni kunga ambayo hulinganisha sehemu mbili ambazo zinakinzana. Mbinu hii inajitokeza pale ambapo pana matumizi ya semi mbili zinzopingana kimaana. Katika utenzi wa S Y N M, kuna mifano ifuatayo:

Mtwana na mjakazi (262)

Mkubwa wala mtoto (263)

Mabwana na kina mama (289)

Wakubwa hata watoto (179)

Wanaume na wanawake (160).

Ulinganishi huu unakinzana kimaana. Mbinu hii inaonyesha msisitizo wa mkusanyiko na wingi wa wahusika wanaozungumziwa na mtunzi.

Katika utenzi wa M N M, ubeti wa 89.

Au yule ni ruhani
au ni mwana wa jinni
aula ni sheitwani
aula ni malakaa

Katika ubeti huo, Mikidadi anadhaniwa kuwa pepo, jinni, shetani au malaika. Kwa upande mmoja, pepo na malaika wanashirikiana na ni kinyume cha shetani na jinni. Kwa hivyo, kundi moja linapinga lile lingine.

Kunga hii pia imetumika katika ubeti wa 301: tunakwenda tunarudi. Semi hizi zinapingana kimaana kwa sababu neno moja ni kinyume cha lile lingine. Mfano mwingine ulio na maana sawa na huu lakini wenye muundo tofauti ni huenda mbele kirudi (331).

Mifano mingine ya matumizi ya kunga hii ni kama:

Kuumeni na kushoto (325),

Kampa khabari za siri na za Dhahiri ( 490).

Mbinu hii imetumiwa kuwasilisha ujumbe kwa njia iliyo wazi na kwa kutilia mkazo ujumbe huo. Kwa kuonyesha machanganyiko unaokinzana. Hali hii inatupa taswira halisi ya kinachozungumziwa.

### 3.4.10 KEJELI

Hii ni mbinu ambapo mhusika husema au hufanya kinyume cha matarajio au anavyokusudia. Katika utenzi wa M N M, mbinu hii imejitokeza pale

ambapo mhusika Jabir anapomwambia Mikidadi kuwa yeye pamoja na watu wa ukoo wake wangefurahia ikiwa Mikidadi angemwoa Mayasa kama inavyojitokeza katika ubeti ufuatao:

Na kwamba wataka ndoa
ya Mayasa kumuoa
twazidi kufurahiwa
sote twayapenda (139)

Hii ni kinaya kwa sababu Jabir hakufurahia uamuzi wa Mayasa wa kukubali kuolewa na Mikidadi ambaye ni masikini.

Maneno ya mhusika Jabir katika ubeti huo yanapingana na njama yake ya kudai posa ya mali nyingi ili Mikidadi ashindwe kulipa (134). Tunaona kuwa hata hapo awali alikuwa anamshawishi bintiye asikubali kuolewa na Mikidadi ambaye ni yatima, fukara ambaye hata hana mtumwa na kutekea Mayasa maji (123):

Huyu ni mwana yatima
Hatimizi darahima
Hapati hata kituma
Cha maji kukutekea

Katika ubeti wa 165 Jabir anampa Mikidadi muda wa miezi mitatu wa kukusanya mahari ili ashindwe. Mikidadi anarudi na mali yote aliyoagiziwa huku akiadamana na Mayasa aliyemtwaa kutoka kwa mhusika Riyahi. Jabir anapomwona Mikidadi, anajifanya kuwa na huzuni. Anasema kuwa alipoona kuwa Mikidadi anakawia kurudi, alishikwa na huzuni kubwa mno kwa kufikiria pengine ameuawa. Anamwambia kuwa kwa vile amerudi,

huzuni yake imepungua (661). Hii ni kejeli kwa sababu tunamwona akipanga njama ya kumshika Mikidadi ili auawe na Mayasa arudishiwe waposaji wake (673). Anampongeza Mikidadi kwa kumtwaa Mayasa – 661:

Jabiri akamwambia
tangu ulipopotea
shughuli zilitungia
tukamba umeuawa

Katika ubeti wa 227, Sheik Luhani anamkejeli Mikidadi kwa kumwambia kuwa yeye (Mikidadi) alitaka kumwoa Mayasa lakini akakataliwa.

Waziri Mkuu wa Kisiri anajifanya kushangazwa na ushujaa wa Mikidadi na kupendekeza kuwa apewe cheo na Sultani (444) ilhali alikuwa anapanga njama ya kumwangamiza Mikidadi ili wachukue mali yake. Anamshauri Sultani kumlisha Mikidadi simba (448):

Wewe una simba wako
Hula watu kila siku
Tumwambie ende huko
Akenda nae taliwa

Katika utenzi wa S Y N M, baada ya Salima kutangazwa kuwa amepotea, wachawi waliomuua wanaungana na wanakijiji wengine katika harakati za kumtafuta (134).

Katika ubeti wa 168, mama Binti Ramadhani anataka kuchoma ubani kabla ya kuanza shughuli za kumtafuta Salima. Hii ni ishara ya kuomba dua ili shughuli hiyo ifanikiwe. Tunaelewa vizuri kuwa mhusika huyo alikuwa

mmoja wa wauaji wa Salima. Vitendo vyake vinapotosha. Anataka kuwaghilibu wanakijiji waamini kuwa yeye hakushiriki katika mauaji hayo. Bwana Shambi, ambaye ni kiongozi wa wachawi waliohusika katika kutoweka na kifo cha Salima anapendekeza Nguvumali aitwe ili asaidie katika kumtafuta Salima. Anasema kuwa kama Nguvumali angekuja na kufanya uganga wake, Salima angepatikana (184, 185):

<u>S Y N M</u>:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 184 | Bwana Shambi kalatwili<br>Na kujitia fahari:<br>'Hapa aje Nguvumari<br>Ndio haswa walekea. | 185. | 'Nguvumali afike<br>Afanye uganga wake<br>Na kiumbe aoneke<br>Mimi ninahitajia.' |

Shambi anaendelea kusema kuwa kama kutakuwa na gharama yoyote ya kumleta Nguvumali, yeye angegharamia (196) na anatia sahihi barua ya kumwalika (197).

Katika ubeti wa 233, Binti Hanifu anasema kuwa amemwona dada yake ndani ya banda. Anaendelea kusema kuwa dada yake Salima alipokuwa anavunja kuni, banda lilimwangukia akafa. Watu tayari walikuwa wamemtafuta Salima bandani hilo lakini hawakumpata. Kwa hivyo, kinaya kinajitokeza katika usemi wa mhusika huyu, kwani yeye pamoja na wachawi wenzake walikuja kumweka baadaye.

Kutokana na mifano hiyo, tuliyotoa katika tenzi hizi, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa kunga hii imefanikisha kazi hizi kwa kuwasilisha ujumbe kwa njia ya ubunifu wa hali ya juu. Mbinu hii imefanikiwa katika kukuza kazi zenyewe kiasi cha kufanya wasomaji kuwa na taharuki ya kutaka

kujua zaidi yatakayotokea.

### 3.4.11 TAHARUKI

Istilahi hii hutumiwa kuelezea hamu kubwa aliyonayo msomaji ya kutaka kujua zaidi katika kisa. Katika utenzi wa S Y N M mtunzi ametumia kunga hii kwa kiasi kikubwa na kwa ufanisi. Katika ubeti wa 40, Binti Hanifu anaamrishwa na kundi la wachawi atoe mmoja wa jamaa zake ili auawe. Akishindwa kufanya hivyo ajitoe mwenyewe. Hapa tunakuwa na hamu ya kutaka kujua kama atamtoa nduguye na kama atamtoa, atatumia njia gani.

Salima Binti Hanifu anaporogwa na kuanza kuelekea porini bila kujua, tunapatwa na hamu na shauku ya kutaka kujua zaidi kitakachotokea (68). Hamu hii inazidishwa na mtunzi anapotwambia kuwa mwanamke huyo alidhani kuwa anaenda huko kuvunja kuni.

S Y N M 72:

> Mwenyewe alijidhani
> 'Nakwenda kuvunja kuni'
> Fikra zake moyoni
> Hajui anapotea.

Salima anapoachwa msituni na wachawi (95), tunajiuliza kama chochote chaweza kutokea ili kumwokoa. Tunajiuliza je, dada yake Binti Hanifu angebadili nia na kuja usiku kumwokoa? Mavyaa yake, Binti Ramadhani angekuja kuokoa mke wa mwanawe? Au wanakijiji wangempata kabla hajauawa? Maswali haya yanatuchochea tusome zaidi ili tupate majibu yake.

Wakati Bwana Shambi anapopendekeza Nguvumali aitwe ili asaidie kumtafuta Salima, tunapatwa na hamu ya kutaka kujua kitakachotokea (184). Tunajiuliza kama Nguvumali ataweza kuwatambua wauaji akiwepo Shambi au tayari alikuwa amefanya uchawi wake ili asitambulike? Maswali kama haya yanatupa ari ya kusoma zaidi. Nguvumali anapoingia, wasomaji wana hamu ya kutaka kujua zaidi yatakayotokea.

Katika utenzi wa M N M Mikidadi anapoamua kwenda kupigana na Mayasa, tunataka kujua kama angefanikiwa. Anapomshinda Mayasa na kukubali kulipa mali yote aliyodaiwa kwa muda wa miezi mitatu (166) bila kulalamika, wasomaji wana hamu ya kujua jinsi Mikidadi angepata mali hiyo licha ya kwamba alikuwa masikini sana. Katika ubeti wa 155, hata mjomba wake haamini kuwa Mikidadi angeweza kupata mali hizo zote. Anaona ni kama Mikidadi alikuwa na wazimu.

Mikidadi anapomuaga mtumwa wake, Khamisi (174) na kukutana na jinni mwenye kutoa ndimi za moto, tunashindwa vile angeweza kukabiliana na yule jinni (179).

Wakati Sultani Kisiri anapowatuma majeshi yake elfu moja (314) ili kumshika au kumuua Mikidadi, tunashindwa kuelewa kama mhusika huyu angenusurika. Mikidadi anaporudi kutoka safarini, anapata mkewe Mayasa tayari ameolewa na Sultani Riyahi. Hapa hadhira inakuwa na hamu ya kujua kitakachotendeka.

Bwana Jabir anapopanga njama ya kumteka nyara Mikidadi na

kumyang'anya Mayasa, msomaji anajiuliza kama angefanikiwa. Mikidadi anaposhikwa na kufungwa ili akauawe, tunakuwa na hamu ya kujua kama atauawa au ataokolewa.

Matumizi ya kunga hii yamezifanya tenzi hizo ziwe za kuvutia na kunata hadhira kwa kujenga hamu ya kutaka kujua zaidi. Kwa kufanya hivyo, hamu inayojengeka inamwezesha msomaji wa kazi hizi kusoma kwa kasi zaidi bila ukinaifu. Mbinu hii imewasilishwa katika tenzi hizi kwa kiwango cha juu sana na kwa ubunifu wa hali ya juu.

### 3.4.12 MBINU REJESHI

Hii ni mbinu ambapo msanii huelezea matukio yaliyokwisha kufanyika. Watunzi wa tenzi hizi wanatufahamisha yaliyokwisha tendeka hapo nyuma katika tenzi zao. Katika utenzi wa S Y N M, ubeti wa 104 na 105, tunaelezwa uhusiano kati ya Salima Binti Hanifu na dada yake Binti Hanifu huko nyumbani kwao. Tunaambiwa kuwa walikuwa na uhusiano mwema. Waliishi vizuri kwa amani na ushirikiano na Salima hakuona kosa lolote alilowahi kumfanyia dada yake ambalo lingemfanya amtoe ili ateswe namna alivyoteswa.

Katika beti za 108 na 116, tunafahamishwa kuwa Salima alikuwa ameolewa na mtoto wake Binti Ramadhani ambaye hawakusikizana. Kwa hivyo, mhusika Salima hakushangazwa na kitendo cha Binti Ramadhani cha kukubali atolewe ili auawe. Vilevile tunafahamishwa kuwa Salima tayari walikuwa wamekosana na mumewe na walikuwa wanataka kuachana:

S Y N M: 119.

'Haswa huyu mkwe wangu
Akimkataa mwanangu
Lakini yako mafungu
Ya wema yanifanyia.

Hatujaonyeshwa au kuelezwa kwa njia ya moja kwa moja juu ya kuuawa kwa Salima na kutiwa bandani bali tuanelezwa baadaye kama mambo hayo tayari yamefanyika. Tunasimuliwa mambo hayo kupitia mawazo ya mhusika Shambi. Anakumbuka vile walivyofanya na wahusika wengine baada ya kumuua Salima (225-229).

Katika utenzi wa M N M, ubeti wa 13, tunarejelewa maisha ya Suwedi, baba yake Mikidadi na jinsi alivyokuwa na mali nyingi. Tuanelezwa kuwa mali hiyo iliisha na akafa masikini. Jambo hili lilimfanya Mikidadi asipate chochote cha kurithi. Kwa hivyo, hangeweza kuoa. Urejeshi huu unatufanya tuelewe asili ya umaskini wa Mikidadi.

Katika ubeti wa 654, tunaelezwa kuwa ndugu yake Sultani Riyahi alikuwa tayari ameuawa na Mikidadi wakati alipokuwa anamnyang'anya Mayasa. Hatukufahamishwa jambo hili hapo awali. Ujumbe huu unamfanya msomaji aelewe kuwa Sultani Riyahi alikuwa amemtuma nduguye kumposa Mayasa kwa niaba yake.

Matumizi ya mbinu hii yamefaulu katika tenzi zote mbili kumwezesha msomaji kujua yaliyotokea hapo awali na ambayo hakusoma yalipokuwa yakitendeka. Kunga hii inampa msomaji msingi na asili ya matukio muhimu katika hadithi. Hivyo basi hii ni mbinu muhimu ya kuendeleza ploti.

### 3.4.13 NAHAU

Hii ni misemo ya picha inayofumbata maana. Katika utenzi wa S Y N M, kunga hii imetumika kwa kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kisanaa .Kwa mfano, Pweza makaa kujiparia (186), kwa maana kuwa kwa kupendekeza kwamba Nguvumali aitwe ili asaidie kumtafuta Salima, Bwana Shambi alikuwa anajitia hatarini.

Mule ngozi (262) - ina maana ya kuwapiga watu ili waseme aliyemuua Salima.

Viliingia vibao (280), watu walianza kuzabwa makofi na marungu. Jambo hili lilifanywa na askari walipokuwa wanapeleleza juu ya mauaji ya Salima.

Vibao vimeenea (352), watu walipigwa sana katika harakati za kufanya uchunguzi.

Wamepata ngozi zao (354), Polisi walikuwa wamepata watu wa kupiga kama vile mwamba ngozi hupindua ngozi katika kazi yake.

Kuja kunipaka vumbi (373) – Kuharibia jina. Bwana Shambi analalamika kuwa Nguvumali alimharibia jina kwa kudai kuwa alikuwa mchawi.

Katika utenzi wa M N M, kuna mifano ifuatayo:

Roho yake kuitupa (95), kwa maana ya kusalimu maisha ya uhai wake. Hapa Mayasa anamaanisha kuwa yeyote anayeamua kupigana naye, ni yule ambaye hana haja ya kuishi tena. Yaani ni kama kujiua mwenyewe.

Fumo na panga mumo kwa mumo -kumaanisha kuwa vita viliendelea kuchacha.

Mwana wa jaha na jaha - mwana wa kifalme mwenye sifa.Hapa Mayasa anajitambulisha kwa Mikidadi kwa kumtahadharisha kuwa yeye si mtu wa kuchezewa.

Niushikapo upanga - kwa maana ya kupigana vita. Mikidadi anatumia usemi huu kuonyesha kuwa ile mali yote aliyoangaziwa kulipia mahari angeyapata kwa vita.

Wote wakalie woga; kuogopa kupita kiasi. Askari waliotolewa na Sultani Kisiri ili wapigane na Mikidadi waliogopa sana hivi kwamba Mikidadi anatoa ripoti kwa Sultani kwa kutumia msemo huu ambao unatupa picha ya vile walivyokuwa na uoga wa kupigana naye .

Matumizi ya semi katika tenzi hizi yanaleta matokeo ya lugha yenye mnato inayovuta hadhira. Tumeona kuwa watunzi hawa wamefinyanga lugha na kubuni misemo ambayo inaleweka katika muktadha wake wa matumizi.

### 3.4.14 METHALI

Mifano ya methali katika utenzi wa S Y N M:

125. Bwana Shambi katamka:
'Maji yakimwagika
(H) ayazoleki kama taka
Na wewe unatambua.

381 Kirefu hakikosi ncha
Usione mocha mocha
Na vingi (h) uwa chachacha
Mbele vitakukimbia.

Katika ubeti wa 125, methali hiyo inaonyesha kuwa haingewezekana Salima kuachiliwa. Hii ni kwa sababu alikuwa tayari amerogwa akarogeka na hakuna dawa ambayo ingeweza kumponya. Vilevile aliwafahamu fika waliomfanyia uovu huo na kwa hivyo, angewasema.

Kirefu hakikosi ncha (381). Mtunzi ametumia methali hii kumaanisha kuwa hata kama wahusika Shambi na Binti Jizi walijaaliwa mali nyingi, mali hiyo ingekwisha kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Methali hizo zinadhihirisha ubunifu na uzoefu wa msanii wa mazingira pamoja na lugha ya Kiswahili. Mtunzi amefaulu katika kuhusisha lugha na mazingira yake pamoja na maisha ya kila siku.

Mbinu hii haikujitokeza katika utenzi wa M N M. Hii haimaanishi kuwa kazi hii ina upungufu au haijafaulu kwa kutotumia kunga hii.

### 3.4.15 LITIFATI

Hii ni mbinu ambapo mtunzi humwachia mhusika ajielezee mwenyewe. Katika utenzi wa S Y N M, mbinu hii imetumiwa pale ambapo badala ya kusimulia yaliyotokea, msanii anawaachia wahusika wazungumze wenyewe. Katika utenzi wote tunashuhudia majibizano kati ya wahusika. Kwa mfano ubeti wa 23:

> 'Awe mtoto wako
> Ao ni ndugu yako
> Isiwe jelani yako
> Siye anayetakiwa.'

Badala ya mtunzi kusimulia walivyofanya wahusika hawa, anawapa nafasi ya kujisemea wao wenyewe. Rej. S Y N M, ubeti wa 37:

'Mimi kunifanya ngoma
sitakubali wa chama
bora mutoe gharama
na miye nikitumia.'

Katika ubeti huo, mhusika Shambi anateta yeye mwenyewe badala ya kuteta kupitia kwa msimulizi.

Katika beti wa 103 (Rej. Uk. wa 85), Salima anajitetea kwa dada yake kutokana na mateso aliyoyapata bila sababu. Kwa kumwachia mhusika huyu ajisemee, mtunzi anamfanya msomaji aathirike na kumhurumia mhusika Salima.

Wakati mwingine mtunzi anaathirika na matukio katika hadithi na badala ya kutumia njeo ya wakati uliopita, anatumia wakati uliopo. Kwa mfano, katika beti zifuatazo:

S Y N M:

74. Anapotea porini
Upande ule wa pwani
Masikini masikini
Salima anapotea.

75 Salima Binti Hanifu
Anakwenda bila hofu
Zimempata harufu
Dawa zimemkorea.

76. Hakika wachawi (h) ao
Wamechapapo dawa zao
Huja wamtakao
Ndivo wanavotumia.

Anasimulia kama kwamba matukio yanafanyika wakati huo huo. Athari ya usimulizi wa aina hii wa mwandishi kujihusisha katika kisa chenyewe ni hatua mahususi ya kumwalika na kumfanya msomaji aathirike kama yeye. Jambo hili linamfanya msomaji kuwa na uhusiano wa karibu na kisa kinachosimuliwa.

Katika utenzi wa M N M, mtunzi pia ametumia mbinu ya litifiti kwa kiasi kikubwa. Tunashuhudia majibizano ya moja kwa moja kati ya wahusika . Vile vile wahusika katika utenzi huu wanajitambulisha wao wenyewe. Taz. mifano katika beti zifuatazo:

94. Mayasa kamkhubiri
ndimi bnti Jabiri
ndimi mwingi wa jeuri
nikifanya yalekea

178. Mikidadi akanena
ewe jinni maleuna
kama wanijua sana
hayo usengenambia

226 Kamba ndimi Mikidadi
Ibnu 'lAswadi
nawe leo huna budi
nakuona kupotea

599 Ndimi simba wa Muungu
ndimi mueka mafungu
ndimi mwana wa makungu
hata jua likatua.

Wakati mtunzi wa S Y N M anapompa mhusika fulani nafasi ya kujisemea huwa anatumia alama za kunukuu katika kunakili maneno yao. Lakini katika M N M, alama hizi hazikutumika.

Kuunga hii imefaulu sana katika kujenga masafa ujumi kati ya hadhira na hadithi yenyewe. Inamfanya msomaji ahisi kama kwamba anawasiliana

moja kwa moja na wahusika.

### 3.4.16 ONOMATOPEYA

Mbinu hii hurejelea sauti inayoigiza sauti ya mwendo au mapigo ya kitu fulani.

Mtunzi wa S Y N M ametumia kunga hii kwa ubunifu wa hali ya juu. Ubunifu huu unasababisha athari zinazotokana na matumizi ya kunga hii. Kwa mfano, ubeti wa 73.

Sakarani ya kurogwa
Aliona zigwazigwa
Kumbe anafukuzwa
Porini anapotea.

Ubeti huo unaelezea vile marogo yalivyomwathiri mhusika Salima. Neno zigwazigwa linaelezea vile alivyokuwa anaona vitu. Alikuwa ameathirika hivi kwamba macho yake hayakuweza kuona vizuri. Neno hili linatufanya kujenga picha mawazoni ya mtu anayekimbia kwa hatua kubwa na ambaye amejawa na hofu kubwa.

Katika ubeti wa 8, mtunzi ametumia neno fufufu kwa kuhakikishia hadhira yake kuwa hadithi atakayoitoa ni ndefu mno na yenye mambo mazito. Hapa tunapata picha ya urefu na uzito wa kimaudhui wa utenzi huu.

Neno pupuripupuri (77) ni tanakali ya sauti linaloelezea jinsi Salima alivyokuwa anatembea. Hapa tunapata taswira ya mtu anayejaribu kuharakisha lakini hana umadhubuti wa kutembea. Anaanguka kisha anainuka kwa haraka na kwendelea na safari.

Katika ubeti wa 96, neno zigozigo, na matokeo ya sauti katika maneno ndogo na muhogo yanaonyesha kuwa msamiati huo una uhusiano unaoleta taswira fulani. Maneno haya yanaleta picha ya mja aliyefungwa na ambaye ni hohehahe. Kupitia maneno hayo tunaona jinsi mhusika Salima alivyoteswa kinyama.

Katika utenzi wa M N M, ubeti wa 733, neno nyumanyuma limetumika kionomatopeya. Linatufanya kujenga picha na kuona vile Sultani Riyahi alivyorudi nyuma alipomwona shujaa Ali. Tunajengewa taswira ya mtu mwenye woga na hofu anayerudi nyuma baada ya kumwona adui ambaye angemuua.

Mbinu hii imefaulu kutuwasilishia ujumbe ambao unatufanya kuchora picha ya hali na vitendo vinavyosimuliwa.

## 3.5 PLOTI

Mbinu za lugha zimetumiwa katika kuendeleza msuko wa tenzi hizi. Baadhi ya mbinu hizo ni taharuki na urejeshi. Ploti ya utenzi wa S Y N M ni sahili. Utenzi wenyewe umegawika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ambayo ina beti tisa ni utangulizi. Katika beti tatu za kwanza, mtunzi anaabudu ambapo anaomba Mwenyezi Mungu amjalie kutunga bila matatizo yoyote. Kutoka ubeti wa nne hadi wa tisa, mtunzi anatanguliza hadithi yake kwa kuelezea dhamira yake ya kutunga.

Sehemu ya pili ya utenzi ni kisa chenyewe, ambapo matukio yake yanafuatana kwa mtiririko. Wachawi wanne wanakutana na kumpendekezea mmoja wao atoe mtu kutoka kwa jamaa yake ili alipie

deni :

S Y N M, 19. 'Sasa hivi duru kwako
Utoe na wewe wako
Kutumai kwa wenzako
Wengi watakukimbia.

Pendekezo hilo linasababisha kupotea na kuuawa kwa mhusika Salima Binti Hanifu. Kwa ushirikiano wa serikali na wanakijiji, Nguvumali anaitwa ili atambue waliomuua mwanamke huyo. Wachawi hao wanne wanathibitishwa kuhusika katika kifo cha Salima na wanashikwa na polisi. Mmoja wao anafia hospitalini alikolazwa kutokana na mapigo ya polisi. S Y N M ni mgogoro kati ya wachawi na mganga maarufu kwa jina Nguvumali katika mashindano ya kuonyesha nguvu za kiajabu.

Sehemu ya tatu na ya mwisho ya utenzi huu ni kimalizio ambacho kina beti kumi. Katika sehemu hii, mtunzi anasema kuwa nguvu zake za kuendelea na utenzi huu zimedidimia na kama atazidi atafanya makosa mengi. Anaelezea asili ya kipawa chake cha utungaji ambacho alirithi kutoka kwa babu yake. Mtunzi anataja jina lake – Hasan bin Ismail (389). Anawaomba wasomaji wamwombee kwa Mwenyezi Mungu ili njia zake zinyooke na hatimaye aingie peponi katika siku ya kiama. Apendwe na watu. Anasema alizaliwa mjini Kilwa lakini amehamia mashambani.

Kama ilivyo ploti ya S Y N M, ploti ya M N M vilevile ni sahili lakini haitiririki ipasavyo kama tutakavyoona baadaye. Hata hivyo, kama ilivyo kaida ya tenzi nyingi, utenzi huu pia umegawika katika sehemu tatu kuu. Unaanza kwa utangulizi unaoendelezwa katika beti kumi na moja za

kwanza. Mtunzi anaanza kwa dua na kumwomba Mwenyezi Mungu amjalie neema ya kutunga kwa vile yeye hana ufahamu wa kutunga. Anaiomba hadhira yake kuwa ikiona kosa katika utenzi huu, imkosoe. Anaendelea kupendekeza kuwa utunzi huhitaji pahali patulivu na mtu mwenye akili timamu. Kisha anaomba baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu wa kuwataja Mitume wake pamoja na Mtume Muhammadi S.A. W ambaye anasema sifa zake hazihesabiki.

Sehemu ya pili ni kisa chenyewe ambacho kinaanzia ubeti wa 12 hadi 776. Tunaambiwa jinsi Mikidadi alivyokumbana na masaibu katika maisha yake lakini kwa majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, anayashinda. Kijana huyu anaanzia akiwa masikini sana lakini baadaye anafanikiwa na kuwa mkwasi.

Katika beti mbili za mwisho, mtunzi anahitimisha kwa kutaja jina lake - Said Abdalla Masud. Anasema kuwa hadithi hiyo ni juu ya vita vilivyofanyika Hijazi (Hejaz).

Hata hivyo, ploti ya utenzi huu haitiririki vizuri na kwa hivyo msomaji wake wakati mwingine anakanganyika. Kwa mfano, Mikidadi anapokutana na Ali na Hamza mara ya kwanza (242 – 273), anajulishwa majina yao na yeye anawaelezea masaibu yake. Anawafahamisha kilichomfanya kusafiri nchi za mbali kwenda kutafuta mali. Masahaba hawa wa Mtume Muhammadi S. A.W wanampa zawadi nyingi za ngamia na farasi kama mchango wa kulipia mahari. Hata hivyo, wanapokutana mara ya pili (285 – 639), Mikidadi hawatambui! Mikidadi anataka kuwanyang'anya taji la mkewe Ali ili ampe Mayasa. Vita vikali vinazuka kati yao na Mikidadi anashindwa. Jambo hili la kutojuana wanapokutana mara ya pili kiasi cha kupiagana

linaharibu muala wa ploti.

Tatizo lingine kama hili ni katika ubeti wa 180, ambapo Mikidadi anaonekana kama ni Mwislamu. Anapokutana na jinni, anasema dua yenye nguvu ambayo inafanya jinni atoroke. Kwa mujibu wa msimulizi, Mikidadi hapa hajapokea dini ya Kiislamu, bali anakuwa Mwislamu katika ubeti wa 631.

Katika uchunguzi wetu, tumegundua kuwa mtafaruku huu umesababishwa na mkusanyiko wa miswada ya tenzi tofauti tofauti aliyokuwa nayo mhariri wa utenzi huu. Mhariri huyo ambaye ni Abd Bashir Mchangamwe (1972 : iii) ,anakili kuwa

> *"Kadhalika nakili nilizopata zahitilafiana katika*
> *baadhi ya beti au mistari. Mimi sikuona kama*
> *ipo haja katika kazi ndogo kama hii kuonyesha*
> *tofauti zote zilizoko katika nakili."*

Kutokana na mhariri kuchukulia kuwa kazi ya kuhariri utenzi huu ilikuwa ndogo ndipo matatizo hayo ya muumano wa ploti yakatokea.

Tenzi hizo zimetangulizwa kwa neno **Bismillahi**. Hii ni kaida ya karibu kila tendi zilizotungwa na Waislamu au kutungiwa katika mazingira ya Kiislamu hata kama watunzi wake si Waislamu. Kama Kineene wa Mutiso (1996:60) anavyodai,

> *"Usilamu ni njia ya kuishi ya kila Mwislamu mahali popote alipo.*
> *Bali na dini ya Kiislamu, kitu kimoja kinachounganisha*
> *Waislamu mahali popote walipo ni lugha tunayoipata katika*

*Kuarani Tukufu, nayo ni Kiarabu."*

Kwa hivyo, tenzi hizi zina athari kubwa za Kiarabu pamoja na Uislamu.

## 3.6 MANDHARI NA WAKATI

Mandhari na wakati za tenzi za M N M na S Y N M zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Mandhari ya M N M ni ya kivita, dini, mapenzi na siasa. Mayasa anapotangaza sifa za mwanaume aliyetaka kuolewa naye, anatangaza vita dhidi yake. Anatoa masharti ya kupigana na yeyote ambaye angetaka kumwoa na mwanamume atakayemshinda ndiye angemuoa. Jambo hili linasababisha vita kati yake na waposaji.

Mikidadi anapomshinda Mayasa, anadaiwa mahari chungu mbovu. Mapenzi kati yake na Mayasa yanamfanya kutangaza vita dhidi ya matajiri wapita njia na kuwanyang'anya mali zao. Anaporudi na kupata mkewe ameolewa na mtu mwingine, anatangaza vita dhidi ya mtu huyo.

Mikidadi anapofungwa na kubebwa ili akauawe, Ali na Hamza wanatumwa na Mtume Muhammadi S. A. W kwenda kumwokoa kwa vita. Katika vita hivyo, watu wengi wanapoteza maisha yao lakini wanaokubali kuwa Waislamu, wananusurika.

Utenzi huu ulitungiwa katika mazingira ya dini ya Kiislamu. Mtunzi ameanza kwa dua. Mikidadi ametumia sala kama fimbo ya kujikinga na maovu, kwa mfano, anatumia dua kumfukuza jinni aliyekuwa anamkataza kunywa maji kisimani (179). Anapotekwa nyara na maadui zake, anamwagiza mama yake Tamina aombe dua (694). Mikidadi na Mayasa wanasilimu. Mikidadi anaposhikwa na kufungwa anamwambia mama yake

amuombee kwa Mwenyezi Mungu (694). Mayasa na Mikidadi wanaamua kwenda kushiriki katika vita vitakatifu pamoja na Mtume Mhammadi S.A.W (767). Jabir anapokataa kuwa Muislamu, anauawa kwa kukatwa vipande viwili (761). Malaika wanatumwa na Mwenyezi Mungu kuja kumletea Mtume Muhammadi S. A. W. ujumbe pamoja na Masahaba wake (704, 721).

Mandhari ya Kisiasa yanapatikana pale ambapo masultani wanapokuja kumposa Mayasa ambaye alikuwa mtoto wa Sultani. Hii ni katika jaribio la kudumisha uhusiano mwema kati ya nchi hizo. Masultani hawa walilindwa na majeshi, walikuwa na watumwa na raia wa kutawala.

Kisa hiki kilitungwa wakati wa uhai wa Mtume Muhammadi S. A. W. Mayasa na Mikidadi walikuwa marafiki na washirika wa Mtume katika vita vya jihadi.

Mazingira ya S Y N M ni ya kijamii na dini ya Kiislamu. Mtunzi anapinga na kushtumu uchawi na wachawi ambao walikuwa wanaangamiza watu katika jamii husika. Wahusika wanaishi kifamilia. Watu walikutana katika diro baada ya kukamilisha ramadhani. Walipokutana, waligundua Salima ametoweka na msako ulianza. Mhusika Salima na Binti Hanifu walikuwa dada wa toka nitoke. Salima alikuwa mavyaa yake Binti Ramadhani.

Katika tenzi hizi tunaona kuwa mazingira yanaafikiana na wakati. Kipengele cha wakati kimechangia sana katika kujenga taharuki na njozi juu ya yale yatakayotokea baadaye. Udhibiti mzuri wa wakati na mazingira huwezesha matukio kufanyika wakati nafasi yake inapotokea. Jambo hili

hutimia lau msanii atayapatia yale makuu wakati kwanza na ndipo yale mengine yafuatie. Mandhari na wakati katika tenzi hizi yanaoana hivi kwamba matukio yanatukia wakati na katika mazingira yanayofaa.

## 3.7 WAHUSIKA

Wahusika wengi wa M N M wamesawiriwa kama mashujaa wa kivita. Kuna Masultani ambao wana milki zao kama vile Sultani Kisiri, Sultani Riyahi, na wengineo. Masultani hawa wana raia wanaotawala, majeshi na watumwa.

Mashujaa wa kivita ni kama wahusika Mayasa, Mikidadi, Hamza, Mtume Muhammadi S.A.W. na Ali. Ijapokuwa hatujaonyeshwa Mtume Muhammadi S. A. W. akipigana vitani, amesawiriwa kama shujaa anayewaamrisha wafuasi wake, Ali na Hamza kwenda kumwokoa Mikidadi. Vilevile Mikidadi anapookolewa, anaamua kwenda kushirikiana na Mtume Muhammadi S. A. W. katika vita vitakatifu vya jihadi (767).

Mikidadi amekuzwa na mtunzi kama shujaa. Kama walivyomashujaa wengine duaniani, Mikidadi ana sifa za kiajabu ajabu. Kwa mfano, anatangulizwa katika utenzi kama kijana aliyekosa cha kurithi baba yake na kuwa masikini sana. Hii ni mojawapo ya sifa za mashujaa. Umaskini huu ulimfanya hata asiweze kuoa kwa sababu hangepata mali ya kulipia mahari (15). Vilevile yeye ni mtoto yatima kwa kufiwa na baba yake.

Umaskini unamlazimisha kuajiriwa kuchunga mbuzi na ngamia. Anajaaliwa kupata nafasi ya kupigana na kumshinda Mayasa. Kama walivyo mashujaa wengi, maisha ya Mikidadi sio mteremko. Anakumbana na masaibu na majaribu mengi. Anadaiwa mahari nyingi ili ashindwe kulipa na kwa hivyo

amkose Mayasa (147-152), mke wake anachukuliwa na kuozwa mtu mwingine (523), kutishwa na jinni (179), kutekwa nyara ili akauawe (690). Majaribio hayo ambayo yanamkumba mhusika huyu yanamjenga, kumkuza na kuthibitisha kuwa kweli yeye ni shujaa.

Kineene wa Mutiso (1999:27) anaunga mkono mawazo haya kwa kudai kuwa

> *"Jagina lazima ajaribiwe ili*
> *aweze kuthibitisha ujagina na*
> *vilevile utakatifu wake.*
> *Hajaribiwi mara moja tu bali*
> *maisha yake yote ni majaribio*
> *juu ya majaribio."*

Mikidadi ana sifa za kishujaa za kiajabu ajabu. Anapigana na kumshinda Mayasa aliyewashinda na kuwaua mashujaa wengi waliokuja kumposa. Anapigana na majeshi zaidi ya mia mara moja (299), mia nne (329) mamia ya watu (317), mia tano (286) na hata elfu moja (314) na kuwashinda. Anamkabili simba mkali mla watu an kumuua
(456). Mambo hayo siyo ya kawaida katika ulimwengu halisi. Hii ni mojawapo ya sifa za jagina kama anavyodai Kineene wa Mutiso (KHJ),

> *"Jagina apiganapo na maadui wake hupigana*
> *kijagina kweli kweli yeye haonekani mtu*
> *wa kawaida. Lolote afanyalo huonekana si jambo*
> *la kawaida, hata likiwa ni jambo dogo sana hata la*
> *kijinga!!"*

Mhusika huyu anawaua maadui zake ili apate mali zao. Anayekataa kumwachia mali anamwangamiza. Jambo hili linatiliwa nguvu na madai ya Kineene wa Mutiso (KHJ),

> " *Mara nyingi adui wa jagina ni kiumbe ye yote ambaye anamzuia kutekeleza lile jambo anuialo kulitekeleza. Adui huyo lazima aondolewe dunaini mara moja. Fauka ya hayo adui aweza kuwa ni kiumbe ye yote ambaye ana lengo sawa na jagina."*

Tunamwona Mikidadi akiwapiga na kuwaua waposaji wa Mayasa (85). Mikidadi anafunga safari na kwenda nchi za mbali ili kutafuta mali. Kama anavyodai Kineene wa Mutiso (KHJ),

> *"Safari hii ni ya kutoka mahali jagina alipozaliwa na kwenda katika sehemu au nchi jirani, ambako kuna watu au viumbe tofauti na watu wa jamii yake. Iwe ni safari halisi au ya kindoto huaminika ya kwamba ni safari ya kweli kabisa... katika safari hii jagina hujaribiwa pia."*

Mikidadi anajaribiwa pia. Motifu ya safari husaidia katika kumjenga na kumkuza jagina kwa kupata maarifa zaidi na elimu mpya. Hurudi nyumbani kama amebadilika kimawazo na hata kimwili. Mikidadi anarudi nyumbani akiwa amebadilika. Anajifunza na kupata ujuzi zaidi wa kivita, anapata taji na mali nyingi ajabu. Motifu ya safari imesaidia sana katika kujenga na kuendeleza ploti ya utenzi huu.

Wahusika wengine katika utenzi huu ni kama Jabir ambaye ndiye baba yake Mayasa. Uamuzi wake wa kumdai Mikidadi posa nyingi unasababisha visa vingi katika maisha ya Mikidadi.

Hatuoni uhusika wa Suwedi, ambaye ndiye baba yake Mikidadi. Yeye ametajwa tu kama mhusika aliyekuwa na mali nyingi sana lakini baadaye akafilisika na kufa maskini na kuacha jamaa yake ikiwa katika hali ya ufukara.

Turadi bin Annan ni mjombake Mikidadi. Alimwajiri Mikidadi kuchunga mbuzi na ngamia. Anampa Mikidadi farasi wa kwenda kupigana na Mayasa. Ni mtetezi wa Mikidadi anapodhulumiwa na Jabir (510). Anamtambua Mikidadi kama shujaa (513).

Mtume Muhammadi S. A. W. ni mhusika muhimu sana katika kisa hiki. Anawatuma washiriki wake kwenda kumwokoa Mikidadi. Utenzi huu ni juu ya mashujaa wa kivita na pia katika kupigania dini ya Kiislamu. Mtume Muhammadi S. A. W. ndiye mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika dini ya Kiislamu. Kama Olali (2004: 214) anavyodai, malengo katika maisha ya Mtume Muhammadi S. A. W. ni kutetea na kueneza Uislamu. Ushindi ulionekana usoni mwake, macho yenye upendo pamoja na jinsi alivyozungumza kwa njia ya kuvutia. Ukweli na nia yake njema ziliwavutia watu wengi kupokea Uislamu.

Ali, Abbas, Hamza na Fatuma.

Abbas ametajwa kama mshiriki na mfuasi wa Mtume Muhammadi S.A.W. Fatuma ni bintiye Mtume Muhammadi S.A.W. na bibi yake Ali. Abbas,

Hamza na Ali walimsaidia Mikidadi kwa mali ya kulipia mahari (265 – 272). Wahusika hawa ndio waliowashawishi Mayasa na Mikidadi kuwa Waislamu (631-632). Ali na Hamza walichangia pakubwa katika kumwokoa Mikidadi alipokuwa karibu kuuawa (743).

Mayasa ni mmoja wa wahusika wakuu. Yeye ni shujaa. Uhusika wake unachangia katika kuendeleza na kukunjua msuko wa utenzi huu. Yeye ndiye sababisho la matukio takribani yote katika utenzi huu. Kwa hivyo, mhusika huyu ni nguzo muhimu katika kisa hiki.

Wahusika wengine ni Waarabu na Masultani waliokuja kumposa Mayasa au kuandamana na waposaji. Kama vile, Abu Sufyana, Amir bin Omar, Hasan, Jeishi bin Amir, Abujahali, Hamtani, Khalid na Seleman. Walileta mali nyingi za kumposa Mayasa. Licha ya kuwa mashujaa wa kivita wa kutajika, walishindwa na Mayasa na wengine wakauawa. Hata hivyo, wengine kwa mapenzi waliyokuwa nayo kwa Mayasa, hawakupendelea kumhusisha katika vita (50). Walitaka kutoa mali na kumwoa. Alikataa mali zao na kwa hivyo wakalazimika kupigana naye. Walionusurika kuuawa walitoroka.

Mhusika Timima ni mama yake Mikidadi. Anafunga safari ya kwenda kwa Mtume Muhammadi S. A. W. kutafuta usaidizi wa kumwokoa Mikidadi.

Khamis ni mtumwa mwaminifu wa Mikidadi.
Jini ni mhusika ambaye anatisha Mikidadi kwa ndimi za moto anapoenda kisimani.

Kesi na Anasa ni mke na mumewe waliotekwa nyara na Sheikh Luhani.

Waliokolewa na Mikidadi na kugawiwa mali aliyonyang'anya Sheikh Luhani.

Sultan Kisiri. Aliyatuma majeshi yake kwenda kumshika / kumuua Mikidadi. Alikuwa na hamu ya kuona jinsi Mikidadi apiganavyo peke yake (375). Anapendezwa na kustaajabishwa na jinsi Mikidadi anavyopigana. Anampenda Mikidadi na kumpa mali nyingi sana pamoja na taji lake. Sultani huyu alikuwa na mkuu wa majeshi aliyeitwa Faswiha. Alishindwa na kutekwa na Mikidadi. Anapopelekewa Sultani, Sultani anakasirika na kuamrisha auawe (413). Waziri Mkuu wa Sultani Kisiri anayetambulika kama waziri, anafanya njama ya kumlisha Mikidadi simba lakini hakufanikiwa (448).

Malike bin Riyahi – anakubaliwa na Jabir kumwoa Mayasa (508). Anauawa na Mikidadi.

Katika utenzi wa S Y N M, wahusika wamegawanyika katika vikundi viwili. Safu ya kwanza ni wahusika waovu ambao ni wanachama wa kundi la wachawi. Nao ni Shambi Bin Dima, ambaye ndiye mkuu wa wachawi, Binti Jizi, Binti Hanifu na Binti Ramadhani. Wahusika hawa wamesawiriwa kama wachawi waovu, wakatili na wanafiki wakuu. Walimuua mhusika Salima kwa kumroga na kumtesa.

Kwa upande mwingine kuna wahusika wema. Wahusika hawa ni kinyume kabisa cha kundi la kwanza. Kwa mfano, Salima Binti Hanifu anayeuawa kinyama na wachawi hao. Mhusika huyu amesawiriwa kuonyesha uovu na ukatili uliotekelezwa na wachawi.

Bwana Mwenye ni mhusika aliyepiga ripoti kwa serikali juu ya kupotea kwa Salima (137). Yasin Kamina na Hamad Ramadhani ni vijana waaminifu waliotumwa na wazee kwenda kumwita Nguvumali ( 200, 201).

Liwali Selemani na Jumbe Bwana Hamisi ni watumishi wa serikali ambao walipokea ujumbe juu ya kupotea kwa Salima (146). Jumbe Hamisi anaamini mazingara. Anakiri kuwa mambo hayo si haramu kwao (170).

Bwana Komera na Bwana Kagendu ni baadhi ya wazee wa kijiji cha Panenenene walioshiriki katika harakati za kumtafuta Salima Binti Hanifu (165, 203).

Nguvumali ni mganga wa kiasili, aliyekuwa na kipawa na ujuzi wa kutoa uchawi chini ya jabali ukajulikana (294). Alisifika na kutambulikana na wananchi na hata serikali (303). Kwa mfano, alipowasili Ruvuja, Liwali aliandikia Makao Makuu ya polisi kuwaleta wachawi waliokuwa wameshikwa na polisi ili Nguvumali athibitishe kama ni wao wenye kumuua Salima (297). Anathibitisha kweli ndio hao kwa kutumia uganga wake.

Wahusika wengine ni Jaluo na Nyamwezi wanaowakilisha kikosi cha polisi katika kufanya uchunguzi. Wamesawiriwa kama wakatili. Wanawapiga watu vibaya mpaka wengine wanazirai.

Wahusika waliomo katika tenzi hizi ni wengi na wenye sifa mbalimbali kama tulivyoona hapo juu. Ni kaida ya tenzi kuwa na wahusika wengi wenye sifa tofauti. Wahusika hao wametekeleza majukumu yao na

kuchangia katika kufikia dhamira na maudhui ya watunzi hawa. Hivyo basi kama walivyo wahusika wa tendi zingine, wahusika hawa wamechukua nafasi muhimu katika kuendeleza ploti ya tenzi hizi.

## 3.8 TONI

Katika utenzi wa S Y N M kuna mseto wa hisia, hali ambayo inatupa mseto wa toni. Mnadhihirika aina nyingi za toni ambazo kimsingi zategemea aina ya mawazo yanayowasilishwa na mtunzi. Aina ya kwanza ya toni ni ile ya kunyenyekea mbele za Mwenyezi Mungu tunapoanza kusoma utenzi. Tunapata toni ya dua katika beti tatu za kwanza.

Kuna toni ya kutisha pale ambapo Binti Hanifu anapopewa masharti ya kumtoa mmoja wa jamaa zake. Anaambiwa kuwa akikosa kutimiza masharti hayo atakimbiwa na wenzake na kukosa faida alizokuwa anapata kwa kuwa mmoja wa kundi hilo (19).

Masharti haya ya kujitoa mwenyewe kama atamkosa mmoja wa aila zake yanatisha mhusika huyu na hata hadhira:

23. 'Awe mtoto wako
Ao ni ndugu yako
Isiwe jelani yako
Siye anayetakiwa.

40. 'Bint Hanifu mwambie
(H) apo atoe nduguye
Ao yeye afidie
Sisi tutampokea.'

Kiongozi wa wachawi, Bwana Shambi ana toni ya kuamrisha, kutishia na yenye matusi. Kwa mfano, katika ubeti wa 63, anatoa matamshi ya kumtisha Binti Ramadhani kwa kukosa kuandamana na wachawi wengine. Matusi anayotoa, na ambayo mtunzi hangeweza kuyanakili (90)

yanaonyesha kughadhibika kwa haraka kwa mhusika huyu.

Matamshi na tetezi za Salima zina toni ya unyenyekevu kama tunavyoshuhudia katika beti zifuatazo:

S Y N M:

104 . 'Mimi nalitumaini
Tukae wote nyumbani
Mwenzangu una undani
Kumbe ukinifanyia.'

110. 'Dada yangu waniua
Bila kisa kujua
Lakini utatambua
Zahani utaingia.'

Toni hii inazua huruma na masikitiko kwa msomaji dhidi ya mhusika huyu. Katika utenzi wa M N M, kuna toni ya kuamrisha, kukejeli, kusihi na za kusisimua miongoni mwa zingine. Kama ulivyo utenzi wa S Y N M, utenzi wa M N M umeanza kwa toni ya kunyenyekea ambayo ni dua.

Kuna toni ya kusihi, kwa mifano, beti 29, 37. Waposaji wanamsihi Jabir akubali mali zao ili wamuoe Mayasa. Katika ubeti wa 37, Jabir ni kama anasihi Mayasa akubali kuolewa na wangwana wenye vitu. Toni hii inaonyesha kuwa watu hao wenye mali ndio waliokuwa chaguo la Jabir la kumuoa bintiye Mayasa.

Katika beti za 109 na 110 pana toni ya mapenzi. Mayasa amejawa na mapenzi dhidi ya Mikidadi.
Katika ubeti wa 307 tunapata toni ya kuamrisha. Sultani Kisiri anawaamrisha askari wake waende wakachinje au kumshika Mikidadi wamletee.

Hiyo ni baadhi ya mifano ya toni zinazojitokeza katika tenzi hizi. Kutokana na mifano hiyo tunaweza kusema kuwa watunzi wa tenzi za M N M na S Y N M wametumia kunga za fani kwa ubunifu ambao unatuwezesha kupata toni za aina mbalimbali. Toni hizo zinatokea wazi katika mazingira waliyoteua na kwa namna inayogusa hisia za msomaji moja kwa moja na kuathiri usomaji wake kwa njia ya kujenga picha ya tukio linalohusika.

## HITIMISHO

Katika sehemu hii tumechunguza jinsi watunzi wa M N M na S Y N M walivyoteua lugha katika utunzi wao. Lugha katika tenzi hizi imeteuliwa kwa usanifu na kwa makini sana ili kutimiza malengo yake. Tumechunguza jinsi watunzi hawa walivyoteua lugha katika viwango vya kileksika, kifonolojia, kisemantiki na kisintaksia. Uteuzi na ukiushi wa lugha ndio mambo muhimu yaliyojenga fani ya kazi hizi. Fani yake imetuwezesha kujenga picha kamili mawazoni mwetu. Taswira hizo zinaafikiana na mandhari na wakati.

Kwa jumla tumeangalia vipengele vya fani vinavyojitokeza katika tenzi hizi ama kufaulu au udhaifu pamoja na uamilifu wake katika muktadha wa matumizi. Tumechunguza na kuonyesha jinsi kila mojawapo ya vipengele hivyo kinavyochangia katika kuendeleza maudhui na dhamira ya kila mtunzi. Vilevile tumechunguza wahusika na uhusika wao, mazingira yalimotungiwa, wakati na toni ya tenzi hizi.

# SURA YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### Utangulizi

Katika sura hii, tutaangazia muhtasari wa somo na matokeo ya utafiti wetu kwa ufupi. Tutajadili pia upimaji wetu wa nadharia tete pamoja na mapendekezo yetu.

## 4.1 Muhtasari Wa Masuala Muhimu

Katika tasnifu hii, tumeshughulikia fani ya tenzi za M N M na S Y N M Tumechanganua fani ya tenzi hizi kiulinganishi. Somo hili halijawahi kufanywa. Sura ya kwanza ya kazi hii ni utangulizi ambapo tumeonyesha vigezo tulivyotumia pamoja na njia tulizotumia kukusanyia data.

Katika sura ya pili, tumejadili dhana ya fani. Tumejadili juu ya uteuzi wa lugha na msamiati wake katika kubuni kazi ya kifasihi. Uchunguzi wetu umeegemea sana utanzu wa ushairi. Tumetanguliza kila mojawapo ya vipengele vya fani na kujadili uamilifu wake kwa mujibu wa wataalamu, wahakiki mbalimbali, pamoja na maoni yetu. Vipengele vya fani tulivyojadili ni kama vile, wahusika, ploti, matumizi ya lugha, toni, wakati, mandhari, mtindo na muundo.

Katika sura ya tatu, tumechanganua fani ya tenzi hizi na kuilinganisha. Tumechunguza uteuzi wa lugha katika viwango vya kifonoloja, kileksika, kisarufi na kisemantiki.

Msamiati uliotumiwa katika tenzi hizi sio mgumu kutamkika au kusomeka lakini baadhi yake kama ule uliokopwa kutoka Kiarabu ni mgumu kwa msomaji asiyekielewa Kiarabu. Aidha kuna matumizi ya Kiingereza (katika utenzi wa S Y N M, lahaja za Kiswahili, na Kiswahili Sanifu. Matumizi haya yanachangia katika hazina ya kileksika ya tenzi hizi. Katika kiwango cha fonolojia, tumeonyesha jinsi watunzi hawa wanavyofupisha, kurefusha na kubadilisha sauti za maneno. Vilevile baadhi ya maneno ya mkopo yamepewa fonolojia ya Kiswahili. Uteuzi wa msamiati, asili yake, uwezo wake, na aina ya msamiati huo zinachangia katika kuleta matokeo ya tamathali za usemi. Matokeo haya yanasababishwa na ukiushi wa lugha katika kiwango cha semantiki. Tamathali hizo zinachangia katika kuboresha tenzi husika na kuendeleza ploti yake. Kuna matumizi ya jazanda, usambamba, urejeshi pamoja na kuunga zingine zinazotuchorea taswira mawazoni.

Watunzi hawa wameteua na kuwaumba wahusika wao kwa namna inayotufanya kuona umuhimu wa uamili wao katika tenzi hizi. Kama ilivyo katika tenzi nyingi, wahusika wa tenzi hizi ni wengi. Aina ya mandhari ambamo wanajitokeza yanaafikiana na wakati pamoja na matendo yao. Hata hivyo, wahusika hawa hawajakuzwa sana kama walivyo wahusika wa kazi za kinathari kama riwaya.

Mandhari ya tenzi hizi inatofautiana sana kwa sababu zilitungiwa katika mazingira tofauti. Mandhari hutegemea aina ya wahusika, wakati na ujumbe unaopitishwa na kazi husika. Wahusika wake pia ni tofauti. Ploti yake ni sahili na inatiririka. Kama ilivyo kaida ya tenzi nyingi, ploti ya tenzi hizi imegawika katika sehemu tatu: Utangulizi, mwili na hitimisho.

Tenzi zote zimetumia lugha kwa ubunifu wa hali ya juu. Kila utenzi una matumizi ya maneno ya lahaja za Kiswahili. Mtunzi wa S Y N M ameteua msamiati wa Kiingereza ambao umefaulu sana katika muktadha wake wa matumizi. Msamiati wa Kiarabu vilevile umetumika katika tenzi zote mbili. Watunzi wa tenzi hizi wametumia uhuru wa mshairi katika uteuzi na matumizi ya lugha kwa jumla. Aidha wamerefusha, kufupisha na kubadilisha mpangilio wa sauti za baadhi ya maneno. Maneno mengine yaliyokopwa kutoka Kiingereza na Kiarabu yametumiwa vivyo hivyo bila kubadilisha umbo lake asilia.

Watunzi hawa wametumia tamathali za usemi katika kuboresha kazi zao kisanaa na kwa kuwasilisha ujumbe waliokusudia. Matumizi ya mbinu kama vile tashihisi na metonimia hayakujitoza katika utenzi S Y N M. Vilevile mbinu kama methali na onomatopeya hazikujitokeza katika utenzi wa M N M.

Wahusika katika utenzi wa M N M ni mashujaa wa kivita, Masultani, askari, raia na watumwa. Vilevile kuna viongozi wa kidini kama vile Mtume Muhammadi S.A.W. na Masahaba wake. Wasiokubali dini ya Kiislamu wanaonekana kuwa waasi. Kwa hivyo, wanaangamizwa. Vilevile wanaopinga Mikidadi katika harakati zake za kutafuta mali wamesawiriwa kama maadui z ake. Kuna mhusika jinni, anayemtisha Mikidadi kwa ndimi za moto. Wahusika hawa ni tofauti na wale wanaopatika katika utenzi wa S Y N M.

Wahusika wa S Y N M wamegawanyika katika vikundi viwili. Kuna kundi la wahusika waovu ambao ni wachawi na wahusika wema ambao

wanatatizwa na kundi lile la wachawi. Wachawi hawa wanatekeleza maovu kijijini. Jambo ambalo linahatarisha maisha ya wanakijiji. Serikali inaingilia kati ili kuwasaidia wanakijiji hawa kupigana na uchawi. Kwa hivyo, kuna maafisa wa serikali, askari pamoja na nganga maarufu kwa jina Nguvumali.

Tamathali za usemi kama vile, mbinu rejeshi na taharuki ni baadhi ya kunga ambazo zimetumiwa kwa ufanisi mkuu katika kukunjua na kuendeleza ploti ya tenzi hizi. Tofauti iliyopo katika tenzi hizi ni kwamba, ploti ya M N M ina masuala ambayo hayajitokezi vizuri na kwa hivyo yameharibu muumano wa msuko. Ploti yake imeathirika kama tulivyoonyesha katika sura ya tatu.

Toni zimedhihirika katika muktadha wake wa matumizi. Uwasilishaji wake unamfanya msomaji atambue aina yake, inahusu nani, nini, mazingira pamoja na wakati wake. Toni imejitokeza kupitia uteuzi wa lugha inayotumiwa na mtunzi au pale inapotumiwa na mhusika fulani. Toni huwa ni matokeo ya uambatanishaji mufti wa vipengele vyote vya fani.

Tasnifu hii imeonyesha kuwa licha ya kuwa na njia nyingi za kuelezea mtindo, hatimaye mtindo ni kipengele muhimu kinachoangazia jinsi lugha inavyotumiwa katika kuwasilisha mawazo. Tumeona ya kwamba hata kama mbinu za lugha ni chombo muhimu katika kazi ya kisanaa, hazijatosha kumwezesha mhakiki kufikia uchunguzi mkamilifu katika kazi fulani. Kwa hivyo mbinu zingine lazima zishirikishwe.

Mchango wa kazi hii ni kwamba, kwanza inaonyesha kuwa tenzi au kazi

yoyote ya kifasihi inaweza kuhakikiwa kiisimu. Pili, njia za mtunzi za kujieleza na ufanisi wa kujieleza kwa kutumia lugha kunategemea uwezo wake wa lugha pamoja na uasili wa lugha hiyo. Tumeonyesha kuwa jinsi mtunzi anavyoweza kutumia mbinu mbalimbali za lugha pamoja na za utunzi ndivyo anavyoweza kuwasilisha mawazo yake kwa njia ya ubunifu na ufanisi zaidi. Kwa njia hii, msomaji huweza kuvutiwa na hivyo kuwa na ufahamu wa kina wa kazi husika.

Wasanii wa tenzi hizi wametumia fani kwa namna ambayo inamruhusu mhakiki kuchanganua vipengele vyake na kutathmini uamilifu wa kila mojawapo. Kwa sababu hii, tumechunguza kila mojawapo ya vipengele hivyo kivyake.

## 4.2 Upimaji Wa Nadharia Tete

Tasnifu hii imeshughulikia fani ya tenzi za M N M na S Y N M. Tumetoa maoni yetu kuhusu matumizi ya fani katika tenzi hizo. Tumeangalia uamilifu, ama udhaifu au ufanifu wa kila mojawapo ya vipengele vya fani.

Katika uhakiki wetu, tulidhamiria kuthibitisha haipothesia tatu. Kwanza, tulitaka kujua kama uteuzi na matumizi ya vipengele vya fani vilivyotumiwa katika tenzi hizo, ama ufanifu au udhaifu pamoja na uamilifu wake katika matumizi. Tumeweza kubainisha kwamba nadharia hii ina ukweli. Fani ya tenzi hizi imeteuliwa kutokana na muktadha wake wa matumizi. Tumeonyesha ama udhaifu au ufanifu wa kila mojawapo ya vipengele vya fani.

Nadharia tete yetu ya pili ilikuwa kufanana kwa fani ya tenzi hizi licha ya

kutungiwa katika mazingira na nyakati tofauti. Tathmini yetu imeweza kubainisha kuwa nadharia hii kwa kiasi kikubwa ina mashiko. Hii ni kwa sababu vipengele vya fani vinavyojitokeza katika tenzi zote mbili vimetumiwa kutimiza malengo sawia. Kwa upande mwingine, nadharia hii inakanushika kwa maana kwamba kuna vipengele vya fani vinavyojitokeza katika utenzi mmoja na kukosekana katika utenzi mwingine. Vilevile mtunzi wa utenzi wa S Y N M ameteua msamiati wa Kiingereza ambao haupatikani katika utenzi wa M N M. Mambo hayo mawili yanaelekea kukanusha nadharia hii.

Nadharia yetu ya tatu ilikuwa, uteuzi wa msamiati na tamathali za usemi katika tenzi hizi umefanywa kwa malengo maalum. Uchunguzi wetu umethibitisha nadharia hii kuwa kweli. Tumechanganua matumizi ya lugha kwa ujumla na kuthibitisha uamilifu wake katika kazi husika.

Tumetumia nadharia ya ufani katika uchunguzi wetu. Tatizo tulilokuwa nalo ni kwamba nadharia hii haishughulikii athari ya kazi ya kifasihi kwa msomaji wake. Tumelazimika kuvuka mpaka huu na kushughulikia athari inayosababishwa na uteuzi wa lugha katika tenzi tulizohakiki. Hii ni kwa sababu hatungeweza kuonyesha uamilifu, ufanifu au udhaifu wa fani hiyo bila kuangazia athari yake kwa mpokeaji ambaye ni msomaji.

## 4.3 Mapendekezo

Kulingana na upeo na mipaka ya kazi yetu, hatukuchunguza suala la maudhui. Kama tulivyotaja hapo awali hatungeweza kuzungumzia fani bila ya kugusia masuala yanayojitokeza kwani fani hubeba maudhui. Kwa mintarafu hiyo, tumegusia maudhui kwa kupita tu wakati tulipokuwa tunafafanua mbinu mbalimbali za kifani. Kwa hivyo, tungependekeza

wahakiki wazifanyie tenzi hizi utafiti wa maudhui.

Kutokana na utafiti tulioufanya, tumegundua kuwa fani ya tenzi za M N M na S Y N M ni pana mno. Vipengele vingine kama usimulizi tumevichunguza na kuvitathmini kwa mipaka ya wakati mfupi tuliokuwa nao. Usimulizi ni kipengele ambacho kinaweza kuchukua muda wote huo tuliotumia katika kushughulikia somo hili. Hili pia ni pengo ambalo linahitaji kuchunguzwa.

Msamiati wa Kiarabu uliopo katika utenzi wa M N M pamoja na wakati wa kisa hicho zinatufanya kushuku kuwa utenzi huu ulitarjumiwa kwa Kiswahili kutoka asili yake ya Kiarabu. Jambo hili linahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M.H. (1968). "A note on the form of the language of the poem" katika Lienhardt, P. (Ed. 1968). *The Medicine Man*. Oxford: Clarendon press uk: 81-83

___________ (1979). *MUYAKA: 19th Century Swahili Popular Poetry.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abrams, M. H. (1957). 3rd Ed. *A glossary of Literary Terms*. New York: Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Allen, J.W.T. (1971). *Tendi.* Nairobi: Heinemann.

Allingham, P.V. (2005). "The Victorian Web: Literature, history and culture in the age of Victoria." Canada Lakehead University. Makala hii inapatikana katika http://www.google.com/

Bakari, M (1978). *"The state of the Art: Swahili Literature in the Nineteenth Century."* Assembly of Kenya Annual Conference Journal.

Bashir A.. (Ed. 1972) *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Nairobi: Heinemann Educational Books (E.A.) Ltd.

Harries, L. (1962). Swahili Poetry. New York: Oxford University Press.

Hichens, W. (1941). "Swahili Prosody" Katika *Swahili Journal of the East Africa Swahili Committee.* Vol. 33.

Kazungu, E.K. (1982). "Deviation and Foregrounding in chosen Swahili literary Texts. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi." (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1983). "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili" katika *Makala za semina ya Kimataifa Ya Waandishi wa Kiswahili III : FASIHI.* Dar-es-Salaam: TUKI.

Kitsao, J. (1975) "A stylistic Approach Adopted For the Study of Written Swahili Prose Texts. *Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi."* (Haijachapishwa)

Knappert, J. (Ed.1964). *Four Swahili Epics.* Supplement to Journal 35/2.

____________ (1979). *Four Centuries of Swahili Verse.* London: Darf Publishers Ltd.

Kuvuna, S.M, Mvati, M.N. na Maliachi, P.A. (1992). *Nuru ya Ushairi: Mwongozo na Uchambuzi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Leech, G. N. & Short, M. (1981). *Style in Fiction*, New York: Longman.

Lienhardt, P. (Ed.1968). *The Medicine Man*. Oxford: Clarendon press.

Masoko, D.L.W. na Mdee, J.S. (Wah... 1984). "Msamiati wa Muda wa Fasihi" katika *Mulika Nambari 16*. Dar-es-salaam: TUKI

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta foundation.

Ochoi, P.O. (1998). "Uchanganuzi Kimitindo wa Ushairi wa Al-Amin Mazrui. Shahada ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi" (Haijachapishwa)

Olali, T.M. (2004). "The Veneration of the Prophet: The role of *Kasida ya Hamziyyah* during the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya: School of Oriental and African Studies University of London." (Haijachapishwa)

Osiemo, D.O. (1997). "Fani katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa *Upisho wa Malenga na Difina ya Umalenga.* Chuo Kikuu cha Nairobi - tasnifu ya M.A." (Haijachapisha).

Oxford (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press

East Africa Ltd.

Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi.* Dar-es-salaam: Press and Publicity.

Shariff, I.N. (1988). *Tungo Zetu.* Trenton: The Red Sea Press, Inc.

Syambo, B. na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi Nairobi*: East African Educational Publishers.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Wales, K. (1989). *A Dictionary of Stylistics*. London: Longman.

wa Mberia, K. (1987). "Ushairi: Kunga za Utunzi (Mswada)" Chuo Kikuu cha Nairobi.

__________ (1989). "Fumo Loyongo" katika *Mulika Na. 24*. Dar es Salaam: TUKI

__________ (1997a). *Natala*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

__________ (1997b). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

__________ (2000). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Wamitila, W.K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

__________ (2003a). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

__________ (2003b). *Mwongozo wa Walenisi.* Nairobi: Focus Books.

__________ (2003c). *Kichocheo Cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Books.

wa Mutiso, K. (1985). "Hurafa na Uyakinifu katika *Hamziyyah.* Nairobi: Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi" (Haijachapishwa).

__________ (1996). "Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: *Kasida ya Burudai.* Tasnifu ya Ph.D: Chuo Kikuu Cha Nairobi." (Haijachapishwa)

__________ (1999). "Sira ya Majagina: Buddha na Muhammadi." Mswada uliowasilishwa katika Semina, Swahili Kolloquism, Universität Bayrenth, Mei 14-15, 1999.

__________ (2002). "The Epic of Princess Fatuma." (mswada)

__________ (2003). "The Epic of Secret of All Secrets."( mswada)

__________ (Mha...2005). Utenzi wa Hamziyyah. Dar es Salaam: Tarsisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Werner, A. (1932). The story of Miqdadi Na Mayasa, Hamphshire: The Azania Press.